



UNIVERSITE NATIONALE DU RWANDA  
FACULTE DES LETTRES

**NADHARIA YA KIFUNGAMANO  
KATIKA MAANDISHI  
YA E. KEZILAHABI**

Mémoire de Licence en Langues  
et Littératures Africaines (L.L.A)  
présenté par  
Balthazar NDUWAYEZU

Directeur : Nathanaël O. MMBAGA

RUHENGARI, JUIN 1985



UNIVERSITE NATIONALE DU RWANDA  
FACULTE DES LETTRES

**NADHARIA YA KIFUNGAMANO  
KATIKA MAANDISHI  
YA E. KEZILAHABI**

Mémoire de Licence en Langues  
et Littératures Africaines (L.L.A)  
présenté par  
Balthazar NDUWAYEZU

Directeur : Nathanaël O. MMBAGA

RUHENGRI, JUIN 1985



Ukiiona taa linang'aa  
ujue kuwa mafuta ndiyo  
yanalipepetea.

Kwa Baba na Mama  
Kwa wadogo na dada zangu  
Kwa rafiki yangu Muhayimana Télesphore

Kwangu nlikuwa mafuta ya taa.

William W. ...  
...  
...



## SHUKRANI

Katika kazi hii watu wengi walinisaidia, nami ninataka kuwashukuru sana kwa msaada walionipa kwa hisani yao.

Shukuru za pekee zimwendee mwalimu N.O. MMBAGA ambaye maonyo na mashauri yake yenye maarifa yaliongoza sana kazi hii tangu mwanzo hadi mwisho.

Ningependa pia kuwatolea shukrani walimu G. MHECHELA na B. MWAFYELA ambao waliniingiza na kunifuata hatua kwa hatua katika ujuzi wangu wa lugha ya Kiswahili.

Tena wanafunzi watangulizi wa Idara ya Lugha na Fasihi za Kiafrika tuliojifunza pamoja washukuriwe kwa mathubutisho yao imara.

Kwa MUJYARUGAMBA J.D., KAYITESI M.G. kwa misaada yao isiyo na kifani; pamoja na wale ambao hawakuchoka kunitia moyo, nasema

AHSANTENI !



## O. UTANGULIZI.

### O.1. Madhumuni ya kazi.

Nilichagua kuchambua nadharia ya kifungamano kwani yajitokeza katika maandishi ya kiafrika kabla na hata baada ya uhuru kupatikana. Msimamo huu pia hujitokeza katika baadhi ya kazi za Fasihi-andishi ya Kiswahili, mojawapo ikiwa ni kazi za E. KEZILAHABI.

Mwanzoni nilikusudia kuchambua ufungamano wa kisiasa katika riwaya za Kiswahili kwa jumla. Kwa mfano maudhui ya kisiasa katika riwaya za Kiswahili kama vile jukumu la viongozi wa kisiasa, ukoloni, uhuru, unyonyaji, ukoloni mamboleo na mengineyo. Lakini baadaye nikaona kuwa kazi hiyo ya kuyakabilia maandishi ya Kiswahili itakuwa pana sana na itahitaji muda mrefu. Pia ukosefu wa vitabu vyenyewe ukanizua. Zaidi ya hayo, kazi hiyo ilikuwa inataka ujuzi zaidi katika taaluma ya Fasihi-linganishi. Basi nikaamua kufanya uchambuzi katika uwanja mdogo, lakini wenye mtazamo kamili juu ya maudhui ya kifungamano kama yajitokezavyo katika maandishi ya Kiswahili.

Ilinibidi kutumia vitabu ambavyo niliweza kupata. Niliposoma vitabu vya Kiswahili vilivyokuwamo maktabani, riwaya moja ilinivuta. Na riwaya hiyo ni Gamba la nyoka, kitabu kilichoandikwa na Euphrase KEZILAHABI. Kitabu hicho kinazungumzia juu ya siasa ya ujamaa na matatizo ya ujenzi wa jamii mpya. Kitabu kimoja tu hakitoshi kuzingatia kikamilifu ufungamano wa mwandishi. Kwa hiyo nikaamua kuchambua vitabu vyake



vingine viwili ambavyo ni Kichomi (diwani ya mashairi) na riwaya ya Rosa Mistika. Kwa hiyo kazi itakuwa ya kuchambua nadharia ya kifungamano katika maandishi ya KEZILAHABI kwa kutumia vitabu hivi vitatu tu.

### 0.2. Umuhimu wa kazi.

Ufungamano unaangalia uwiano ulioko baina ya mwandishi, kitabu na jamii. Kusudi la kwanza katika kazi hii, ni la kuchambua uhusiano kati ya kitabu na jamii ya mwandishi, na jinsi mwandishi anavyoendesha ufungamano wake katika maandishi yake. Kazi hii ni ya kwanza kufanyika chuoni humu tangu Kiswahili kishughulikiwe nchini Rwanda. Hivi matatizo kadhaa yatanikabili : zaidi ya lugha yangu kuwa changa, hakuna kazi za uchambuzi wa maandishi ya kiswahili ziwezazo kunisaidia hasa kwa sababu maktaba ya chuo bado ni maskini katika maandishi ya Kiswahili. Hata hivyo, nadhani kuwa kazi hii itaweza kuwasaidia wale watakapo kushughulikia fasihi ya Kiswahili. Tena wakati umefika wa kuishughulikia fasihi ya kiafrika katika lugha za kiafrika. Hivi kazi hii, licha ya kuwa na nia ya kukuza na kuieneza lugha ya Kiswahili, itawapa hamu wasomaji, hasa wasomaji wanyarwanda, kushughulika na fasihi ya Kiswahili ambayo iko karibu nao badala ya kuzikimbilia fasihi za ng'ambo. Kwani yatubidi siku hizi kujua jinsi wenzetu waafrika wanavyofikiri ikiwa mazingira ya kiafrika yanalingana kwa kiasi fulani. Pia kazi hii itaweza kuwasaidia walimu na wanafunzi katika ujuzi wao wa kukuza taaluma ya fasihi ya kiafrika.

### 0.3. Mdini za uhakiki.

Kazi hii ambayo itahusishwa na nadharia ya kifungamano ikizingatia maandishi ya KEZILAHABI ni ya uhakiki. Kuna



mbinu nyingi za uhakiki ambazo zinaweza kutumiwa katika uchambuzi wa kazi hii. Kabla ya kuzieleza na kuchagua mbinu inayofaa, yatupasa kutupa jicho juu ya swali la kujua mbinu zinazolandana na fasihi ya kiafrika. Ikiwa fasihi ya kiafrika ni ya pekee kutokana na historia ya Afrika yenyewe, wataalam mbalimbali washughulikao na fasihi ya kiafrika, walishikwa na haja ya kutafuta mbinu maalum zinazofaa katika uchambuzi wa kazi za fasihi ya kiafrika.

Kuna hoja inayodai kwamba maandishi ya kiafrika yohakikiwe na waafrika wenyewe. Msimamo huu ulijitokeza hasa katika Baraza la kwanza la kimataifa la maandishi na wasanii weusi lililofanyika huko SORBONNE, Ufransa mwaka 1956. Katika baraza hilo ilionekana kuwa hakuna mtafiti mgeni mwenye uwezo wa kugundua uzuri, mvuto na kufufua siri za fasihi ya kiafrika; kwani wahakiki wasio waafrika wanazo nia zao ambazo zinawazuia kuhakiki vilivyo hisi zilizomo katika sanaa za kiafrika. Inasemekana kuwa wahakiki hao hawana nadharia sahihi na mtazamo unaofaa juu ya maandishi ya waafrika kwani hawajui mazingira ya kiafrika, jambo ambalo linawazuia kutoa uchambuzi unaofaa. Tena wageni hao wanatumia mbinu ambazo hazifai katika uchambuzi wa kazi za kiafrika kwa sababu mbinu hizo zimetokana na nadharia ambazo misingi na mazingira yake tofauti na yale ya Afrika.



Uelekeo huo ulikuwa na nia ya kumfanya mwafrika mwenyewe atoe mbinu sahihi za uchambuzi zinazolandana na mazingira ya kiafrika. Msimamo huo waweza kueleweka kama tukiweka katika mazingira na wakati wake yaani wakati wa uzalendo ambapo mwafrika alitaka kujiepusha moja kwa moja na mambo yote ya kigeni. Baraza hilo lilisahau kuwa kazi ya sanaa ina ujumbe fulani ambao hauna budi kuwasilishwa mbele ya hadhira fulani.

Msimamo wa pili ni wa SENGHOR (1) ambaye anasema kwamba kinachotambulisha sanaa za kiafrika ni maono na mtindo maalum. SENGHOR anazingatia uhakiki ni kufuata kanuni. Ni kusema kwamba mchambuzi atatafuta katika kazi anayoihakiki; na akizikosa au akishindwa kuzitoa, basi atakuwa amefanya uhakiki mbaya. Uelekeo huu haufai kwani unamfanya mwafrika katika ulimwengu wa ki-kale na usiobadilika.

Msimamo mwingine unajitokeza katika Baraza lililowakusanya waandishi waafrika katika lugha ya kiingereza lililo-



fanyika Kampala mwaka 1962. Katika mazungumzo ya wataalamu walitoa kanuni mbili zinazotambulisha kazi za kiafrika: mtindo wa pekee na lugha ya pekee ambayo ni kiingereza (au kifransa) cha kipidjin. Msimamo huo hautofautiani na ule wa kina SENHOR. Tena msimamo huu unasahau maandishi yanayotumia lugha za kiafrika.

Baadaye kulitokea mikutanoni mingi ya wataalamu wa fasihi ya kiafrika ambayo yote ilikuwa ikitoa haja ya kuwa na mbinu maalum za uchambuzi wa maandishi ya kiafrika. Ni navyoona mimi ni kwamba mbinu hizo sio za lazima, kwani ni kufinya sanaa za kiafrika katika sheria na kanuni ambazo hubadilika kufuatana na wakati, kazi zenyewe, na msimamo wa wahakiki. OKONDA OKOLO anasema hivi kuhusu swali hili:

"Kutafuta uhakiki wa kipekee wa kazi za kiafrika ni kupinga taaluma ya uhakiki ambayo ni ya kisayansi."

Anaendelea kusema kuwa "hakuna na haiwezekani kuwa na mbinu

maalum za kiafrika katika taaluma ya uhakiki. Hakuna mbinu za kisasa za uhakiki ambazo haziwezi kutumika katika uchambuzi wa kazi za kiafrika. Kama mazingira halisi ya kiafrika yanatufanya tutoe mbinu mpya na za kisayansi, mbinu hizo hazina budi kutumika katika uchambuzi wa fasihi nyingine, na kutumiwa na wachambuzi wasio waafrika". (2)

Katika kutoa mbinu maalum zinazofaa kuchambua tu kazi za kiafrika ni kukanusha hali ya kisayansi ya taaluma ya uhakiki. Jambo la muhimu ni kusoma mwandishi, na kutokana na ujuzi wa uhakiki mwenyewe, kutoa mbinu inayofaa. Na hii si kusema kwamba mbinu itakayochaguliwa itakuwa ya pekee katika kuchambua maandishi yanayohakikiwa. Mbinu nyingine zaweza kuaidia kutoa maana na mwanga zaidi. Kama nilivyosema juu, kuna mbinu nyingi za uhakiki. Kuna uhakiki wenye kanuni (dogmatic criticism) ambao nia yake ni kutoa sheria maalum za uzuri wa kuchambua kufuatana na kanuni hizo. Uhakiki huu unachambua kitabu bila kumchunguza mtungaji wala kumhusisha na wakati,



mahali na jamii ambamo kazi ya sanaa inatokea. Mbinu nyingine ni ile ya kimaelezo (explicative criticism). Hapa mhakiki, kabla ya kuthamini kazi ya sanaa, anaingia moja kwa moja katika kuifafanua. Kazi inafafanuliwa kutokana na maisha ya mtunzi mwenyewe. Tena mbinu hiyo huhusisha kazi na hali ya jamii; na inakubali kuwa uzuri wa sanaa unaweza kupatikana katika fani mbalimbali. Halafu kuna uhakiki wa kimatokeo (impressionist criticism) ambao unathamini kazi kufuatana na matokeo ya kazi. Hapa LEMAITRE anasema : "Hatupendi kazi za kiakili kwa sababu ni nzuri, lakini zinakuwa nzuri ikiwa tunazipenda."(3)

Katika kazi hii nimechagua kutumia mbinu ya kisosholojia kufuatana na mwelekeo wa kazi zenyewe ambazo zina uhusiano na nadharia ya kifungamano. Fasili ya uhakiki wa kisosholojia ndiyo itakayothibitisha matumizi ya mbinu hiyo katika kazi kama hii. Wataalam wengi (4) wanakubaliana kuwa msingi wa uhakiki wa kisosholojia ni kwamba kila kazi ya sanaa ni kioo cha jamii, maana jamii ndiyo izaayo kazi ya sanaa. Hivi uhakiki huo utashughulikia hasa uwiano uliokobaina ya jamii na kazi ya fasihi. Mbinu hii ya kisosholojia inaweza kugawanywa katika mafungu matatu : bourgeois criticism, Marxist criticism na socio-criticism.

#### 0.3.1. Bourgeois criticism.

Njia hii ina mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza unaeleza na kufafanua kitabu ukihusisha yaliyomo na mwandishi na ukionyesha jinsi mtunzi alivyoathiriwa na mazingira yake mwenyewe kama vile familia yake, masomo yake, safari zake, kazi yake n.k. Mtazamo wa pili unachambua maandishi ukitazama yaliyomo na jinsi yalivyoathiriwa na mazingira bila kuainisha jamii katika matabaka yenye kupambana. Ninaona kuwa ule mtazamo wa kwanza haufai kama mbinu ya uhakiki, kwani athari ya mwandishi mwenyewe juu ya maandishi ni mtazamo wa kuyaangalia maandishi kama kioo cha mtu mmoja. Kutazama familia, masomo, kazi na mengineyo yanayomhusu mtungaji ni kumhusisha mwandishi kuliko jamii



aishimo. Mtazamo wa pili nao haufai kwani unatazama jamii kwa-jumla, tena mtazamo huo ni wa juujuu na hauziingilii kwa unda-ni zaidi shughuli za jamii. Hivi uhusiano wa mwandishi na jamii haukamiliki kama maisha yote ya jamii hayakusishwi.

### 0.3.2. Marxist criticism.

Mbinu hii inamweka mwandishi katika jamii inayoongo-zwa na mapambano ya kitabaka. Inatafuta maelezo katika mapamba-no hayo, hata kama maandishi hayahusiki moja kwa moja na mapa- mbano hayo. Uhakiki huo unatazama yaliyomo kuliko fani. Mbinu hiyo yajitokeza katika vigezo avitoavyo RUMBU-a-KAYIMBU katika makala yake (5).

1. Kujua kwa undani maandishi.
2. Kuchunguza mambo katika mabadiliko na hitilafu zake na kutafuta maelezo humo humo.
3. Kuangalia kwa makini yaliyomo, kuyachambua bila kutazama mambo ya jamii.
4. Kuangalia wahusika wakuu (mashujaa) wanaoendesha hadithi katika kitabu na kuwaweka katika tabaka fulani la jamii.
5. Kisha ainisha wahusika katika matabaka, mhakiki anatakiwa kutafuta misingi ya kiuchumi na njia zote za uzalishaji mali zinazotumika katika ri- waya.
6. Kutafuta itikadi inayojitokeza katika ufafanuzi wa mawazo, hisi na fikra za mwandishi, pamoja na athari yake kwa msomaji.
7. Kujua mambo kikamilifu ili kuyazungumzia vilivyo.
8. Kueleza mwishowe kazi ya maandishi hayo, kama ni kuchongea au kusifu.

Njia hii yaweza kutumika katika riwaya lakini haiwezi kufaa katika diwani ya mashairi.



### 0.3.3. Socio-criticism.

Mbinu hii inatilia mkazo katika uwiano wa maandishi na ukweli wa mambo kama yajitokezavyo katika jamii inayohusika. Licha ya kushughulika na yaliyomo, mbinu hii huangalia pia fani. Mbinu hii inatazama yanayozungumzwa na jinsi yanavyozungumzwa. Kama asemavyo SARTRE, "kuwa mwandishi sio kuchagua kuyazungumzia mambo fulani, lakini kuchagua namna fulani ya kuyazungumzia."(6)

Njia hii ingefaa kwa kazi hii, lakini kuna ukosefu wa vitabu vinavyoeleza mbinu hii kwa undani, na ukosefu wa kazi za uchambuzi zilizoitumia. Kwa hiyo nilionelea kuunganisha njia hii na ile ya kimarx kutaleta mafanikio zaidi. Ni kusema kwamba kutakuwa na kazi ya kutoa mihtasari ya vitabu kwa kuangalia jinsi wahusika wakuu wanavyoendesha visa na itikadi inayojitokeza katika mawazo ya mwandishi. Ili kuwa na mtazamo kamili juu ya uwiano wa maandishi na ukweli wa mambo, itabidi kupitia jamii aishimo mwandishi yaani TANZANIA. Uwiano huo utazingatiwa zaidi kwa kufafanua dhamira anazozizungumzia KEZILAHABI katika kazi zake. Ingefaa tena kutafuta jinsi mwandishi anavyoweza kuwaathiri wasomaji, lakini kazi hii inataka uchunguzi na kuishi katika jamii ya mwandishi ili kugundua mabadiliko yaliyotokea. Kinachoweza kufanywa ni kuchunguza matatizo anayoyazungumzia mwandishi na masuluhisho anayoyatoa. Hivi vitabaki vidokezo vifuatavyo :

1. Kuyajua maandishi.
2. Kufafanua jamii kama ijitokezavyo katika maandishi.
3. Kutenganisha jamii hiyo na jamii ya Tanzania.
4. Kutafuta itikadi inayojitokeza katika maandishi hayo.

Kwa kufanya hivi tutaweza kuzingatia vipengele vya kifungamano katika kazi ya mwandishi.



Hatuwezi kuzungumzia nadharia ya kifungamano katika maandishi ya KEZILAHABI bila kujua ufungamano ni nini, na jinsi nadharia hiyo inavyojitokeza katika fasihi ya kiafrika kwajumla, na ya Kiswahili hasa. Ni kusema kwamba sura ya kwanza itazungumzia maana ya nadharia ya kifungamano, nadharia ya kifungamano katika Afrika, na katika Afrika ya Mashariki, ili kumweka KEZILAHABI katika fungu fulani la maandishi wa kiafrika. Halafu, mbinu iliyochaguliwa yaani uhakiki wa kisosholojia utabidi uzingatie hali ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi ya jamii ya Tanzania ambayo ilimzaa mwandishi, kadhalika maandishi yake. Hivi sura ya pili itakuwa ya kujua jamii na maandishi ya Kezilahabi. Baadaye tutaifikia sura muhimu ambayo inahusu dhamira kuu za kazi za Kezilahabi. Dhamira hizo zitachambuliwa katika kitabu kimoja hadi kingine. Sura hii ndiyo itakayoonyesha ufungamano katika maandishi ya Kezilahabi yaani msimamo wake na masuluhisho anayoyatoa. Na mwisho tutakuwa na hitimisho ambalo litazingatia mapendekezo na maoni yangu binafsi. Kwa kifupi sura zitapangwa kama ifuatavyo :

- I. Nadharia ya kifungamano na fasihi ya kiafrika.
- II. Jamii na maandishi ya Kezilahabi.
- III. Dhamira katika maandishi ya Kezilahabi  
Hitimisho.



Tanbihi.

- (1) SENGHOR, L.S., Liberté I : Négritude et Humanisme, Seuil, Paris 1964.
- (2) "L'idée d'une critique spécifiquement africaine ne va-t-elle pas à l'encontre de la critique, entendue comme une discipline scientifique ? [..]. Il n'existe pas et il ne peut exister des méthodes spécifiquement africaines de critique littéraire. Et il n'est pas de méthodes actuelles d'analyse critique de textes qui ne puissent être appliquées aux productions littéraires africaines. Et même si le contexte spécifique nous amène à découvrir de nouvelles méthodes scientifiques, elles doivent être applicables à toutes les autres littératures du monde, et par des critiques non-africains".
- OKONDA OKOLO, "Herméneutique et Problématique de la critique littéraire" in La sémiologie et la littérature africaine, Actes du séminaire tenu à Lubumbashi, Mars 1977, Edité par le Centre d'Etudes et de Littératures Africaines (CELA).
- (3) "Nous n'aimons pas les oeuvres de l'esprit parce qu'elles sont bonnes, mais elles sont bonnes quand nous les aimons."
- LEMAITRE, akikiriwa na DOUTREPONT, C., La composition et les genres littéraires, Namur, 1965, uk 237.
- (4) RUMBU-a-KAYIMBU, "Problématique de la critique littéraire contemporaine." in La sémiologie...op.cit.
- ZERAFFA, M., Roman et société, coll. sup., P.U.F., Paris 1976.
- GOLDMANN, L., Marxisme et sciences humaines, coll., Idées, Ed. Gallimard, Paris 1970.
- FAYOLLE, R., La critique, coll. U. Armand Collin, Paris 1978.



- (5) RUMBU-a-KAYIMBU, Taz. makala iliyokiriwa juu.
- (6) "On n'est pas écrivain pour avoir choisi de dire certaines choses, mais pour avoir choisi de les dire d'une certaine manière."

SARTRE, T.P., Qu'est-ce que la littérature ? Ed. Gallimard, Paris 1949, uk 34.



1. NADHARIA YA KIFUNGAMANO YA FASIHI YA KIAFRIKA.

1.1. Nadharia ya kifungamano.

Kufuatana na mwelekeo wa ufungamano, kuna fasili na hata dhana tofauti kidogo kuhusu jambo hilo. Haitawezekana hapa kutoa fasili zote walizozitoa wataalam mbali mbali. Bali jambo hili litazungumziwa kwa ujumla kutokana na niliyoyasoma, na kukiri maoni ya wataalamu wengine.

Kwa kawaida, kufungamana ni kushikamana, yaani kuwa katika hali ya kushikana sana na kitu au jambo fulani. Pengine huweza kufasiliwa kama kujipa masharti au kupeana maagano na mtu fulani juu ya jambo fulani. Ufungamano ni amali inayomshirikisha mtu na jambo fulani. Na yampasa mtu anayefungamana na jambo fulani kuyatimiza makusudi aliyejipa. Pengine, neno ufungamano laweza kufahamika katika njia mbili : kama mwenendo au kama kitendo. Ufungamano unakuwa mwenendo ikiwa binadamu ameamua kufuata njia fulani ya maisha kwa ajili ya kuujenga ulimwengu mzuri zaidi, na kuwa mtetezi wa yote yatakayotokea kwa sababu ya mwenendo huo. Na unakuwa kitendo ikiwa binadamu anashikamana na tendo fulani kwa makusudi ya maisha bora ya baadaye, hivi akiwa na majaribio fulani ya kutimiza au kazi fulani ya kufanya. Maana hizi mbili zinajitokeza katika dhana zote za nadharia ya kifungamano; na zinahitaji maelezo kwa undani zaidi.



1.1.1. Ufungamano kama mwenendo.

Mwenendo wa kifungamano ni msimamo unaoishughulikia hali fulani. Unaweza kuvifikia vitendo fulani, lakini hujishirikisha na tendo halisi. Ni mtindo fulani wa maisha, namna fulani ya kupambana na matukio, msimamo fulani wa kisiasa, na binadamu wengine, na hata na mtu binafsi. Mwenendo wa kifungamano wahitaji mambo matatu ambayo ni kujishirikisha, kuwa mtetezi, na kuwa na makusudi ya kutimiza kwa wakati ujao

Anayefungamana hujishirikisha baada ya kutazama hali fulani ya matukio, na kuamua kushika msimamo fulani kutokana na hali hiyo. Kwa hiyo anajihusisha na kuelekezwa na mwenendo anaouchagua. Mwenendo huo huonyesha wazi wazi hisi za yule anayefungamana, tena unaweza kudhihirishwa kimwili ili kushikamana kikamilifu na hali anayoishughulikia. Ndivyo MOUNIER anaeleza akisema kuwa ufungamano unalingana na "ufungamano wa roho katika tendo la kimwili." (1) Ufungamano wa kimwenendo unakuwa kama shughuli yenye juhudi ya kupambana na matatizo ya kila siku kwa ajili ya maendeleo ya ulimwengu. Hivi binadamu anayefungamana anakubali hatari ziwezazo kutokea kwani mwenendo wake unavifikia vitendo na utekelezaji wa hali ya juu.

Hali ya kujishirikisha inaambatana na usimamizi. Maana kufungamana ni kujitia katika yale unayoyakusudia. Hivi ufungamano unakuwa shauku inayomfanya mtu kuwa msimamizi wa jambo fulani. "Niko tayari kuyaeleza mambo ninayoyafanya, na ninayoyaongoza ikiwa nalazimishwa kuyaeleza", (2) kama asemavyo Gabriel MARCEL. Basi mwenye kufungamana anakubali yote yatakayomtokea, anasimama thabiti na haki aliyoichagua dhidi ya jambo fulani. Kwa kifupi, anajihatarisha bila hofu.

Lazima ufungamano uwe na makusudi yanayotakiwa kutimizwa katika wakati ujao. Maana yenyewe ya kifungamano ndiyo ielezayo kuwa na nia ya mafanikio fulani katika wakati ujao.



Kufungamana ni kukataa hali fulani ya vitu, yaani kuwa na madhumuni ya kubadili mambo. Lakini mambo hayo hayawezi kubadilika hapo hapo. Mabadiliko hayo yanahitaji muda fulani. Ni kweli kuwa ufungamano unateka katika wakati uliopita, lakini sio kwa madhumuni ya wakati ule ule, bali ni kwa kujenga wakati ujao. Hakuna jambo litokealo bila sababu. Ufungamano unategemea yaliyotokea, na unashikamana na yaliopo. Lakini lazima kuwa na uwezo wa kutoa njia zinazofikisha kwenye maisha bora zaidi. Hisani ya ufungamano ni ya kuzuia hali ya mambo kuharibika na kuchafuka zaidi. "Kufungamana ni kuchukua jukumu la jambo fulani ambalo linatakiwa kutimizwa katika wakati ujao, kwa makusudi ya kujenga ustawi wa binadamu."(3) Anayefungamana lazima ajue matukio yote ya kihistoria ya jamii aishimo, na ayafahamu matakwa ya waanadamu wenzie. Ufungamano wake unatakiwa kukubaliana na mwelekeo wa maisha bora ya jamii katika historia yake. Hivi ufungamano wa kimwenendo unakuwa wa vitendo mwishowe.

#### 1.1.2. Ufungamano kama kitendo

Ufungamano huo unatia katika vitendo mawazo yanayomsumbua mtu kutokana na hali fulani ya maisha. Ni maamuzi na nia thabiti inayomsughulisha mwenye kufungamana. Binadamu anaamua kufanya kazi fulani na hata kujibadilisha binafsi kufuatana na kusudi halisi. Lengo la ufungamano litakamilika ikiwa mwenye kufungamana anakuwa chombo cha jukumu alilolishika. Katika kitendo cha kifungamano mtu anajishughulisha binafsi, akiwa na nia ya kuleta mabadiliko mema katika maisha ya jamii. Anaweza kuamua kuunda chama cha kisiasa, kuunda shirika au pengine kuandika akiyapinga au kuyaunga mkono mambo fulani.

Ufungamano huo ni mkataba au mapatano fulani. Kwani ukiingia katika chama unakubali kuyafuatilia matakwa ya chama na kuyatumikia vilivyo bila kusitasita. Unatakiwa kuhakikisha



yanayohitajiwa kutimizwa mfano makusudi, matakwa, kanuni na hata maarifa ya vita na kufanya lolote liwezalo kukifanya chama kifanikiwe. Ufungamano una makusudi ya kuitetea haki. Hautakuwa timamu ikiwa utabaki akilini, moyoni tu. Ni lazima kutoa majaribio yakini yanayoweza hata kuchukua mwendo wa kisiasa. Haitoshi kujua na kufahamu jambo linalotakiwa tu. Pia kuna haja ya kujishughulisha na mbinu za kutimiza lengo hilo. SARTRE anasema kwamba ufungamano ni "kazi inayofanywa ulimwenguni ili kupa ulimwengu sura yake ya baadaye."

Hivi, ufungamano ni kazi, na kazi hiyo itakuwa chombo cha kusafirisha msimamo wa mwenye kufungamana, huyu akiwa tayari kufanya chochote kinachohitajika ili makusudi yake yatokee kama yaliivyokusudiwa. Kama vile ufungamano wa kimwenendo, ufungamano-kitendo nao unakusudia wakati ujao. Ikiwa ufungamano-mwenendo ni mtindo fulani wa maisha kutokana na hali fulani ya mambo, ufungamano-kitendo unapata umuhimu wake na uzito wake katika vitendo ambavyo vinatakiwa kuwa na matokeo katika muda fulani. Wakati ufungamano-mwenendo unakumbatia, ufungamano-kitendo ni dhahiri. Ufungamano huu ndio mahsusi; kwani kufungamana kikamilifu kunahitaji vitendo halisi, vinavyoambatana na makusudi imara. Na fasihi ni mojawapo ya fani zinazoweza kutimiza matakwa ya ufungamano huo.

### 1.2. Ufungamano katika fasihi.

Ufungamano katika fasihi wajitokeza katika fasili ya fasihi yenyewe ingawa si rahisi kueleza moja kwa moja maana ya fasihi. NDUNGURU anasema kuwa "fasihi ni maelezo ya maisha ya jamii yaliyowakilishwa katika maandishi." (5) Fasili hii ina kasoro kwani inasahau fasihi simulizi, <sup>twa</sup> fasihi ina mizizi yake katika maisha ya binadamu. Nakubaliana na maelezo ya RAMADHAN ya kuwa "fasihi ni somo juu ya ubinadamu, inamulika kwa darubini binadamu katika maisha. Hii ndio sababu wengi wanaiita fasihi kioo cha maisha ya jamii." (5)



Tunaona kuwa fasihi ina kazi rasmi ya kuonya jamii. Na yajulikana kuwa maisha ya jamii yana mema na maovu. Lakini nia hasa ya Fasihi ni kuyaendeleza mambo mazuri na kuyarekebisha mabaya. Kiango na Sengo wakilinganisha fasihi na mwamvuli wanasema yafuatayo :

"Kazi ya mwamvuli ni kukinga jua au mvua. Mwamvuli huu unaolinganishwa na fasihi ni mwamvuli unaokinga amali za maisha ya watu. Amali hizi hujengwa na binadamu, ili kujenga misingi mizuri, hifadhi njema na maendeleo mema ya hadhi na taadhima yake. Amali hizo ndizo zijingazo fasihi. Fasihi huzihifadhi amali hizo na kuzifichua kwa kuonyesha watu ubora na uovu wa kila kipegele cha maisha, wakati mwingine kwa njia ya kujadili, kushauri, kuasa, kuusia, kuadhibu na kuelimisha."(7)

Ni kusema kwamba fasihi inapata misingi katika yanayomzingira mwandishi, huyu akikusudia ustawi wa jamii. Na hapa njia fulani ya kifungamano inaanza kujitokeza yaani makusudi ya maisha bora ya binadamu. Ndivyo SARTRE aelezavyo kuwa mwandishi mahsusi sharti ayazingatie mazingira yake na kuamua kuwajulisha wenzie ili washiriki katika kuyabadili kwa makusudi ya maisha bora ya baadaye. Ufungamano katika fasihi unaelezwwa kwa ufasaha zaidi kwa kuyajibu maswali haya matatu anayojiuliza SARTRE(8) anapozungunzia swala la Fasihi :  
kuandika ni nini? Kwa nini mwandishi aandike? Nani anayeandikiwa?

SARTRE yasema kwamba "fasihi ni lugha"(9). Na yajulikana kuwa lugha ni chombo cha mawasiliano, maana mwandishi anapoandika anawasilisha ujumbe. Kazi hiyo haiwezi kuishia katika kutafakari tu, kwani kusema ni kutenda. Ni kweli kuwa kile kinachozungumziwa hakibaki vile vile. Kwa mfano ikiwa tabia ya mtu fulani inazungumziwa na kulaumiwa, mtu huyo haiwezi kubaki yule yule. Anajitahidi kujirekebisha na kuchukua mwenendo mpya. Anaweza kukazana katika mwenendo ule ule wa zamani kwa ukaidi, lakini pale ana sababu zake; ukweli ni kwamba hatabaki yule yule wa asili. Kwani kwa kumtangaza, anafunuliwa kwa wengine na hata kwa upande wake mwenyewe. Anakabiliwa na kuingiliwa. Na kila mmoja lisenwalo juu yake lina



kusudi la kumbadili. Yaonekana wazi kuwa kusema ni kutenda, ikiwa kumsemasema mtu kunamlazimisha kubadilika au kutenda jambo fulani.

Kadhalika, mwandishi ni mtu anayechagua njia fulani ya kitendo. Kitendo hicho ni cha kufunua. Mwandishi anaingilia hali fulani ya matukio, na kuufunulia ulimwengu mzima ili kuubadilisha. Mwandishi anajua anachokifunua, na mabadiliko gani anayotaka kuletea ulimwengu kwa kutumia mbinu hiyo. Kazi ya uandishi ni ya kumfanya mtu ajue ulimwengu aishimo na apate kushughulika mwenyewe na yanayomhusu. Mwandishi akisha kata shauri la kuyafunua yanayomsumbua kwa kutumia lugha, hawezi kujiepusha na kazi hiyo. Hawezi kuficha tena uwezo wake wa kusema. Na SARTRE yasema kwamba: "Kunyamaa si kuwa kigungumizi, bali ni kukataa kusema; kwa hiyo basi ni kusema."(10) Mwandishi akichagua kutosema lo lote juu ya jambo fulani ana sababu zake. Anajua umuhimu wa kulizungumzia jambo fulani kuliko lingine. Akiwa na makusudi ya kubadili, anajua mambo anayotaka kuyabadili. Hivi kuandika hakumuumbi mwandishi, bali kinachomuumba ni jinsi anavyopinga mambo yanayotakiwa kupingwa.

Kama anavyosema SARTRE, mwandishi wa kisasa hana haja ya kushughulikia uzuri wa mazingira mfano kuyasifu mabonde. Kazi yake ni kutoa ujumbe kwa msomaji. Lazima mpango sahihi wa kisanaa utoe ujumbe halisi ambao ni wito wa binaadamu kuyashughulikia yanayomhusu. Ikiwa mwandishi katika maandishi anakubaliana au anatengana na ulimwengu aishimo, anazo sababu zinazomfanya achukue msimamo fulani na kuutoa kwa wasomaji wake. Anafungamana kikamilifu na msimamo huo, na anawataka wasomaji wawe waaminifu na ikiwezekana wafuate msimamo huo.

Kila mwandishi ana sababu zake za kuandika, lakini wote wanayo sababu moja inayowaunga : wanaandika ili wasomwe. Mwandishi hawezi kujiandikia yeye mwenyewe. Anayatoa maoni yake na matakwa yake kwa msomaji ili naye ayatafakari na kuya-



pima yanayomsumbua. Kwanza mwandishi anasumbuliwa na hali ya yanayomzingira, lakini hawezi kuyabadili yeye peke yake. Inambidi kuwaita wenzie, kuwaamsha na kuwashirikisha katika mapambano. Ni muungano wa mwandishi na msomaji ambao unatoa sababu halisi za kazi hiyo ya akili; maono sanaa hiyo inawasilishwa kwa mtu mwingine. Mwandishi anaandika ili kumshirikisha msomaji. Hivi anakuwa msimamizi wa yatakayotokea. Ni kweli kuwa mwandishi anapoandika juu ya udhalimu wa ulimwengu, akitoa maoni yake, fikra zake, chuki zake, masikitiko yake, na kumwo-nyesha msomaji kama haya ni maovu yanayotakiwa kukomeshwa, sharti msomaji naye achukue hatua fulani. Hakika ni kuwa haya-takubaliwa na wote. Wanaoshambuliwa hawatafurahia msimamo wa mwandishi, ila watampinga. Ndio sababu mwandishi anakuwa mtetezi na kukubali yatakayotokea hata ikiwa yanampinga sana.

Ikiwa msanii anampa msomaji kazi ya kutimiza yale aliyoyanza na kama msomaji anapata umuhimu wa kazi hiyo katika dhamira za mwandishi, basi hapa mtunzi anamwita msomaji ashiriki katika mapambano. Mwandishi anamwita msomaji kutoa maoni yake juu ya ufunuo wa mwandishi. Nakubaliana na SARTRE kwamba mwandishi mashuhuri lazima andike lakizilaumu dhulumu za ulimwengu. Na hata ikiwa anazikubali, inakuwa njia fulani ya kuzipitia na kuziondoa. Kwani msomaji mwenye busara hata-soma na kuvumilia tu, atachukue msimamo fulani wa kumkubali au kumpinga mwandishi. Hivi ulimwengu anaoshtaki mwandishi utafunuliwa kutokana na maoni, sifa au chuki za msomaji. Kwa kifupi, mwandishi anaandika ili kutoa maoni yake juu ya maisha ya ulimwengu akipinga udhalimu fulani katika jamii, na kutoa masuluhisho yanayoweza kutufikisha kwenye ustawi wa jamii. Hapa ndipo ufungamano unapojitokeza. Lakini ni msomaji gani anayemfikiria anapojiingiza katika mapambano hayo Na kijamii na hata ya kisiasa? Hapa tunalikabilia lile swali la mwisho yaani ni nani anayeandikiwa?

Inaonekana wazi kuwa mwandishi anamwandikia kila awezaye kumsoma. Tulishaona kuwa mwandishi anawakabili watu wote kwa jumla. Lakini mwandishi anajua kuwa anawaandikia wale



ambao uhuru wao umepotea, wale ambao wanaonewa; na anawajua sana wale ambao wamepokonywa uhuru wao. SARTRE yasema kwamba mwandishi "anawaendea watu wa rika lake, wananchi wake, ndugu zake kikabila na kitabaka." (11) Ni kweli kuwa kitabu kita-waendea watu wanaoishi wakati mmoja, katika jamii moja; wale wanaoishi katika matukio sawa sawa, walio na matatizo sawa, kwa kifupi wale walio na historia moja. Mwandishi maarufu atayachagua mambo na maneno fulani ya kutilia mkazo. Mambo haya yatachaguliwa kufuatana na hadhira ambayo anataka kuishughulikia. Mwandishi atawashambulia waonevu, akiwaonyesha wanaokandamizwa njia ya kujikomboa.

Lakini mwandishi pia anawaandikia wale wadanganyifu akiwapinga, kuwashambulia na kuwaonyesha uovu wao. Anawapinga wale wenye madaraka ya juu hasa watawala waaminio katika itikadi ya kikandamizi. Hivi mwandishi anakuwa mtetezi. Anahuzunishwa na kuwaona wenzie wakionewa na kunyonywa na watu wachache tena wenye madaraka.

"Ni katika jamii zisizo imara na zinazogawanyika katika makundi ya kijamii, ambamo mwandishi (...) anatoa maelezo ya masikitiko yake." (12)

Kwa yule anayetawala, mwandishi anamwita kurekebisha tabia yake ya majivuno na ya kuwaonea binadamu wenzake. Kwa yule anayonewa mwandishi anamshauri kujishughulisha na ukombozi wake.

Basi, kazi ya mwandishi ni ya wito. Ili maandishi yawe makamilifu inawabidi wasomaji kuchukua yale wanayoyapewa na kuyafikiria kwa makini. Maandishi yaweza kuwa kanuni halisi ya kitendo, maana yaweza kuwafanya wanadamu washughulike wenyewe katika ujenzi wa jamii bora zaidi. Kwa kifupi, hadhira anayoiandikia mwandishi imo katika makundi matatu kama ayatoavyo SARTRE : kuna watawala na wasomi wenye maarifa, jamii ambayo inahusika katika maandishi; halafu mtu yeyote awezaye kusoma, hasa yule ambaye mazingira yake yanaweza kulingana na yale aishimo mwandishi. Kutokana na haya tuliyoyaona kuhusu ufungamano katika fasihi, inabidi kutazama jinsi nadharia hiyo inaji-



tokeza katika fasihi ya kiafrika ili tuweze kuhusisha na vitabu vinavyohusika katika kazi za KIBZILAHABI.

### 1.3. Ufungamano katika fasihi ya kiafrika.

Barani Afrika, kama mahali pengine kuna aina mbili za Fasihi yaani fasihi simulizi na Fasihi-andishi. Fasihi simulizi, tangu zamani za kale ilikuwa kipengele kimojawapo muhimu cha utamaduni wa kiafrika. Baadaye ikafika Fasihi-andishi. Fasihi-andishi yaweza kugawanywa katika mafungu mawili: kuna maandishi ya kifasihi yanayohusu Afrika lakini yaliyoandikwa na wageni. Hayo yalitokea kabla na hata baada ya hati kuingia Afrika, kama tutakavyoona. Pia kuna yale yaliyoandikwa na waafrika yakihusu Afrika na watu wake. Na hayo yamo katika mafungu mawili : kuna yanayotumia lugha za kigeni, na mengine yanayotumia lugha za kiafrika. Yote hayo yalitokea baada ya hati kuingia. Katika kurasa zifuatazo, Fasihi-andishi ndiyo itakayohusika, hasa ile iliyoandikwa na waafrika (na weusi wengine) wakizungumzia Afrika na watu wake, kwa kutumia lugha za kigeni au za kiafrika. Fasihi hii ilisababishwa na ile waliyoandika wageni kuhusu Afrika. Hivi ni muhimu pia kupitia maandishi ya wageni hao.

Yasemekana kuwa tangu karne ya 18, kulizuka huko Ulaya (Ufransa, Wiingereza, Ujerumani) maandishi yaliyokuwa yakiongozwa na mawazo ya ROUSSEAU kuhusu mtu na jamii, na maandishi hayo yalikuwa yakimwona mwafrika kama mnyama. Sura ya mwafrika ilichukua nafasi kubwa sana katika fasihi hiyo iliyokuwa ikishughulikiwa hasa na akina HUGO, MERIMEE, PROMENTIN, (33) n.k. Maandishi yao yanonya Afrika kama bara lililojaa mafumbo, maajabu, wanyama wakali na majitu ya kikale ambayo hayana utu wowote. Kitabu cha Franoudh Sieger(14) kinachozungumzia Mwafrika na Afrika yenyewe kama ijitokezavyo katika fasihi ya kifransa ya tangu 1800 hadi 1945, ndicho kionyshacho wazi kuwa maandishi yalikuwa chimbuko la ukoloni.



Vitabu hivyo viliwapa wazungu nia ya kuja na kuwaelimisha Waafrika katika mambo ya kidini na ya kistaarabu.

Baadhi ya waandishi katika lugha ya kiingereza pia, walishughulika na kazi hizo za kumnyanyasa mwafrika. Huko Marikani ambako mambo ya kiutumwa yalienea kuliko mahali peengine ulimwenguni, fasihi ya aina hii iliimarishwa. Miongoni mwa waandishi waliozungumza mambo hayo kuna kina Beecher Stowe. (15) Wakati huo huo, kukaja maandishi mengine ambayo yalikuwa yakinwonya mweusi kuhusu kukataa kuvumilia anayotendewa na kuchukizwa na hali yake ya kiutumwa huko Marikani. Fasihi hiyo ndiyo iliyowaamsha weusi wa Marikani na kwanza kuandika wakimtetea mtu mweusi. Mnamo mwaka 1920, weusi wa Marikani akina James Weldon Johnson, Claude Mackay, Countee Cullen, Langstone Hughes na Richard Wright wakaanza kuandika wakipinga mambo ya ubaguzi wa rangi pamoja na utumwa.

Wakati huo, Afrika ilikuwa imeisha gawanywa katika sehemu sehemu na kutawaliwa na wakoloni. Ingawa mwafrika alikuwa akiteswa na kuharibiwa utamaduni wake, kulikuwa na baadhi ya waafrika ambao walimsifu mkoloni kwa kazi yake ya ukombozi, kazi ambayo wanadai kupewa na Mwenyezi Mungu yaani kumtoa mwafrika katika ushenzi. Walikuwa wanathibitisha uhalali wa mzungu kumtawala mwafrika. Kwani Afrika ilikuwa inajulikana kama nchi ya wanyama waliotawaliwa na ushenzi, jadi na desturi za kijinga, pia jamii zisizo na ustaarabu wowote na itikadi yoyote ya kuwangoza.

Hali hii iliwasikitisha sana wanafunzi waliokuwa wakisoma Ufransa ambao baadhi yao ni CÉSaire, DAMAS, na SENGHOR. Maandishi ya Weusi wa Marikani yalikuwa yameisha wafikia. Na kutokana na wale weusi watetezi wa ukoloni wanafunzi hao walianza kuandika wakimtetea mwafrika na kuwapinga wale waliwaunga mkono wazungu. Wanafunzi hao walijiunga na kutoa majarida (16) mengi ambapo waliwaamsha ndugu zao kupigania uhuru wa kisiasa na kitamaduni. Hivi kilikuwa kimeisha zuka chama cha Uzalendo



(Négritude) ambacho nia yake ni kurudisha heshima ya mwafrika na kufufua utamaduni wake. Chama hicho kilikuwa kinatumia hasa mashairi.

Chama hicho kiliimarishwa mmamo mwaka 1934 hadi 1945. Mashairi yao yalikuwa tena malalamiko juu ya hali ya kumtesa na kumnyonya mwafrika. Kwani

"Kati ya mkoloni na mwafrika, hakuna uhusiano wowote isipokuwa, kufanyisha shokoa, hofu, mshurutisho, polisi, kodi, unyonyaji, nguvu, masharti, dharau/.../ ambavyo vinamfanya mkoloni kuwa jemedari mwangalizi wakati mwafrika anakuwa chombo cha uzalishaji mali."(17)

Basi ukoloni ambao ulikuwa umeonekana kama njia ya kumtoa mwafrika katika ushenzi na ujinga wa maisha, unashambuliwa na kuonyeshwa kama kitendo cha kinyama. René MARAN, katika kitabu chake Batouala, ingawa alikuwa mtume wa kikoloni barani Afrika, aliweza kueleza maovu ya wakoloni kwa uhodari sana. Waafrika nao wakaanza kuusifu utamaduni wa Afrika wa kabla ya ukoloni, na kuushambulia ukoloni uliokuja kuharibu utamaduni na jamii ya asili ya kiafrika. Hata mwafrika akasifu uafrika wake. Ndipo Bernard Dadié akatunga shairi liitwalo: "Nakusifu Mwenyezi Mungu kwa kuniumba mweusi."(18)

Baadaye waandishi hodari wa riwaya wakatokea. Kina Mongo BETI ambaye katika vitabu vyake(19) anazungumzia mwingiliano wa taasisi za kigeni na za kiafrika ambao umechafua jamii za kiafrika. Anatenganisha kwa mfano maisha ya mjini na ya vijijini. Pia analalamika juu ya maisha ya mwafrika ambaye anakandamizwa na kunyonywa na mkoloni. Pia anashambulia dini za kigeni ambazo zinashiriki katika kueneza ukoloni. Pamoja na OYONO(20) ambaye katika vitabu vyake anaonyesha unafiki na unyama wa mkoloni. Wote hao wanataka mabadiliko yenye nia ya kumkomboa mwafrika hivi maandishi yao ni ya kifungamano. Maandishi yao yalikuwa ya kimapinduzi kijamii na kisiasa. Kazi za kundi hilo zilikuwa yowe la huzuni na uasi, zikionyesha wazi maovu ya kikatili ya mkoloni; na kumwonyesha mwafrika



kuwa wakati umefika wa kupigania uhuru kimaandishi na hata kisilaha.

Kama ulivyoamua mkutano wa pili wa waandishi na wasanii wa kiafrika uliofanyika huko Roma mwaka 1959, dhamira kuu ya maandishi ya kiafrika ilikuwa ya kueneza haja ya kupigania uhuru. Lakini chini ya dhamira hiyo ya kisiasa inayomtenganisha mwafrika na mkoloni, mtawala mzungu na mnyonywaji mwafrika, kuna migogoro mingine kama vile usasa na ukale, mji na kijiji, mgogora wa vijana na wazee n.k. Maandishi ya kina C.H. KANE, BETI, M., F. OYONO yalizingatia sana dhamira hizo. Na kazi hizo zikaamsha mwamko wa kisiasa katika wasomaji wake hasa Waafrika.

Baada ya uhuru kupatikana, waandishi waliendelea na kazi yao : walikuwa wameisha tambua kuwa ushupavu wao ndio utakaofanya mapinduzi halisi barani Afrika na kumpa uhuru mtimilifu mwafrika. Ukaidi wa nyakati za ukoloni ulibadili sasa mwendo wake kufuatana na matukio ya baada ya uhuru. Dhamira zinazokabiliwa ni mbalimbali na zinatofautiana kufuatana na nchi kwani matatizo yanayowasumbua waandishi ni tofauti kufuatana na mazingira yao. Tunavyoweza kusema ni kwamba, kwa jumla, maandishi hayo yalikuwa yakiiongelea juu ya udhaifu wa utawala mpya ambao ulikuwa wa kikandamizi, kisultani, na kijeuri kuliko ule wa kikoloni. Dhamira nyingine zinazojitokeza ni umaskini, ukoloni mambo leo, unyonyaji n.k.

Maandishi hayo yanawasilisha masikitiko kuwa uhuru uliokuwa ukitegemewa haujapatikana, bali hali imeharibika zaidi kuliko zile nyakati za ukoloni. Kina Mongo BETI(21) katika maandishi yake ya nyakati za uhuru, anayachukua yale mashtaka yaliyokuwa yakiwaendea wakoloni katika maandishi yake ya mwanzoni, na kuyawawekea watawala wanya wa kiafrika. Hata hivyo, ukali upatikanao katika maandishi ya nyakati unapita yowe, bali unakuwa projekti ya kifasihi ambayo inakusudia ujenzi wa jamii mpya na muundo wa kiuchumi unaofaa ili kuhakikisha uhuru mkamilifu wa Afrika na watu wake.



Dhamira inayoshughulikiwa hasa ni ya kisiasa, nayo yahusu uovu wa utawala ambao unafuata siasa ya chama kimoja kimoja(22), pia ni kilio juu ya upotofu wa kundi la watu wachache (matajiri) ambao wananyonya wenzao. Kuna wengine ambao wananyamaa na kutojasiri kuwashambulia watawala hawa wapya, na hata wale wanaosifu utawala huo.

Hivi tunaweza kusema kuwa Fasihi-andishi ya kiafrika ni ya kifungamano, maana si ya kuremba na kuyasifu mabonde, bali inawasilisha ujumbe halisi ambao ni kupigania kujenga jamii yenye maisha bora. Kila ukurasa, kila msitari, kila aya, kila neno lina alama ya mashaka ya binadamu huyu mwafrika na kumtetea kufuatana na nyakati za historia ya Afrika na watu wake, hasa tangu wazungu walipoanza kuligawagawana bara hilo. Maandishi hayo ni kama mabarua ya kibalozi yanayopelekewa wale wapaswao kuyashughulikia, na hao ni wakoloni wa nyakati za ukoloni, viongozi baada ya uhuru, na hasa wale wanaokandamizwa ili wenyewe wakazane na kazi ya kujikomboa.

Ni hakika ya kuwa mwandishi wa kiafrika, mwanzoni mwa karne hii, alifungamana sana na ari ya kupata uhuru kiasi ambacho fasihi yake ikawa kama vita ambavyo vinamshambulia mkoloni, na kugombania kumrudishia heshima mwafrika mweusi. Na makusudi yao yakafikiwa katika pande zote mbili. Upande wa Waafrika hakuna mwandishi ambaye hakushikwa na ari ya uanamapinduzi na kuwa na haja ya kujiepusha na udanganyifu wa mkoloni. Hivi kufungamana si lengo bali ni chimbuko lenyewe la maandishi, maana maandishi yanatokea baada ya mwandishi kusumbuliwa na hali fulani.

Ufungamano waonekana pia katika nia ya SARTRE ya kukashifu. Ufunuo huo unapatikana katika maneno anayoyatoa SARTRE kwa wazungu wenzake :

Mlikuwa mmatumaini nini walipoondoa kizibo kilichokuwa kinaifunga midomo hiyo mieusi? Kwamba wataanza kuimba sifa zenu? Vichwa hivyo ambavyo mababu zetu walivipinda kwa nguvu, mlikuwa mnadhani kuwa vitakapoinuka, mtapata



kuabudiwa? Watu weusi hao hawa hapa wanasimama na kutukazia macho; na nawatakia (nyie) kutambua, kama mimi (nimeshatambua), ya kuwa tumefunuliwa."(23)

Ufunuo huo na uaminifu ukamfikisha mwafrika kwenye uhuru; hivi ufungamano wa maandishi ukafaulu. Na kama tulivyoona, baada ya uhuru, fasihi ikabadili sura na kufuatana na matukio.

Baada ya uhuru kupatikana, utawala ukabadilika. Licha ya kuwa wa Kisultani, ukawa wa kijeshi katika nchi kadhaa barani Afrika, na kumkandamiza zaidi binadamu. Sehemu nyingine siasa za ujamaa zikaimarishwa. Yote hayo yakazungumzwa. Waandishi kadhaa wakaandika wakulaumu utawala huo wa kisasa kiasi ambacho utawasikia wahusika wakipiga kelele: "Afadhali ukoloni!" Mojawapo ya maandishi walijishughulisha na dhamira hiyo ni kina KOUROUMA, LABOUTANSI, MONENEMBO.(24) Wote hao wanalalamika juu ya hasara ya uhuru ambao haukutimiza lengo lake. Maandishi ya fungu hili yalianza kulaumu utawala na kumtetea mnyonge. Haitakuwa rahisi; kwani baadhi ya maandishi hao walifukuzwa nchini mwao, wengine wakakimbia, wengine wakafungwa na hata kuuawa. Baadhi ya waliokimbia ni AYI KWEI ARMAH wa Ghana, MONENEMBO wa Guinea, E. DONGALA wa Kongo. Mojawapo ya waliofungwa ni NGUGI wa Thiong'o wa Kenya. Na kati ya waliouawa, kuna M. KAYOYA wa Burundi.(25)

Wanaoandikiwa ni wale walio na uwezo wa kuleta mabadiliko, licha ya kuwa wenyewe ni watawala, pia wasomi wenye maarifa, na hata watu wa kawaida wameanza kuandikiwa katika lugha za kiafrika. Waandishi hao wanafanya jinsi iwezekanavyo ili waijenge jamii mpya, yenye maisha bora zaidi. Ingawa hadi leo jamii hiyo bado haijapatikana, jitihada yao huenda ikafikiwa.

Hivi fasihi ya kiafrika kufungamana katika njia tatu zifuatazo kufuatana na nyakati: kumrudishia heshima mwafrika na utamaduni wake, ukoloni na madhambi yake, na ujenzi wa jamii mpya. Yaonekana kuwa hadi leo, fasihi ya kiafrika ni



ya kifungamano. Mwandishi ni mjumbe anayeiamsha jamii aishi-  
mo, anayechunguza yanayomzingira, anayetazama kwa makini hali  
ya jamii, anayeshambulia mwenendo fulani na kupendekeza njia  
ya kufuata ambayo anaifikiri ya kuridhisha. Hapa tukiuangalia  
ule msimamo wa GOLDMANN wa kuwa kazi ya fasihi si uvumbuaji,  
bali zao na hata picha ya maisha ya jamii anayoipiga mwandishi;  
yaani mtungaji wa kitabu si mwandishi bali jamii yenyewe.  
Kazi ya mwandishi ikiwa ni kunukuu matakwa ya jamii. Kama  
mwandishi angeambiwa na umma : 'Wewe unayeelimika na unayejua  
kusema na kuchunguza kuliko yeyote, nenda kawe mjumbe wetu  
kwa maongozi ya ulimwengu na uzitetee baki zetu.' Hadi leo  
hii ndiyo kazi ya mwandishi mwafrika.

### 1.3.1. Ufungamano katika fasihi ya Afrika ya Mashariki

Hadi hapa, yalishughulikiwa hasa maandishi ya ki-  
afrika katika lugha ya kifransa; kwa sababu kuna ukosefu wa  
maandishi yanayotumia lugha nyingine hasa lugha ya kiingereza.  
Tena sio rahisi kuikumbatia fasihi ya waafrika katika lugha  
ya kiingereza kwa jumla kwani lazima kuwa na tofauti kati ya  
mtu wa Ghana na mtu wa Kenya. Ingawa wote wanazungumza  
kiingereza, mawazo yao yanatofautiana kufuatana na mazingira.

Fasihi ya kiafrika katika lugha ya kiingereza hai-  
kuenea sana nyakati za ukoloni. Waandishi katika lugha hiyo  
hawakushughulikia sana wazo la uzalendo. Baadhi yao wanatoa  
lawama kwa kusema : "Chui haimbi uchui wake bali anayarukia  
mateka yake." Walakini nao walipigania uhuru. Na mtu anaweza  
kujiuliza sababu zilizowafanya waafrika hao wasiandike kama  
wenzao wa lugha ya kifransa.

Wataalamu wengi wanakubaliana kuwa tofauti hiyo ni  
matokeo ya mbinu walizozitumia wakoloni hao wawili katika  
kumtawala mwafrika. Ni kweli kuwa wafrransa, katika ukoloni,



waliwafundisha Waafrika mambo ya kwao, walimjenga kielimu na kumfanya mwafrika ajiepushe na utamaduni wake, na aushike ule wa kigeni. Wafransa walikuwa wakiwafundisha lugha ya kifransa tangu mtoto akiingia katika shule ya msingi wakati waingereza walikuwa wakiwaanzisha wanafunzi kiingereza darasa la sita. Ndivyo Taban Lo Liyong anasema: "Mutojua kiingereza kikamilifu kwa waafrika ni tokeo la utawala wa kifalme wa waingereza. Waafrika wanaosema lugha ya kifransa wanaifahamu kuliko sisi tunavyofahamu kiingereza."(26)

Utawala huo wa kiufananisho ambao uliongozwa na Wafransa ulitoa wasomi mashuhuri kama SENGHOR ambao hawapati-kani katika Afrika Mashariki. Katika mambo waliyowafundisha Wafransa walitilia mkazo ushairi, sanaa ambayo waafrika wanashughulikia kwa kawaida. Sanaa hiyo ikawa chombo cha kupigania uhuru. Waingereza walifanya kinyume chake. Na jambo hilo lilizuia elimu ya Waafrika waliotawaliwa na Waingereza. Waingereza waliwafundisha mambo machache ya kuwawezesha kuwatumikia tu. Hata hivyo, waandishi wenye maarifa walijitokeza kama vile ARMAHAYI KWEI, CHINUA ACHEBE na wengine ambao waliweza nao kuyazungumzia mambo mbali mbali kama yale waliyoyazungumzia wale wa lugha ya kifransa. Kwa mfano kumrudishia heshima mwafrika na utamaduni wake na mengineyo.

Katika Afrika Mashariki, fasihi katika lugha ya kiingereza haikuenea sana kabla ya uhuru. Katika harakati za ukombozi lugha iliyotumiwa hasa ni kiswahili. Katika lugha ya kiingereza, mwandishi anayewakilisha fasihi ya Afrika Mashariki ni NGUGI wa Thiongo ambaye aliandika hasa baada ya uhuru, japokuwa mara kwa mara alifungwa kutokana na maandishi yake. Ebu tuone anayoyazungumzia kwa kifupi.

Ngugi anaamini kuwa mwandishi wa manufaa ni yule ambaye katika maandishi yake anayashughulikia matatizo ya jamii yake; kuyakabili akilaumu udhalimu na unyonyaji wa



binadamu. Katika utangulizi wa Secret Lives(27), anasema kuwa aliporudi kutoka Marikani, aliwakuta watu, ambao kutokana na hali yao mbaya, wamekimbilia katika ulevi. Watu hao ambao walikuwa wameisha tambua kuwa wamedanganywa walikuwa wanasikitishwa sana na wakati ujao ambao waliuona utakuwa mbaya zaidi. Ndipo labda akaamua kuandika. Katika maandishi yake anayazingatia hasa mambo mawili : ukoloni na madhambi yake, pamoja na ujenzi wa jamii mpya.

Katika Home Coming(28) Ngugi anapinga upebari, siasa ambayo inaeneza unyonyaji na ukandamizi wa binadamu. Ana-laumu pia dini ambayo ni chombo cha ubepari na ukoloni. Anaona kuwa wakuu wa dini (mapadri) wanashirikiana na mkoloni katika kumfarakisha mwafrika. Wakati mkoloni alimyang'anya ardhi yake mwafrika, padri alimyang'anya roho yake. Hivi mwili na roho ya mwafrika vikachukuliwa. Anaona kuwa ubepari na dini vinazuia ustawi wa jamii.

Lakini Ngugi ambaye alikuwa akitegemea kuwa hali hiyo itaondolewa baada ya kupata uhuru, analalamika sana kuiona hali hiyo ikiendelea na hata kuharibika zaidi. Watawala wapya ambao ni waafrika wenyewe wanaliyenga tabaka la wanyonyaji. Hakuna mabadiliko ya kisiasa wala kijamii yaliyotokea kimsingi. Watawala weusi wanawakilisha wasungu na mambo yanabaki yale yale ya kabla ya uhuru. Hivi uhuru haukupatikana kikamilifu. Hakuna uhuru ikiwa watu wengi, ambao walipigania uhuru hawana maisha mema. Malalamiko hayo anayatoa katika kitabu chake Petals of blood(29) ambapo yaonekana kuwa watu waliopiga vita wazalendo wa uhuru, ndio wavunao mazao ya uhuru huo, wakati wale walioupigania kwa ujasiri (kuna Abdulla ambaye alipoteza mguu katika mapambano) ni wanyonge na wenye maisha ya kutisha.

Mwandishi anaikusudia jamii bora yenye usawa, ambayo itaimarishwa na ujamaa wa kiafrika. Katika kuijenga jamii mpya mkazo utawekwa kwenye maisha ya jamii za Afrika ya awali ambapo jamii inamshughulikia binadamu kuliko binadamu anavyo-



jishughulikia mwenyewe. Kwani katika Afrika ya asili, bina-  
damu anafurahia kufanya kazi katika jamii na kwa manufaa ya  
jamii. Matajiri na masikini, wote wanapaswa kushughulikia  
ustawi wa jamii. Mwandishi anaona kuwa ujamaa huo ndio njia  
pekee itakayoleta mapinduzi kijamii, kisiasa na kiuchumi.  
Mwishoni mwa Petals of blood, tunaona wafanyakazi na wakulima  
wakijiunga katika chama cha Ukombozi, na kuwaua viongozi wa-  
dhaifu. Tunawaona MZIGO, KIM RIA na CHUI (wahusika) ambao ni  
mabingwa wa ubepari wakiunguzwa. Kifo chao ni dalili ya kua-  
nguka kwa ubepari. Basi maandishi ya NGUGI ni ya kifungamano.

Ingawa utawala wa waingoreza ulizuia fasihi katika  
lugha ya kiingereza, iliruhusu matumizi ya lugha za kiafrika  
kiasi ambacho kiliwawezesha waafrika kuandika wakitumia lugha  
zao katika harakati za uhuru. Mfano wa pekee ni Tanzania  
ambako vitabu na magazeti yalikuwa yakitolewa katika lugha ya  
kiswahili. Katika magazeti kama gazeti la Mambo leo, washairi  
wengi, kina S.A. KANDORO, MNYAMPALA, na wengine walikuwa waki-  
andika kwa ujasiri mashairi yanayompinga mkoloni. Walikuwa  
wakizungumzia ubaya wa utawala wa wakoloni, unyonyaji, uganda-  
mizaji, uonezi na madhambi mengi ya kikoloni, mfano kuwalimisha  
na kuwanyang'anya mashamba waafrika, n.k. Mashairi yao yali-  
toa wito wa kujikomboa. Nyakati hizo ushairi ulienea sana.  
Ndicho chombo kilichotumiwa sana kati ya vyombo vya fasihi ya  
harakati za ukombozi. Sababu ni kwamba "utanzu huu ndio hasa  
uliohitajika kwa mapambano haya kwani mashairi yaliweza kuandi-  
kwa na kusambazwa, na kusomwa kwa haraka zaidi kuliko riwaya au  
thanthiliya." (30) Mwandishi mwingine ni Shaban Robert, ambaye  
katika vitabu vyake na mashairi kadhaa anaonyesha utambuzi wa  
umuhimu wa kutumia nguvu katika kujikomboa. Kazi zake hasa  
zina malalamiko kuhusu kuoza kwa dunia. Waandishi wote wa  
kabla ya uhuru walikuwa wakiugombania uhuru kwa kuonyesha maovu  
ya mkoloni.

Fasihi ya kiswahili ilienea baada ya uhuru kupatikana  
hasa katika utanzu wake wa riwaya. Waandishi wengi wakatokea.



Wachache kati yao ni M.S. Mohamed, C.A. Mhina, A. Shafi Adam, E. KEZILAHABI n.k. Hamu yao ni kuumba jamii mpya, kufuatana na jinsi wanavyoona matatizo yanayoikabili jamii yao. Baadhi ya matatizo hayo ni ukoloni mambo leo, na unyonyaji wa mwafrika kwa mwafrika, jambo ambalo ni urithi wa ukoloni. Ni kweli kuwa baada ya uhuru kulizuka tabaka la "wazungu weusi" ambalo linawakusanya wanajeshi, wana-siasa na wafanyakazi na kuwakandamiza wanakijiji na wakulima. Maandishi yao yanaonyasha haja ya siasa ya ujamaa ambayo ni chombo cha kumwoko mwafrika mnyonge. Kuamua kufuata siasa ya ujamaa sio kuji-pendekeza bali ni njia mojawapo ya kimapinduzi. Ikiwa katika kazi zao wanaonyesha madhambi na upotofu wa watu kadhaa ambao wanazuia jamii kuufikia ustawi. Na ikiwa watu hao hawajiepu-shi na udhaifu wao, hapatakuwa na uhuru kamili. Hivi waandishi wa kiswahili, hasa E. KEZILAHABI wanaweza kuchunguzwa katika njia hizi tatu zifuatazo : kumrudishia heshima mwafrika na utamaduni wake, ukoloni na maovu yake kama vile unyonyaji, upuuzi; na ujenzi wa jamii mpya.



TAYBIHI.

- (1) "esprit engagé dans une action corporelle"  
MOUNIER, E., Le manifeste 1938.
- (2) "Je me tiens prêt à répondre de mon action si l'on  
l'exige de moi."  
MARCEL, G. Journal métaphysique, 1928.
- (3) "S'engager c'est assumer la responsabilité d'une oeuvre  
à réaliser dans l'avenir, dans le sens orienté vers la  
formation d'un avenir humain."  
LANDSBERG, P.L., Problèmes de Personnalisme,  
Seuil, Paris, 1952.
- (4) "C'est l'action menée dans le monde pour lui donner  
son visage futur."  
SARTRE, J.P. op.cit..
- (5) NDUIGURU, Kanuni na mbinu za kufundishia, E.A.P.L.,  
Arusha, 1979, uk. 122.
- (6) RAMADHAN, J.A., Ktk MULIKA n° 2 uk. 7
- (7) KIANGO, S & SENGO, T.S.Y., "Fasihi" ktk Mulika n° 4  
CHUO KIKUU cha DSM, ..... uk 2.
- (8) SARTRE, J.P. op.cit.
- (9) SARTRE, J.P. op.cit., uk. 28. "La littérature est  
un langage"
- (10) SARTRE, J.P. op.cit., uk 32.
- (11) SARTRE, J.P. op.cit. uk 88 "L'écrivain parle à ses  
contemporains, ses compatriotes,  
ses frères de race ou de classe."
- (12) SARTRE, J.P. op.cit. uk 119 "C'est dans les sociétés  
instables et quand le public  
s'étage sur plusieurs  
sociales, que l'écrivain (...) invente des explications à ses  
angoisses."
- (13) HUGO ktk kitabu chake : Bug jargal  
MERIMEE ktk kitabu chake : Tamango  
FROMENTIN ktk kitabu chake : Une année dans le Sahel



- (14) FRANOUDH, Siefer, Mythe du nègre et de l'Afrique noire dans la littérature française de 1800 à la 2ème guerre mondiale. Klincksieck, Paris, 1968.
- (15) BEECHER STOVE, Ktk Uncle Tom's Children
- (16) Majarida hayo ni - Légitime Défense  
- Revue du monde noir  
- L'étudiant noir
- (17) CESAIRE, A., Discours sur le colonialisme, Paris, P.A. 1970.  
"...entre le colonisateur et le colonisé, il n'y a de place que pour la corvée, l'intimidation, la pression, la police, l'impôt, le vol, les cultures obligatoires, le mépris, (...) des rapports de domination et de soumission qui transforment l'homme colonisateur en adjudant... l'homme indigène en instrument de production."
- (18) "Je te remercie mon Dieu de m'avoir créé noir."
- (19) MONGO BETI, - Ville cruelle, P.A., Paris, 1954.  
- Le Pauvre Christ de Bomba, Robert Laffont, Paris, 1956  
- Mission terminée, Buchet-Chastel, Paris, 1958
- (20) OYONO, F., - Une vie de boy, Paris, Julliard, 1962.  
- Le vieux nègre et la médaille, 10/18, Paris 1972
- (21) M. BETI ktk Remember Ruben, L'Harmattan, Paris, 1982.  
Péripétie et l'habitude du malheur, Buchet/Chastel, Paris 1974.
- (22) Maandishi ya NOKAN, FANTOUR, na wengineo.
- (23) "Qu'est ce que donc vous espérez, quand vous otiez le baillon qui fermait ces bouches noires? Qu'elles allaient entonner vos louanges? Les têtes que nos pères avaient courbées jusqu'à terre par la force. Pensez-vous, quand elles se relèveraient, lire l'adoration dans leurs yeux? Voici les hommes noirs debout qui nous regardent et je vous demande de ressentir comme moi, le saisissement d'être vus." SARTRE, Orphée Noir. dibaji ya kitabu cha SENGHOR, op.cit.
- (24) KOUROUMA, A., Les soleils des indépendances, Seuil, Paris, 1970.  
LABOUTANSI, S., La vie et denie, Seuil, Paris, 1979.



- MONENEMBO, T., Les crapauds-brousse, Seuil, Paris, 1979
- (25) -- ARMAH, AI KWEI, The beautiful ones are not yet born,  
Houghton Mifflin Company, Broton 1968
- MONENEMBO, T., op.cit.
- DONGALA, E., Un fusil dans la main, un poème dans la poche, Albin Michel, Paris 1973.
- NGUGI wa Thiongo, alipoandika  
- Petals of blood (niwaya)  
na - The trial of Dedar Kimathi (mchezo wa kuigiza)
- KAYOYA Michel, Sur les traces de mon père, Lavigerie, Bujumbura, 1971.
- (26) "La connaissance imparfaite de l'anglais de la part des Africains est le résultat de l'attitude impérialiste britannique. Les Africains francophones connaissent mieux le français que nous l'anglais" Taban Lo Liyong,  
13 offensives against our Enemies  
akikiriwa na PAOLI, L'Afrique des Grands Lacs, Sotgers, Paris, 1978.
- (27) NGUGI wa THIONGO, - Secret lives and other stories, Heinman, Nairobi 1975 uk. 10.
- (28) " " " - Home Coming, essays on African and Caniblean litterature culture and politics, Heinman, Nairobi 1975
- (29) " " " - Petals of blood, E.P. Dutton, New York 1978.
- (30) SENEKORO, "Mwamko wa kisiasa katika ushairi wa Shaban Robert" ktk Mulika n° 8, Chuo kikuu cha Dar-es-Salaam 1976.



## 2. JAMII NA MAANDISHI YA KEZILAHABI.

Kama tulivyoona, fasihi, hasa fasihi-andishi ni maelezo ya maisha ya jamii yaliyowakilishwa katika maandishi. Ni kusema kwamba sanaa ni matokeo ya jamii kuliko kubuni kwa mwandishi mwenyewe ingawa naye anayo kazi kubwa katika shughuli hiyo. Ni kweli kuwa jamii ihusikayo, itoayo kazi hiyo ya sanaa hujitokeza katika nafsi ya mwandishi. Na jamii hiyo ni ile aishimo msanii. Ndiyo sababu, kabla ya kuzungumzia jamii inayohusika, yatupasa kumjua kwanza mwandishi.

Mwandishi KEZILAHABI Euphrase kazaliwa Tanzania, mkoani Mwanza katika kisiwa cha Ukerewe mwaka 1944. Baada ya masomo yake katika shule ya msingi, alielimishwa katika seminari ya Kikatoliki ya Nyegezi, ambako alijifunza falsafa za kidhanifu za dini, lugha ya kilatini na mengineyo ya kawaida. Baada ya kidato cha VI alifukuzwa katika seminari kwa sababu walimu wake walifikiri hakuwa na wito wa kutosha kwa kazi ya upadre. Basi akaingia katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, ambako alisomea ualimu, lugha na fasihi. Alipopata shahada yake ya B.A. mnamo mwaka 1970, alijishughulisha na kufundisha katika shule ya sekondari ya Mzumbe, na baadaye ya Mkwawa mwaka 1971. Baadaye akajiunga na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Na mpaka sasa ni mwalimu katika chuo kikuu hicho. Kezilahabi ameo na ni baba watoto.

Kezilahabi anajulikana sana katika eneo la wataalamu wa Kiswahili kwa sababu ya makala zake hasa kuhusu ushairi. Makala zake hupatikana katika jarida MULIKA litolewalo na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam. Kwa mfano "Mashairi ya SADAAN" katika Mulika n°9 (uk. 32-38), na "Diwani ya Masamba" katika Mulika n°13 (uk. 44-50). KEZILAHABI pia ni mshairi na mtungaji wa riwaya. Baada ya riwaya Rosa Mistika, E.P.L., Arusha 1971, aliandika diwani ya mashairi Kichomi, H.E.B., Nairobi 1974, na riwaya nyingine Gamba la nyoka,



E.A.P., Arusha 1979. Vitabu vyake vingine ni Dunia uwanja wa fujo, E.A.P., Arusha 1982, na Kichwamaji.

Kutokana na mbinu iliyochaguliwa kutumiwa katika uchambuzi huu, yaani uhakiki wa kisosholojia, inabidi kujua jamii ya mwandishi ambayo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kueleza Tanzania ilivyo, mambo manne yataangaliwa, yaani jiografia, historia, hali ya kisiasa na kiuchumi. Haya yatawezesha kuyaelewa zaidi maandishi ya Kezilahabi.

## 2.1. Nchi ya Tanzania.

### 2.1.1. Jiografia.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo iliundwa tarehe 26 April 1964 kama muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni mojawapo ya nchi huru za bara la Afrika. Jamhuri hiyo ina kilomita za mraba 945.000 kwa jumla. Nchi ya Zanzibar ilikuwa inavikusanya visiwa Zanzibar (kilomita za mraba 1.660) pamoja na Pemba (kilomita za mraba 990) ambavyo vimo katika bahari ya Hindi kilomita 35 toka bara.

Sehemu ya bara, yaani nchi ya Tanganyika ndiyo kubwa zaidi. Inazungukwa kaskazini na Jamhuri ya Kenya, ziwa Victoria na Jamhuri ya Uganda. Upande wa magharibi kuna Jamhuri ya Rwanda, ya Burundi na ziwa Tanganyika. Kusini kuna Jamhuri ya Zambia, Malawi, ziwa Nyasa na Jamhuri ya Mozambika. Kandokando ya bahari, kuna Tambarare pana sana yenye urefu wa mita 120, ambamo yasimama milima mirefu ya Afrika, kama vile Kilimandjaro (mita 5895), mlima Meru (mita 4567), karibu na mpaka wa Kenya. Upande wa magharibi, ng'ambo ya tambarare ya katikati kuna maziwa ambayo yanakusanya asilimia sita ya nchi kavu. Tabia ya nchi ni ile ya nchi zilizoko kusini mwa ikweta. Mahali panapofaa kwa kilimo nchini Tanzania si pakubwa sana, kwani isi-



pokuwa pwani na kandokando ya bahari, sehemu zingine nchini ni kavu na hazipati mvua ya kutosha. Hivi utawakuta watu wamekusanyika kando ya bahari na maziwa, pale pawezapo kuridhisha kilimo.

Mji mkuu ni Dar-es-Salaam ambao pia ni bandari kubwa. Miji mingine ni Zanzibar, Tanga, Mwanza, Arusha na Dodoma. Dodoma sasa inashughulikiwa kuwa mji mkuu. Watu wa Tanzania ni waafrika ambao wanagawanyika katika makabila 120 yanayozungumza kibantu, mengine yasiyozungumza kibantu. Kabila kubwa ni la Wasukwa. Wahindi, Waarabu na Wazungu wanafanya asilimia moja ya Wananchi wa Tanzania. Kiswahili na Kiingereza ndizo lugha rasmi. Dini kubwa ni mbili yaani dini ya Kikristo na Kiislam. Dini ya kiislaam inawakusanya robo ya watanzania wote na musu ya wakazi wa Zanzibar.

### 2.1.2. Historia.

Waarabu na Wajerumani ndio walianza kutawala pwani na visiwani mnamo karne ya 17 na ya 18, wakati bara lilikuwa bado halijavumbuliwa hadi karne ya 19. Alipopita VASCO de GAMA mnamo mwaka 1499, waafrika wa Zanzibar wakawaita Masultani wa Oman, ili wawasaidie kufukuza Wareno. Masultani wakaja na kukaa kisiwani ambako walistawisha soko kubwa la watumwa. Mwaka 1832, masultani walijenga mji ili kuweza kusimamia biashara yao huko pwani. Wakati huo ndipo waarabu na wazungu walipoanza kuingia nchini.

Mwaka 1885, Wazungu waligawagawana bara la Afrika. Tanzania ikachukuliwa na Wajerumani. Shirika la Kikoloni la Wajerumani lilipokuwa likiongozwa na Karl Peters, likachukua nchi kadhaa za Afrika Mashariki. Mwaka 1890, Waingereza walishambulia Wajerumani na kuwanyang'anya Zanzibar ambayo waliweka chini ya himaya yao. Wakati ilipokuwa himaya ya



Wajerumani tangu 1891, Afrika ya Mashariki ikawa uwanja wa vita. Viliyowapambanisha Waingereza na Wajerumani mwaka 1914 hadi 1918. Mkataba wa Versailles uliwanyang'anya utawala Wajerumani na mwaka 1919, Afrika Mashariki ikatawaliwa na Waingereza na hata baada ya vita vya pili vya dunia.

Hata hivyo, Waafrika wasomi wakaanza kupigania uhuru. Tanganyika African Association (TAA) iligeuzwa hapo tarehe 7 Julai 1954 kuwa chama cha TANU (Tanganyika African National Union), kikiongozwa na J.K. NYERERE. Madhumuni yake yalikuwa kutetea uhuru. Chama cha TANU kikashinda katika kura zilizo-pigwa mwaka 1958-1959, ingawa Waingereza walikihifadhi chama cha U.T.P. (United Tanganyika Party) ambacho kimeundwa ili kuvunja athari ya TANU. Mwaka 1960, mwezi Septemba, kulitokea uchaguzi ambao ulikipa chama cha TANU viti sabini kati ya viti sabini na moja vilivyokuwa vikigombewa. Ushindi huo uliongoza nchi katika kupata uhuru. Uhuru wa Tanganyika ulitangazwa tarehe 9 Desemba 1961. Jamhuri ilitangazwa 9 Desemba 1962. NYERERE aliteuliwa kuwa Rais. Tarehe 24 Januari 1964, wanajeshi walitaka kupindua serikali, lakini jaribio hilo halikufaulu.

Nchini Zanzibar, himaya ya Waingereza ilianza mwaka 1890. Mwaka 1897 utumwa uliondolewa. Mwaka 1926, Halmashauri kuu ziliundwa. Mwaka 1957, kura zilipigwa, lakini utawala wa kisultani uliendelea. Waafrika asilimia sabini na sita ya wakazi wa nchi, waliendelea kutawaliwa na Waarabu ambao ni wachache sana. Katika kura zilizopigwa mwaka 1963, chama cha A.S.P. (Afro-Shirazi Party) ambacho kiliwakusanya waafrika wengi na kuongozwa na S.A. KARUME tangu 1959, kilishindwa na Z.N.P. (Zanzibar National Party) chama kilichoundwa mwaka 1955. Mwaka 1963, kiliundwa chama cha Umma ambacho kiliwauunga Waarabu na Waafrika wasomi. Kiliongozwa na M. BABU. Uhuru ulipatikana mwaka 1963, lakini Zanzibar iliendelea kuhi-



fadhi utawala wa kisultani chini ya Sultani Seyyid bin Abdul-lah.

Tangu tarehe 4 Januari 1963, fujo zilianza kutokea kwa sababu ya mateso waliyopata wanachama wa Umma ambao walishitakiwa kuwa na nia ya kuleta Ukomnisti Zanzibar. Tarehe 12 Januari 1964, waasi wakiongozwa na mganda John OKELLO, walipindua serikali. Jamhuri ilitangazwa na sultani alifukuzwa. KARUIDE aliteuliwa kuwa Rais na mkuu wa Halmashauri kuu ya kimapinduzi na kuendesha chama cha A.S.P. ambacho kiliisha ungana na Umma. Wakati huo huo, Nyerere huko Dar-es-Salaam alikuwa akipambana na uhaini wa kijeshi. Basi kutokana na hali hizo mbili zinazofanana muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliundwa.

### 2.1.3. Hali ya Kisiasa tangu 1964.

Mapatano ya tarehe 26 April 1964 yaliimarisha muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Halmashauri ya Serikali ilikubali hapo tarehe 5 Julai 1965 kuyafuatilia maongozi ya Tanganyika. Utawala uliamua siasa ya kidemokrasi yenye chama kimoja, Tanganyika pakiwa na TANU na Zanzibar pakiwa na A.S.P. Nyerere aliteuliwa kuwa Rais mwaka 1962, mwaka 1965, mwaka 1970 na mpaka sasa ni Rais wa Tanzania. Anao wasaidizi wawili, mmoja ni kiongozi wa Zanzibar na ni mkuu wa Baraza la Kimapinduzi la Zanzibar. Mwingine anachaguliwa katika wabunge na kuongoza Tanzania bara. Wabunge wako 204. Baadhi yao wanateuliwa kufuatana na hadhi zao, wengine wanapigiwa kura. Kuna mikoa ishirini, tatu kati ya hiyo imo kisiwani. Kila mkoa unagawanywa katika wilaya kadhaa. Isipokuwa mambo ya kijeshi, kodi, biashara ya nje, usafirishaji, kila nchi ya muungano inayo mambo ambayo inayatawala na kuyaongoza binafsi. Zanzibar ina serikali yake na baraza lake la wabunge.



Tangu 1964, viongozi wawili waliendesha siasa ya Tanzania. Hao ni Mwalimu J.K. NYERERE na S.A. KARUME. Karume alikazia mambo fulani fulani yenye kuleta demokrasia na usawa mfano kugawagawana mashamba, kupinga ukandamizi wa Waarabu na unyonyaji wa wafanya biashara na kuwakomboa wanawake. Hali hii ilizusha uhaini. Wahaini hao walimuua tarehe 7 April 1972. JUMBE Aboud ambaye alikuwa msaidizi wake alichukua nafasi ya kuiongoza Zanzibar.

Bara ni tulivu zaidi. Baada ya kuwabana waliojaribu kupindua serikali mwaka 1969, Nyerere alikitegemea zaidi chama cha TANU na kujitahidi kujenga nchi kwa kuamua kutumia siasa ya ujamaa na kujitegemea, yenye msimamo wa pekee kufuatana na maisha ya jamii za Afrika ya awali. Kanuni za siasa hiyo zimo katika Azimio la Arusha lililotolewa tarehe 5 Februari 1967. Lengo la Ujamaa huo ni kuleta usawa kati ya wananchi; kwa kugawanya mapato kwa usawa, kuondolewa kwa kodi ya kichwa, kutafishwa kwa mabenki, kujitegemea, kukishughulikia kilimo kuliko viwanda.

Tangu 1969, wakulima wanapelekwa katika vijiji vya ujamaa ambamo watu wanakusudia kufanya kazi kwa pamoja.

Misingi ya siasa ya nje ni kupinga aina yoyote ya ukoloni na ubaguzi wa rangi, kushirikiana na mataifa yote bila kufungamana na siasa yoyote. Kwa hiyo Tanzania ina uhusiano mzuri na Urusi, Jamhuri ya China, Jamhuri ya kidemokrasia ya Ujerumani na hata Marikani, Uingereza, Kanada n.k. Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizo chini ya Commonwealth. Tena imo katika Umoja wa Mataifa (UNO), kamati ya Umoja wa nchi huru za Kiafrika (O.A.U.). Ilikuwamo katika Ushirika wa nchi za Afrika Mashariki uliokuwa ukiziunga nchi Kenya, Uganda na Tanzania. Lakini kwa sababu ya matatizo mengi, ushirika huo ulianguka. Tanzania imo pia katika shirika la kutengeneza bonde la mto Akagera (O.B.K.) ambalo linaiunga na Uganda, Rwanda na Burundi.



#### 2.1.4. Hali ya kiuchumi.

Ukulima ambao unawashughulisha asilimia tisini ya Wananchi, ndio msingi wa uchumi wa Tanzania ingawa hautoi mazao ya kuridhisha. Bara wanapanda mkonge, pamba, kahawa, mahindi, karanga, nazi, mpunga n.k. Kisiwani Zanzibar wanapanda hasa karafuu. Juhudi ya serikali ni ya kuendeleza mazao hayo pamoja na ufugaji wa ng'ombe, kondoo, mbuzi na uvuvi. Tanzania ina madini mengi ambayo baadhi yao bado hayajatumika kama vile makaa ya mawe, na mengine yanayoshughulikiwa kama vile chumvi, dhahabu, almasi n.k. Katika bidhaa zinazouzwa nje, bidhaa za kilimo ndizo zinaongoza hasa kwa kuuza pamba, kahawa, na katani ambavyo vinauzwa Uingereza, U.S.A.; Zambia, Japan, China, na mahali pengine. Bidhaa zinazonunuliwa nje ni trekta, magari na mengineyo yawezayo kusaidia ukulima.

Kijamii, Tanzania bado inao watu wengi wasiojua kusoma. Wanafunzi katika shule za msingi wanaanza kuongezeka. Kuna shule mbalimbali za sekondari. Pia kuna Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Chuo cha SOKOINE Morogoro ambacho hutilia mkazo katika kilimo.

#### HATIMA.

Yaonekana kuwa jamii ya Tanzania ilikuwa na mabadiliko kijamii, kisiasa, kiuchumi hasa baada ya uhuru kupatikana. Maswali mbalimbali yanajitokeza yakiuliza kama mabadiliko hayo yanafaa au hayafai. Na katika kazi hii, tutaona jinsi Kezilahabi anavyo kabili matatizo ya jamii yake ambayo inajengwa katika misingi ya ujamaa na kujitegemea.



## 2.2. Muhtasari wa kazi zinazohusika.

### 2.2.1. Rosa Mistika.

Rosa Mistika ni riwaya yenye kurasa 119 iliyogawanywa katika sehemu mbili kubwa na sehemu ndogo ya mwisho. Kizilahabi anatuonyesha katika kitabu hiki, jinsi ambavyo jamii za kiafrika zinavyopotea kutokana na mwingiliano wa taasisi za kigeni. Jambo hilo mwandishi analikabili akitumia dhamira ya malezi. Anawachora wahusika ambao wanaendesha mgogoro huo tangu mwanzo hadi mwisho mwa riwaya.

Mwanzoni mwa kitabu, mwandishi anatuchorea mji wa Zakaria ambao una maisha ya kusikitisha. Zakaria au "Majimachafu", jina lake la ulevi, ni mkristo ambaye aliwahi kuwa mwalimu na kufutwa kazi kwa sababu ya ulevi wake. Anawapa binti zake malezi makali yasiyoambatana na mila na desturi za kiafrika wala ulimwengu tuishimo. Mwenendo wake wa ulevi umeiweka familia yake katika umaskini kiasi cha kukosa nauli ya kumpeleka shule bintiye Rosa, ijapo mkewe, mama watoto wa kiafrika kabisa anajitahidi kuondoa hali hiyo.

Kigoli Rosa ambaye mwanzoni ni mwenye tabia ya kuvutia, anaharibika anapoingia shule ya sekondari ya Rosary inayoongozwa na Masista. Jambo hilo linatokea kwa sababu ya yale malezi ya kulindwalindwa aliyopewa na baba yake. Upotofu wa jamii unajitokeza hasa katika mhusika Deogratias, bwana maendeleo wa Mwanza "mmoja wa wale watu watumiao vyeo vyao na pesa kwa kupata chochote wapendacho". Bwana huyu anamlaghai Rosa akijidai kwamba atamwoa. Alipofika Morogoro T.T.C., tabia ya Rosa iliharibika zaidi, kiasi cha kupewa jina la "laboratory" yaani nyumba ya majaribio. Baadhi ya watu wanaoshiriki katika upotofu wake kuna Thomas mwalimu wake na mkuu wa shule. Rosa ambaye ni picha ya upotofu wa jamii za kiafrika dhidi ya taasisi ngeni, anajitahidi kurekebisha mwenendo wake baada ya kuma-



liza masomo, bila mafanikio. Kwani mchumba wake Charles anamkataa. Na Rosa ambaye hawezi kuishi katika dunia inayomkataa, anajua saa chache baada ya vifo vya baba na mama yake. Kwa kifupi mwandishi anaonyesha mgongano wa utamaduni. Katika kumaliza kitabu chake kama ifuatavyo "Homines interrogabo" yaani nitawauliza watu, mwandishi anamwalika kila mwafrika kujishughulisha na ulinzi wa utamaduni wake ambao unaharibiwa na taasisi za kigeni.

### 2.2.2. Kichomi.

Kichomi ni diwani yenye kurasa sabini na mbili, inayokusanya mashairi 42. Kitabu hicho kinagawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ambayo kichwa chake ni "Mashairi ya Mwanzo" ina mashairi tisa. Mashairi hayo kama asemavyo mwandishi(1) yaliandikwa kwanza katika lugha ya kiingereza, lakini yakatafsiriwa kwa ajili ya mtu atakayetaka kuona jinsi Kezilahabi alivyoanza kujitosa katika mashairi. Sehemu ya pili "Fungueni Mlango" ina mashairi 32 yaliyotungwa kwa Kiswahili. Mashairi yaliyomo katika kitabu hiki, isipokuwa shairi liitwalo "Dakika 15 za Uzalendo" (uk. 51-58), ni mashairi guni maana hayana vina na ulinganifu wa mizani. Ngonjera ya "Dakika 15 za Uzalendo" ina vina vya kati na vya mwisho, na ni yenye mizani 16. Mwanzo kuna dibaji ya Topan Farouk, inayofuatiwa na utangulizi wa KEZILAHABI mwenyewe.

"Yaliyomo, anasema TOPAN, ni mawazo ya kisasa, ni mawazo ya kijana aliyezungukwa na mazingira ya kisasa ya kisiasa, kielimu, kijamii, na hata ya kidini. Mambo aliyoyao-na na kumpata maishani na fikra zilizomjia kichwani zaelezwa katika mashairi haya. Hisi za ndani zimeelezwa kwa mtungo mpya. Mpangilio wa maneno katika mtungo huu waambatana na kufuatana na mtiririko wa mawazo ya mashairi toka mwanzo hadi mwisho."(2)

Na mwandishi anasema mwenyewe kuwa aliandika katika  
"sehemu ya kwanza [ ] juu ya mambo mbalimbali. Lakini



katika sehemu ya pili wazo moja hasa li(li) msumbua. Jambo lenyewe lilikuwa swali linalohusu maana ya maisha."(3).

KEZILAHABI anazungumzia ukoloni, uhuru na ujamaa. Anaona kuwa kuingia kwa ukoloni kulirahisishwa na baadhi ya Waafrika wenyewe (Hadithi ya Mzee uk.69). Ukoloni ukaja na kuharibu mambo mengi barani Afrika. Kuhusu uhuru, mshairi analalamika kuwa uhuru uliokuwa ukitegemewa haukufikiwa kikamilifu. Kwani watawala wapya wanamnyonya mwafrika kama vile alivyokuwa akifanya mkoloni (Hadithi ya Mzee uk.72). Tena ukoloni mamboleo unaendelea kuikabili Afrika (Vipanya, uk.49). Na mwandishi anawaita wananchi kupinga hali hiyo. Kuhusu ujamaa, mshairi anasifu ujamaa ambao ungetimiza lengo la kuijenga jamii bora ikiwa viongozi wangepanya kazi yao kama inavyotegemewa. Ni kweli kuwa kila mwelekeo wa kisiasa una mafanikio na makosa yake, hivi na siasa ya ujamaa ina kasoro na faida zake. Mengine anayoyazungumzia ni mgogoro wa wazee na vijana ama ukale na usasa, matatizo ya maisha ambayo ni magumu na yanahitaji kukabiliwa kwa ujasiri. Pia analaumu upotofu wa jamii kwa jumla.

### 2.2.3. Gamba la nyoka.

Hii ni riwaya yenye kurasa 151 na kugawanywa katika sura 14. Kitabu cha Gamba la nyoka kinazungumzia matatizo yaliyotokea nyakati za kuanzisha vijiji vya ujamaa nchini Tanzania. Mwanzoni kwa kitabu, tunawaona wananchi wakiwa na wasiwasi kutokana na maamuzi ya serikali ya kuwahamisha na kuwapeleka katika vijiji vya ujamaa. Uhamishaji huo unayakabili matatizo mbalimbali. Kwa mfano; tatizo la ukoloni mamboleo : Padri Madevu ambaye anasimamia ubepari anavuruga siasa nzuri ya ujamaa. Mahubiri yake yanawafanya Wana-Kisole waka-tae kuhamia katika vijiji vya ujamaa. Baada ya mapambano makali, Wana-Kisole wanashindwa na kuhamishwa kwa nguvu.



Padri Madevu ambaye hachoki kuisingizia na kuilaghai serikali mpaka alipouawa kwa ulozi, anashambuliwa kisiasa na wazalendo wa siasa ya ujamaa kama Mambosasa na Mamboleo.

Tatizo lingine ni viongozi wenyewe kutoelewa maaana ya ujamaa. Pia viongozi hao hawafuati kanuni za siasa ya ujamaa. Mwandishi anoonyesha jinsi viongozi wabichi-kina Mamboleo wanaweza kushindwa kutekeleza siasa nzuri ya ujamaa. Tunamwona jinsi Mamboleo baada ya kuchaguliwa kuwa kiongozi, anavyoharibu mambo, kwani zaidi ya kutoelewa siasa yenyewe ya ujamaa nia yake ni kumeza mali ya umma. Mwandishi anaonyesha kuwa ujamaa hautafanikiwa ikiwa viongozi kama Mamboleo wataendelea kuiongoza nchi. Mateso yanayowapata wakina Mambosasa na Mamboleo yanaonyesha kuwa uzalendo mtupu hauna maana kama haukuambatanishwa na siasa nzuri na vitendo. Ingawa pole pole maendeleo yalipatikana vijijini, kulikuwa na watu ambao hawakuelewa vizuri siasa ya ujamaa na waliotaka kuishi maisha yao ya jadi; kwa mfano Mze Chilongo ambaye anakataa mambo yote ya kisasa. Ukweli ni kwamba watu hao hawakuelewa maana ya vijiji vya ujamaa bali walipelekwa humo kwa nguvu na bila ya kuelimishwa. Mwandishi anaonyesha kuwa matatizo hayo yanayokabili siasa ya ujamaa ni kama "Gamba la nyoka", na yakiondolewa, ujamaa utafaulu kuijenga jamii yenye ustawi.

Inaonekana kwa kiasi fulani kuwa maandishi ya Kezilahabi yanazungumzia matatizo ya ujenzi wa jamii mpya. Isipokuwa kitabu cha kwanza cha Rosa Mistika, kinachozungumzia upotofu wa jamii za kiafrika kiutamaduni, vingine vinahusu mambo ya kisiasa kama tutakavyoona katika sura ifuatayo ya kuzichambua dhamira za mwandishi.

#### Tanbihi.

- (1) KEZILAHABI, E., Utangulizi wa Kichoni.
- (2) TOPAN, F., Dibaji ya Kichoni.
- (3) KEZILAHABI, E., Utangulizi wa Kichoni.



### 3. DHAMIRA.

"Dhamiri kubwa ya fasihi ni kuelimisha mtu apate kuelimika. Si wasomi wote wapatao elimu ya maisha ingawa wanayo elimu ya kisomo cha juu. Hivyo, fasihi ni somo lenye kujishughulisha na maisha ya watu. Huanzia mtu binafsi hadi mtu na jamii nzima, mahala pamoja hadi ulimwengu mzima. Ni somo lenye dhima kubwa kumwandaa mtu ili aweze kuchukuana na maisha popote pawapo."(1)

Hivi ni kusema kwamba fasihi ni mafunzo. Mafunzo hayo hutokea kufuatana na mawazo ya mwandishi ambayo anayazungumzia kufuatana na ujumbe ambao anataka kuutoa. Katika kurasa zifuatazo, ujumbe anaoutoa KEZILAHABI, yaani dhamira zijitokezazo katika maandishi yake zitachambuliwa kufuatana na nadharia ya kifungamano kama tulivyoona katika utangulizi. Maandishi haya yatachambuliwa kufuatana na nyakati za kutolewa kwa vitabu vyake, yaani kwanzia Rosa Mistika, halafu Kichomi na kuishia Gamba la nyoka. Uchambuzi huo utatuonyesha jinsi KEZILAHABI alivyofungamana na wanafilosofia na wasanii wengine katika kupinga ukoloni na maovu yake na pia katika kutafuta mbinu mpya za ujenzi wa jamii mpya.

#### 3.1. Mgongano wa utamaduni katika Rosa Mistika.

Kwa jumla, katika maandishi yake, Kezilahabi yasumbuliwa na wazo moja kuu ambalo ni upotofu wa jamii za kiafrika usababishwao na taasisi za kigeni ambazo ziliivamia Afrika wakati wa ukoloni. Kezilahabi huchukua vipengele mbalimbali vya maisha ya jamii kama vile mila na desturi, siasa na mengineyo kuonyesha maovu yaliyotendwa na ukoloni. Katika Rosa Mistika, mwandishi anaukabili upotofu huo kwa kutumia dhamira ya malezi. Ingawa kiini cha ujumbe wa Rosa Mistika ni malezi, kuna dhamira nyingine ambazo zinahusiana na kuambatana na dhamira hiyo kuu.



### 3.1.1. Tatizo la malezi.

Ili kuona msimamo wa Kezilahabi kuhusu malezi, yapaswa kwanza kuzingatia maana ya malezi, hasa misingi ya malezi ya kiasia. Inavyoeleza Kamusi ya Kiswahili sanifu, malezi ni "njia ya ukuzaji wa watoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki(2). Tunasoma tena katika "encyclopaedia" kuwa malezi ni "taratibu maalum itumikayo kuongoza na kufundisha vijana"(3). Mtaalam HUBERT anaongezea kuwa malezi ni

"mkusanyo wa matendo na athari zinazotendwa kwa hiari kati ya binadamu na binadamu mwingine, kwa mfano mtu mzima na vijana, akiwa na nia ya kuumba aina zote za tabia zinazolingana na maisha atakayokuwa nayo wakati apevukapo."(4)

Ingawa fasili hizi zinakamilishana na kulijumlisha wazo la malezi tukiacha ile ya HUBERT, zote zina kasoro. Maana hazitambui nafasi na athari ya jamii nzima katika malezi na uhusiano wake na utamaduni. Ni kweli kuwa malezi yanatokana au yanatakiwa kutokana na mfumo, na misingi ya utamaduni wa jamii fulani. Malezi ni kiini cha maisha ya jamii. Ndio maana Kezilahabi ameifunga dhamira nzima ya malezi katika maneno yafuatayo : "Amani duniani kwa watu wenye malezi mema."(uk.14)

Na katika kitabu hiki yaonekana jinsi malezi ambayo hayaambatani na mazingira na utamaduni wa jamii yanavyoweza kuharibu maisha ya wanaolelewa. Toka mwanzo hadi mwisho mwandishi anaonyesha jinsi mtu ambaye hakupata malezi mema asivyoweza kuonja maisha Jenye amani. Rosa Mistika, ni kitabu ambacho kinakabili mgongano wa tamaduni katika jamii iliyoingiliwa na taasisi ngeni. Mgongano huo unakabiliwa kitabuni kwa kutumia wazo la malezi. Upande mmoja kuna malezi kama yalivyokuwa yakijitokeza katika Afrika ya jadi. Upande mwingine, kuna malezi yanayoongozwa na kanuni za kigeni zina-



zotolewa na taasisi ngeni kama vile dini, shule, burudani za kigeni n.k.

Katika Afrika ya jadi, mtoto ni zawadi isiyo na kifani awezaye kuipata binadamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hivi hamu na haja ya wazazi ni **laumba** mtoto kikamilifu, apate kukua, kuaminiwa katika jamii na kutovunjia wazazi heshima. Tangu kuzaliwa hadi kuwa na uwezo wa kujiongoza mwenyewe, mtoto anahitaji wasaidizi. Wasaidizi ambao ni wazazi, ndugu na jamii nzima, wanaungana katika kumwonyesha njia ya kuishi katika jamii.

Kwa jumla, mama ndiye ampaye mtoto maongozi ya kwanza. Mama ndiye amfundishaye na kumwonyesha mwenendo wa kiutamaduni wa jamii yake. Malezi wanayoyatoa wazazi hasa ni ya kimfano, maana wazazi wanafanya jinsi iwezekanavyo ili watoto wawaige; kwa mfano, msichana kwa kumwiga mama na mvulana akimwiga babae. Mwigo wa kila siku unakuwa kama somo kwa watoto. Hivi familia inakuwa shule ya kwanza na ya muhimu kwa watoto. Na mwalimu ni mama, ndugu na baba kwani wanatoa maonyo ya mara kwa mara.

Kielimu, hata kijamii, watoto hufundishwa kwa kutumia hadithi, vitendawili na mengineyo yanayoihusu jamii. Katika hadithi watoto wanaonyeshwa mabaya yaliyowapata waovu, na mema waliyopata waadilifu na wenye maarifa; na kuwaacha wachague njia ya mafanikio maishani ili wasiangamie. Pengine vijana hufundishwa na wazee katika maongozi. Kwa mfano mambo ya kihistoria ya jamii yanasimuliwa kwa watoto kwa njia ya mdomo. Mambo ya sanaa kama vile vipengele kadhaa vya fasihi simulizi vinafundishwa na wazee. Utawaona wazee wakiimba majigambo na kuwalazimisha vijana kutunga mashairi yao. Mambo ya kiburudani yanafuata utamaduni wa jamii. Nayo ni michezo na ngoma zinazojitokeza hasa katika sherehe kufuatana na matukio mbalimbali.



Ingawa wote wanashiriki kumlea mtoto, kuna mambo ambayo yanahitaji mlezi maalum. Msichana ambaye anatarajiwa kuwa mke, mzazi na mlezi anaelezwa mengi na mama yake. Baba haingilii mambo yanayomhusu bintiye. Yeye atashughulika hasa na mvulana. Hata hivyo, mambo ya siri, vijana hufundishwa katika unyago. Unyago unanyoosha sana tabia na mwenendo wa kuishi kijamii. Kwa kifupi katika Afrika ya jadi binadamu anathaminiwa kwani ana akili na uhuru. Tena ni mtetezi na msimamizi wa yote anayoyatenda. Ana wajibu na haki ambazo zinamwelekeza kwenye kutenda jambo fulani ambalo haliruhusiwi kwuingiliwa na ye yote. Hivi malezi ni kazi inayofanywa na watu wazima kwa vijana ili kuwaonyesha na kuwaongoza katika njia halisi, na kuzikuza tabia zao kimwili, kiroho, kielimu na kiungwana. Wanawasaidia kuitimiza nasibu yao binafsi. Kwa hiyo, kulea katika Afrika ya jadi, sio kumjenga bali kumsaidia kijana kujijenga yeye mwenyewe. Malezi hayo, ambayo ni mazuri kwa jumla yana kasoro. Mara kwa mara yanatumia vitisho na adhabu ambazo zinapingwa na taaluma la kimalezi. Kwani vitisho hivyo vinamzuia mtoto kuwa huru katika maendeleo yake.

Malezi hayo katika kitabu yanaendeshwa na Regina. Wakati Zakaria anayatumia maongozi anayoyatoa kwenye taasisi za kigeni ambazo hazifahamu. Katika jamii zote za ulimwengu mtoto wa binadamu si kama mti unaokuwa peke yake na kutokana na jitihada yake binafsi. Rosa, mwanzoni alikuwa mwenye tabia na mwenendo mzuri, kama atuelezavyo mwandishi :

"Rosa alikuwa msichana mzuri, mrefu kiasi mnyenyekevu na mnyamavu. Kama akienda kuoga kisimani utamwona kabla ya kuvua nguo anaanza kuangalia huku na huko, huvua, huoga upesi upesi, huvaa, huchukua maji na kurudi nyumbani [...] alikuwa hapendi kuangaliwa kwa muda mrefu. Ukimwangalia machoni huinamishwa kichwa." (uk.9)

Mwenendo huo ulikuwa unafaa kwa wasichana kama Rosa. Lakini kama tulivyoona, mtoto wa binadamu anahitaji mtu wa kumsai-



dia katika kunyoosha tabia yake. Anategemea mengi kutoka kwa mama, baba na hata kwa jamii aishimo. Na wazazi ndio wenye madaraka juu yake. Kwa sababu Rosa ni mtoto wa kike, mamlaka hasa yalikuwa ya mama. Mtaalam MENDOUSSE anasema :

"Kwa jumla [7...7] mama ndiye peke yake mwenye uwezo wa kwanza katika kumfundisha (mtoto wa kike), kutokana na nguvu za sheria ya jadi. Yeye peke yake ndiye anayeweza kujua kwa undani zaidi hali ya kimwili na ya kihisi ya bintiye na anayejua kwa uhalisi maneno ya kumwambia na wakati unaofaa."(5)

Regina mama ya Rosa hakukosea katika kutimiza lengo hilo la kuwaelimisha binti zake. Alikuwa anajitahidi kuwalea watoto wake vizuri - si kisukari - kwani, kama mzazi yeyote mwenye maarifa, anajua kuwa "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo". Na kila siku, kila saa, alikuwa tayari kumwonya binti yake. Usiku kando ya moto, kama ilivyo katika desturi ya kiafrika, ndio wakati anaoutumia kuwaonya watoto. Tena anatumia hadithi na vitendawili. Kila mtoto anapewa maoni yanayolingana na umri wake. Hivyo maonyo haya yalipewa Rosa, msichana aliye-vunja ungo :

"Mwanangu, wewe sasa umekuwa mtu mzima. Karibu unakwenda huko ng'ambo Usukumani. Usitusahau sisi wazee wako, tuandikie barua mara kwa mara. Jambo moja hasa ningependa kukuhadhirisha : wavulana wakorofi. Huenda watakutaka mapenzi, nia yao ikiwa tu kukupa mimba itakayokukatisha masomo yako. Daima wakwepe hao. Na iwapo utakuwa mpumbavu na kupata mimba, usiitoe."(uk.17-18).

Onyo hilo ni zuri na lenye busara. Na linatolewa kwa njia isiyo ya ukali. Kweli "Regina alikuwa mwanamke mwenye busara ingawa hakuwa na kisomo chochote"(uk.18). Katika desturi za kiafrika, kuwa mlezi maarufu hakuhitaji kisomo rasmi, kisomo ambacho pengine, kama tutakavyoona kimempotosha Rosa. Mama hankatazi mwanawe kukutana na wavulana. Kwani wavulana huishi katika jamii na hawezi kuwaepuka - ila anamwomba tu kuchunguza na kuwa mwangalifu katika uhusiano wake nao.



Kwa desturi, malezi ya kiafrika si maonyo tu ya kila siku, bali pia ni matendo mema ya mlezi ambayo yanakuwa mifano wanayoweza kufuatia kwa hiari hasa wale wanaolelewa. Hivi, kando ya kuwavisha, kuwalisha na kuwaonya, wajibu wa mzazi ni kufanya bidii kuwaelimisha watoto wake kwa njia ya mifano. Watoto wanarithi mengi kwa wazazi. Ndivyo Regina aonyeshavyo anapojitahidi kuwafanya watoto wake wapende kazi. Regina anajiepusha na uvivu na bila msaada wowote kutoka kwa mumewe Zakaria; alijitegemea na kuwafunza wanawe kupenda kazi. Alikuwa anatimiza wajibu wa baba hali akiwa na ule wake wa kina mama. Na huo ni mfano wa uvumilivu ambao unatakiwa kufuatiwa na mtoto mwangalifu.

Malezi hayo yangalifaa, yasingaligongana na yale yasiyoambatana na utamaduni wa kiafrika. Miongoni mwake ni yale anayeyatumia. Zakaria ambaye aliwahi kuwa mwalimu na anayezikimbilia zile kanuni za malezi ya kigeni alizozipata huko shuleni, na ambazo hazifahamu kwa undani. Zakaria kama mlezi, anaamua kuwa askarijela akimbiaye nyuma ya wafungwa badala ya kuwa mshauri wa wale anaokusudia kuwalea. Je, kama mkristo, anafuatia mifano ya maonyo yanayotolewa katika Biblia? "Ninyi akina baba, msichokoze watoto wenu, bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana;"(6) au "Ninyi akina baba, msichokoze watoto wenu, wasije wakakata tamaa."(7)

Tunaona kwamba Zakaria anaepa maonyo hayo. Maonyo ya Baba si kuwachungachunga watoto. Hapa tunaugundua unyonge wake kidini. Ingawa watu kama Zakaria wanazikimbilia taasisi za kigeni, hawazizingatii vilivyo. Zakaria hazingatii malezi ya Biblia katika kuwalea watoto wake; tunaona kwamba anachungu binti zake katika umri wa miaka ambamo wanahitaji uhuru. Anasahau kuwa

"maisha ya binadamu ni kama mti. Mti unahitaji maji, hewa na mwanga. Kama mti ukinyimwa mwanga wa kutosha



na miti mingine, utarefuka [...]. Zakaria aliwamyima mwanga wakati walipokuwa wakiuhitaji sana."(uk.56)

Jambo hilo ni tokeo la mgongano wa tamaduni. Ingawa anazikimbi-  
lia taasisi za kigeni, Zakaria hazielewi, na hawezi kujiepusha  
kikamilifu na kanuni za jadi, tunamwona akitumia vitisho kiasi  
cha kumwaga damu ya bintiye. Yeye ananing'inia katikati ya  
tamaduni zote mbili. Tunaelezwa kitabuni kuwa Zakaria aliwahi  
kuwa mwalimu ama mlezi. Kwa kuwa alipata masomo ya namna ya  
kulea, ingebidi atumie busara na maarifa ya kiutu uzima kama  
ilivyo katika jamii za kiafrika. Je, ni elimu gani aliyopata  
huko mashuleni ?

Mwenendo huo bila shaka, Zakaria aliupata shuleni. Yasemekana kuwa hapo mwanzo, katika shule mbalimbali, ambazo kwa wingi zilikuwa zikiongozwa na wakuu wa dini, wanafunzi walikuwa kama wafungwa. Mfano ni katika seminari ambapo hawa-kuwa na likizo. Kosa filo tunaliona tena huko shuleni ambako bintize Zakaria waliokuwa wakisomea. Malezi mabaya waliyopata nyumbani kwao yaendelea huko shuleni. Shule hizi zilikuwa zikiongozwa na Masista. Na zilikuwa zikilindwa kiasi cha kutumia polisi. Kwa hiyo shule ilikuwa kama jela. Na hilo lilikuwa kosa kubwa kimalezi. Kwani waliwachungachunga kama wanyama waki-fikiri kwamba hili ndilo jawabu kama mwandishi asemavyo :  
"Wanafikiri hii ndiyo njia ya kuwazuia wasichana wasipate mimba! Hawa watu hawafahamu."(uk.74). Watoto wenyewe wanali-gundua kosa hilo, "... shule yetu hii ni ya ajabu. Tunalindwa kama watoto wadogo. Wanafikiri hata wakati wa livu watatuchunga ?"

Ni kweli kuwa kulindwa huko hakuzuii maovu; kwani wasichana wengi wanapata mimba hata wakiwa shuleni. Ndivyo tusomavyo :

"Shule hii! Hii hapa! Bure sana. Ingawa wanalindwa wanachukuliwa na wapishi wa wahindi mjini. Kwa saba-bu ya kulindwalindwa wamekuwa kama wanyama. Wanampe-



nda mtu yeyote apataye bahati ya kuonana nao. Wamepo-  
teza uwezo wao wa kuchagua."(uk.77)

Mambo hayo ndiyo yalimjia Rosa na akampenda Deogratias bila kuchunguza kwani hakufahamu mambo ya wavulana. Hata hivyo matatizo mengi yalimjia kiasi cha kumfanya "ashirikiane" na wasichana wenzake. Tunamwona Rosa akimrukia mwenzake Theresa na kumbusu lakini bila tamaa yake kupunguka, kwani kama aelezavyo mwandishi "moto ulikuwa ukiwaka upande wa kusini lakini wao walikuwa wakizimisha upande wa kaskazini"(uk.41).

Matendo hayo yanawakilisha shauku kubwa aliyoihitaji Rosa toka utoto wake mpaka siku hiyo. Mwishowe anakuwa kama mbwa aliyekata kamba. Na mabaya yote yanamkabili : utoaji mimba, umalaya kiasi cha kuitwa "laboratory" yaani nyumba ya kufanyia majaribio. Kiango anasema kuwa

"Rosa baada ya kuonja maji akawa anayanywa kwa pupa. Akawa mwingi wa habari na mkuu wa mambo. Baada ya kupata mwanga ambao alikuwa anafichuwa na kujua tamu ya mwanga akawa anazidi kuikimbilia ili azidi kuona utamu wake."(8)

Hivi alishindwa kutumia uhuru wake; na shule ilishindwa kumwongoza. Alikuta mambo mengi ambayo yanamweka katikati ya matatizo ambayo yanampa shida kuyatatua. Shule haimsaidii kurekebisha tabia yake, ila tu inamkorafisha zaidi. Shule naye inashiriki katika kumpotosha Rosa, haimpi mwenendo unaofaa. Kwa mfano mwalimu mkuu mwenyewe, Thomas anampevusha Rosa. Na anapoanza kulalamika, ndipo tunapocna mgongano kati ya malezi ya jadi alivyopewa na mama, na yale anayopewa na taasisi za kigeni.

Shida hiyo ya kunaswa katikati ya taasisi tofauti ambazo hawezi kuamua ni ipi inayofaa inajitokeza sana kitabu buni. Tunamwona Rosa akikata shauri kuenda densi. Na jinsi densi inavyokwenda naye polepole anaanza kuona kwamba kuna kitu fulani anachokosa. Anagundua kuwa yeye peke yake hawezi kujitosheleza. Lakini baada ya densi hiyo alikuwa



kama msafiri mpotovu mbele ya njia mbili tofauti na bila moyo wa kuchagua. Tunamsikia akiwaza : "Kama nikifanya urafiki na wavulana, baba atafahamu". Na anaongeza : "Yeye yuko Ukerewe, mimi niko Usukuma. Baba anakaa akinichunga, anafikiri atanioa"? (uk.40).

Baasi anaanza kuyapinga malezi ya baba yaani ya kigeni. Anaona kuwa itamlazimu kuishi na wavulana. Je, ataweza? Swali hili ndilo kiini cha mgogoro. Linaweza kuulizwa hivi : Je, Rosa ataweza kupatanisha njia mbili za malezi yaani kuunganisha taasisi mbili tofauti ? Jibu ni kifo cha Rosa. Na hapa ndipo tunajiuliza "kosa ni la nani ?"

Kama wazazi wanalifahamu kwamba tendo lao moja linaweza kuharibu maisha ya watoto wao, wangejitahidi kujua ugumu wa madaraka yao na kuzingatia kwa uangalifu yale yapasayo. Yaonekana kuwa kosa linatupiwa kwa wazazi. Lakini si kwao peke yao, kwani wanawakilisha jamii nzima. Maana jamii katika maisha ya Rosa, ilikuwa shahidi aliyeona kwa macho matendo yake na bila kutafuta sababu na suluhisho sahihi la matatizo yake badala yake anakimbilia kujiua. Jamii ndiyo isiyozingatia malezi yanayofaa. Jamii inashtakiwa. Zakaria anaaisimamia jamii iliyoteguka katika utamaduni wa jadi, inayozidi kupoteza misingi yake.

Kutojua njia ya kuchagua ni matokeo ya wakati. Dunia inageuka na ndisi tunaoigeuza. Basi yatupasa kuyaishi matukio sisi wenyewe. "Huu si ulimwengu wa kuambiwa [...]" Huu ni ulimwengu wa kutoka nje, ona, amua na tenda". Ikiwa binadamu anashindwa kufanya hivyo, hupotea. Ndivyo zishindwavyo jamii za kiafrika : labda zinatenda bila kuona na kuamua. Ndiyo sababu mwishoni mwa kitabu, Bwana Mungu anapatia uamuzi kwamba jamii ndiyo inayotakiwa kuchagua njia inayofaa kufuatana na kanuni zake za maisha na mfumo wake kuliko kufuata mfumo wa maisha ya jamii tofauti. Ikumbukwe



kuwa "nguo ya kuazima haisitiri matako". Tena "mpanda farasi wawili hupasuka msamba"!

### 3.1.2. Dhamira zingine.

Dhamira nyingine, kama ile iliyochambuliwa juu, zinahusu mwingiliano wa taasisi za jadi na za kigeni, mwingiliano ambao unaleta upotofu wa jamii za kiafrika.

Kwa mfano tukilichukua swala la ulevi tutaona kwamba kabla ya ukoloni kuingilia mila na desturi za kiafrika, ingawa kulikuwa na pombe na ulevi kwa kiasi fulani ambao ulikuwa ukipingwa, hapakuwa na mabaa au mahali panapouzwa pombe. Kilabu ni jambo la kigeni kabisa. Katika Afrika ya jadi, pombe inaambatana na nyakati maalum kama vile sherehe za aina kadhaa. Lakini vilabu vinalenga uchumi wa kifedha zaidi. Ulevi ambao unawapotoa wafuasi wake kama kina Zakaria, unatokea humo humo. Na unaleta maovu na shida nyingi. Tunamwona Zakaria ambaye, zaidi ya kuifukarisha jamii yake "anafutwa kazi kwa sababu ya pombe"(uk.10). Jambo jingine linalojitokeza ni kwamba Zakaria alikuwa haijali familia yake.

"Jirani zake (Zakaria) walisema kuwa alijali pombe kuliko watoto. Alikuwa hajatoa hata chapa kuwalipia watoto ada za shule[...]. Tangu Ijumaa mpaka Jumapili, Zakaria alikuwa anakwenda kunywa na siku zingine za juma alijifanya mgonjwa kitandani"(uk.11).

Udhaifu huo unamfanya asijenge hata nyumba. Na kinyongo cha kutoshiriki katika ujenzi wa mji wake, kilimfanya awe mkali, ili kuonyesha kuwa yeye ni mkubwa pale. Hayo, ni matokeo ya kilabuni! Hata kifo chake kilisababishwa na ulevi. Ikumbukwe kuwa kifo cha Rosa pia kilisababishwa na ulevi. Asingekunywa kupita kiasi, mchumba wake hangegundua kuwa yeye si bikira. Baada ya kugundua kwamba Rosa si bikira mchumba wake anaa-mua kumwacha. Alipoachwa Rosa ndipo alijiua.



Mambo hayo yote ni matokeo ya mila na desturi za kigeni. Si kawaida ya kigoli mwafrika kunywa pombe. Lakini tunamwona Charles akimkaribisha Flora pombe, aghalabu pombe ya kigeni. Pengine, wanawake wanaenda vilabuni na mabaa, ambako wanawanyonya wanaume. Upotevu wa wanawake unaimarishwa hasa na burudani za kigeni kama vile densi. Hata chimbuko la udhaifu wa Rosa lilijitokeza katika densi.

Upotofu wa jamii unazungumzwa katika vipengele vingi- ne vya maisha. Katika desturi za kiafrika uzazi ni jambo muhi- mu sana. Katika jamii ya kiafrika ya jadi, mtoto ni amana ya kesho na anategemewa sana katika kuwatunza wazazi na jamaa zake. Ndiyo sababu NDALO na BIGEYO, katika kitabu, wanasumbu- liwa sana na kutopata mtoto, na kufanya kila chochote wanacho- fikiria kuwa kinaweza kuwapatia mtoto. Wakati hawa wanakerwa na jambo hilo, tunawakuta wengine, hasa wale wenye kisomo, wakitoa mimba kama watakavyo. Mwafrika angeshangaa kusoma "Hakuna sababu ya mwanadamu mwenye akili kuamini kwamba utu- miaji wa vidonge vya kuzuia mimba unaingilia utaratibu wa ulimwengu kuliko mimba zitokeazo, mimba baada ya mimba"!

Upotovu wa jamii wapatikana tena katika udanganyifu na unafiki wa watu wazima ambao wangukuwa washiriki hasa kati- ka ujenzi wa jamii. Maafisa ambao ndio wanategemewa kuwa wa- jenzi wa jamii na mfano mzuri wa kuigwa ndio hao wanaotumia madaraka yao vibaya; kwa mfano, Deogratias ni mmoja kati ya wale watumiao vyeo vyao na pesa kwa kupata chochote wapenda- cho. Wanawakataza vijana kustarehe na wasichana, lakini ndio wanaowakorofisha. Kina THOMAS ambaye ni mkuu wa shule anawa- kilisha udhaifu na upotevu huo wa viongozi. Vile vile mkuu wa Wilaya ambaye anamchukua Rosa nakumtenganisha na babae. Basi hapa, wenye vyeo wanashtakiwa kuyatenda mambo ambayo hayalingani na sheria. Wanaotakiwa kuwa mfano wa kufuata sheria ndio wakorofi. Je, huo ni ungwana?



Tunaona kuwa taasisi za kigeni zimeleta kuteguka na kukanganyika kwa jamii. Katika jamii kadhaa za kiafrika kuna kanuni za kuhakikisha kwamba msichana anaolewa akingali bikira. Lakini leo miiko hiyo haitiliwi mkazo. Wavulana hukutana na wachumba zao kabla ya ndoa. Jambo hili halikuwemo katika desturi za kiafrika. Mgongano wa tamaduni unamfanya Charles ahakikishe ubikira wa mchumba kabla ya kumwoa. Bado anazikumbuka taasisi za jadi lakini anazichanganya na hizi za kigeni. Kwani anapoonja anafanya kinyume cha desturi. Na ikumbukwe kuwa "ukimwonya mchumba wako kabla ya ndoa si bikira tena, hata kama alikuwa"(uk.13). Hapa tunaona kuwa tabia za kigeni zimetuvunja kanuni nzuri ya malezi ya jadi ya msichana wa kiafrika.

Yote hayo ni matokeo ya mabadiliko ya wakati. Mabadiliko hayo yanaleta kuteguka kwa utamaduni ambao unahifadhiwa hasa na wazee na kuharibiwa na vijana. Hivi wazee na vijana wanashambuliana katika fani mbalimbali za maisha. Suluhisho la utengano huo, Kezilahabi analitoa anaposema : "Mapatanisho yanaweza kuletwa kama kundi moja likipiga hatua moja mbele na kundi jingine hatua moja nyuma". Je, itawezekana ?

#### HATIMA.

Kutokana na mhusika mruu yaani Rosa, ambaye anaendesha visa vyote vya hadithi, riwaya hii ya Rosa Mistika yaweza kusomwa kwa mitazamo mbalimbali. Tumeona humo ndani mwingiliano na mgongano wa tamaduni tofauti. Tatizo ni kwamba taasisi za kigeni ambazo zimeletwa na wakoloni, zinakubaliwa na kukimbiliwa na waafrika bila kuchagua jinsi ya kuzitumia kwa manufaa ya jamii za kiafrika. Taasisi hizo, kama vile dini, shule, burudani n.k. zimechukuliwa bila kuchunguzwa na zimeleta mgongano wa kitamaduni katika jamii za kiafrika. Inaonekana kuwa mambo hayo yalimfikia ghafla mwafrika, na



akayachukua bila kuyapima.

Rosa Mistika ni riwaya inayoeleza tangu mwanzo hadi mwisho malezi ya mtoto mwafrika wakati wa sasa na jinsi malezi hayo yalivyoingiliwa na taasisi za kigeni. Tunaona kuwa kijamii, Rosa yumo katika hali ngumu ya kielimu, kiadilifu na hata kidini. Akitoka katika familia ya kiafrika, kama mhusika mkuu, tunamwona Rosa katikati ya mgongano wa tamaduni, akiwa shabaha na sadaka ya misimamo miwili tofauti ya maisha inayopingana. Kwa upande mmoja kuna mwelekeo unaohifadhi mambo na desturi za jadi, nao unaendeshwa na akina Regina kitabuni. Kwa upande mwingine kuna mwelekeo wa kimapinduzi ambao unataka kubadili mwenendo wa jamii kwa kuzichukua moja kwa moja taasisi za kigeni. Mwelekeo huu wa pili uko karibu kushinda, hasa tunapowaona kina Rosa wakikimbilia mambo hayo ya kigeni. Shule inamwepusha Rosa na mazingira ya jadi na utamaduni na mila za kabila lake. Huko shuleni, Rosa anavumbua mambo mengi ya kigeni kama vile densi, mafundisho ya kuzuia mimba na mengineyo.

Lakini baada ya kumaliza masomo, tunamwona Rosa akiamua kurudia ule mwenendo wake wa mwanzoni. Jambo hilo linaonyesha hasara ya malezi ya shuleni pamoja na ya babae. Ina maana kuwa taasisi za kigeni zinashindwa kumwongoza. Maskini! "Maji yakisha mwagika hayawezi tena kuzoleka!" Hawezi kuupata tena ule mwenendo wa awali, ule aliokuwa nao alipokuwa mdogo. Mambo hayo yanamfanya ajiue. Kifo chake, ambacho kinamruhusu kutupilia mbali matatizo ama kushinda mgongano huo usio na suluhisho, kinakuwa njia ya kujikomboa. Hata kifo cha Zakaria kinaweza kuangaliwa kwa jicho hilo; kwani naye anachanganya mambo mawili tofauti, taasisi za kiafrika kama vile utani na taasisi za kigeni ambazo hazielewi kikamilifu.

Mwandishi anafungamana katika kupinga upotofu wa jamii za kiafrika, upotofu uliosababishwa na kuja kwa mko-



loni na kuimarisha taasisi zake, hivi akiondoa misingi ya jadi ya jamii za kiafrika. Ufungamano wake ni kama ule wa C.H. KANE, CHINUA ACHEBE, M. BETI(9), ambao wanalalamika juu ya upotofu wa jamii za kiafrika. Ingawa wanataka utamaduni wa kiafrika ushughulikiwe, msimamo wao si kama ule wa kina SENGHOR ambaye anataka kumfinya mwafrika katika ulimwengu wake, anapoagiza kushughulikia utamaduni wa kiafrika bila kuangalia tamaduni zingine; jambo ambalo haliwezekani. Ikiwa mwafrika anatakiwa kuishi vizuri katika dunia ya leo hana bu-  
di kushirikiana kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi na nchi nyingine. Tumeishaingiliwa na taasisi za kigeni na hatuwezi kurudia ile hali ya jadi kama vile Rosa alivyoshindwa kurudia ule mwenendo wake wa mwanzoni. Kinachotakiwa ni kuchukua katika taasisi za kigeni mambo ambayo yanaweza kuambatana na mazingira ya kiafrika. Yapasa kuunganisha ya jadi na ya sasa kwa kuchunguza na kuchagua yanayofaa kwa pande zote mbili, kwani kila upande una kasoro zake.

### 3.2. Dhamira katika Kichomi.

Kitabu cha kichomi, kama kionyeshavyo kichwa chake, ni diwani inayokusanya mawazo yanayomchoma mshairi na mwandishi KEZILAHABI. Mambo hayo yanayomsumbua yanaangalia fani mbalimbali za maisha kama vile siasa, elimu, jamii na mengineyo yawezayo kumpata binadamu maishani. Katika kitabu hiki, jambo linalozungumziwa hasa ni siasa katika stahili zake kadhaa, na jinsi inavyoathirishwa na mambo mbalimbali ya maisha ya jamii. Mambo hayo ndiyo tutakayozungumzia katika kurasa zifuatazo kufuatana na msimamo wa mwandishi mwenyewe. Hatuwezi kupitia kila shairi; kwa hiyo tutatoa maoni ya kijumla kwani kuna mashairi ambayo yanazungumzia dhamira moja, na baadhi yanayozungumzia dhamira mbalimbali kwa wakati mmoja.



### 3.2.1. Mwamko wa kisiasa.

"Katika dunia ya leo... uandishi wowote na sanaa yoyote ni ya matabaka maalum na inaelekezwa kwenye msimamo maalum wa kisiasa"(10).

Inajulikana kuwa fasihi haina budi kuambatana na mkondo pamoja na misingi ya historia ambayo fasihi inatumikia. Maneno ya MAO yaliyokiriwa juu yanapata maana yake hapa. Na Kezilahabi hakujiepusha na wazo hilo. Kama mwandishi mwafrika, anazungumzia siasa ya kiafrika kwa ujumla, na kama mtanzania anaongelea siasa ya Tanzania. Kufuatana na yaliyokabili bara la Afrika katika historia yake, mshairi anatupa jicho juu ya ukoloni, uhuru, ukoloni mamboleo na mengineyo yaliyotokea baada ya uhuru kama vile mwelekeo wa siasa uliochaguliwa na waafrika wenyewe kama vile ujamaa nchini Tanzania.

#### 3.2.1.1. Ukoloni.

Mshairi, katika mashairi kadhaa yaliyomo katika diwani hii, anaonyesha jinsi wakoloni walivyoivamia na kuichafua Afrika. Ni kweli kuwa kabla ya wakoloni kufika, Afrika ilikuwa na mila na desturi zake, utamaduni wake, kwa kifupi mfumo fulani wa maisha. Wakoloni wakaja kuzishambulia na kuzifuja jamii za kiafrika katika vipengele mbalimbali vya maisha. Lakini kama atuelezavyo mshairi, jambo hilo halikufanyika kwa urahisi. Mwandishi anatueleza katika shairi "Hadithi ya Mzee" kuwa waafrika walianza kupambana kwa kutumia silaha.

"Tukaamua kwa pamoja Mikuki kutengeneza  
ngao na zana zingine kisha tukapeana  
zamu ya kulinda mipaka"(uk.70).

Lakini mashujaa waafrika walishindwa kwa sababu ya silaha hafifu. Wakoloni wakaanza kuwapumbaza. Hii ni hatua ya kwanza ya ukoloni.



Waliposhindwa waafrika walianza kugundua shimo lililokuwamo kati yao na wageni hao. Tofauti haikuwa tu ya kimaumbile, hata kitamaduni hawakufanana. Hatua ya pili ikaanza, nayo ni kukimbilia mambo ya kigeni. Mwingiliano wa tamaduni ukaanza wakati waafrika walipoamua kujifunza mambo ya kigeni, mabaya na mazuri

"Likatufundisha lugha  
lugha hiyo ya nzige  
wanadamu tukaimudu  
tukawaona wazuri

...

wakatufunza na kula  
kula kama nzige  
yaani bila kushiba"(uk.71).

Hivyo ukoloni ulikuwa umesha anza, na Afrika kuanza kuharibika kijamii, kiuchumi, kitamaduni n.k. kwa kifupi, upotofu wa jamii za kiafrika ulikuwa umeshaenea. Na mshairi analalamika juu ya upotofu huo anapolilia Afrika ya asili katika shairi "Namagondo" mahali alipozaliwa kati ya ardhi na nyota. Anaeleza pia jinsi wakoloni hao waliinyonya Afrika, wimbo wao ukiwa

"Kuleni majani yoho!  
Vya chini tuachieni!  
Kuleni majani yoho!  
Mazao tuachieni!(uk.71)

Ni kusema kwamba wakoloni walikula Afrika, wakasambaa nchini, madini wakaongoa kiasi cha kuiacha maskini Afrika. Ndivyo mshairi asemavyo :

"Wanakijiji wenzangu isikieni sauti ya leo  
Nyota zenu, zimeanza kuzimika  
Jua nalo, sasa latoa mwanga hafifu  
Mtungi wenu wa bahati chini utazama  
kwani udongo wenu rutuba hauna tena  
Wakoloni waliufaidi siku zile za zama.

Basi mshairi anawaita waafrika kuungana katika vi-  
ta hivi na kuijenga Afrika kutokana na misingi thabiti ya



kiafrika ili kujirudishia heshima kwa kujiepusha na mambo ya kigeni waliyoyakimbilia bila kuyachunguza. Anawaonya waafrika wasiendeleo kuyajenga maisha yao juu ya misingi mibovu waliyopewa na wakoloni. Kwani hata yale ambayo waafrika waliyafikiria mazuri hayana misingi katika Afrika, ni unafiki mtupu. Elimu waliyoileta haikuwa sawa na ile iliyotolewa Ulaya, ilikuwa elimu ya kikoloni kwa madhumuni ya kutumiza matakwa ya kikoloni kama atuelezavyo katika shairi la "Kumbe"

Kumbe  
Kwamba elimu walotupa wale wakoloni  
Kama suruali iliyopasuka matakoni  
Kweli kama ng'ombe waliostushwa  
Na siafu tumetambua dhahiri  
(...)

Lo!lo!lo! tulikuwa tukichezewa!(uk.37)

Huu ni ufumbo anaoutoa mwandishi kwa waafrika wenzake ambao anaalika kushughulikia ujenzi wa jamii mpya kwa kutumia misingi mipya na inayoambatana na mazingira na jamii za kiafrika. Maovu na madhambi ya ukoloni anayoyaonyesha hapa si kwa kumfanya mwafrika amchukie mkoloni, hali ni kumwamsha aji-shughulishe kikamilifu na maisha yake. Makosa yaliyotokea zamani yasiye kuendelea, bali yamsaidie kuamua njia nzuri ya kumfikishia kwenye uhuru kamili.

### 3.2.1.2. Uhuru.

Akizungumzia uhuru, mshairi anaeleza jinsi uhuru huo ulivyopiganiwa; akiwasifu majasiri walioupigania na kuwakomboa wenzao. Kwa mfano anapomsifu Mkwawa anasema :

"Tone lako moja la damu lilitosha kuandika vitabu vingi vya uzalendo katika mioyo ya vizazi vilivyo-fuata Urithi mkubwa kwa Taifa la Tanzania na Afrika"(uk.59).

Lakini mshairi analalamika sana ya kuwa uhuru huo hauku--



tikana kikamilifu, kwani wale wakoloni bado wanaendelea kututawala, hapa mwandishi analalamika pia juu ya ukoloni mambo leo. Na anawaalika waafrika kuuondoa haraka, kabla haujaimarishwa kama ule wa mwanzoni.

"Mimi ninaona mgonjwa  
bado amelala kitandani

(...)

Miiba iliyomo ndani mwetu lazima  
Pia iondolewe upesi kabla haijaingia

(...)

Baada ya kuitoa tuvae viatu vya chuma  
Halafu tucheze nao mchezo wa siasa na uchumi"(uk.19).

Ni kweli kuwa mkoloni ameondoka, lakini sasa anajigeuza katika hali nyingine, na inawapasa waafrika kutofanya makosa yaleyale waliyoyafanya hapo mwanzoni. Inwabidi kuwa wajanja na waangalifu.

Hata hivyo waafrika wenyewe, wale majasiri waliopigania uhuru na kuwatoa ndugu zao katika hali mbaya ya ukoloni hawajiepushi na yale waliyokuwa wakipinga, bali nao wanawatia utumwani ndugu zao, na kuwanyonya kiasi ambacho wangependa kuirudia ile hali ya kikoloni. Katika "Jinamizi" mshairi anatoa maoni yake juu ya uhuru uliopiganiwa. Ingawa majasiri waliwashambulia wakoloni, lakini mwandishi anayaogopa "meno marefu" ya hao wazalendo.

Katika "Hadithi ya Mzee", mshairi anaeleza unyonyaji ~~kuo wa~~ waafrika kwa waafrika wenzao akitumia taswira ya nzige ambao wanakula mazao. Nzige hao wamo katika makundi matatu. Kundi la kwanza lilikuwa Waarabu, la pili likawa wakoloni wazungu, na la tatu ambalo ni urithi wa hayo makundi mawili yaani waafrika wenyewe, viongozi wa kisasa. Viongozi hao wanauendeleza na kuuhudumia mfumo wa kibepari ama kinyonyaji baada ya uhuru.



"Hao watoto wa nzige  
Au ni watoto wetu  
Tukashindwa kuwaua".

Watu hao ambao wananyanyasa wenzao, ingawa hawakubaliki katika jamii, ni vigumu kuwaondoa. Waafrika walifaulu kuwapiga na kuwafukuza kwa kiasi fulani wakoloni, na inawabidi kuamua siasa itakayowasaidia kuwapiga vita viongozi hao.

Zaidi ya hayo, waliopigania uhuru si wao wanaovuna mazao ya jasho lao. Ingawa walipigania uhuru "kuna watu wenye viganja vikubwa zaidi, vile vile wako wamezao upesi upesi" (uk.66). Hata hivyo anaonyesha kuwa hakuna uhuru wowote. Na mshairi anazidi kulalamika katika "Dhamiri yangu" akijifanisha na mbuzi aliyefungwa kamba.

"Namshukuru aliyenifunga hapa  
Lakini lazima nitamke kwa nguvu  
'Hapa nilipo sina uhuru'" (uk.38).

Ndiyo asemavyo pia katika "Funguoni mlango". Kwani viongozi wanaijenga jamii ya kibwanyenye na kikabaila, hivi wakiwakandamiza watu wa kawaida. Katika "Barua ya Mkata kwa Rehema" yaani barua ya maskini kwa tajiri, mshairi anaonya kuwa viongozi hawaridhiki, tena wanawashambulia raia kwa maneno machafu. Lakini mwandishi anawaonya viongozi kuwa macho kwani wanaangaliwa na kuchunguzwa na wananchi. Kama isemavyo methali ya Kinyarwanda "Uwiba ahetsa aba yereka uwo mu mugongo" yaani "Aibaye akinbeba mtoto mgongoni humfundisha" maana ukifanya maovu wakati watoto wanakuangalia nao watafanya vile vile. Na vijana wakifuatilia mfano wao, je, jamii itakuwaje ?

Tena kama asemavyo katika "Upepo wa wakati" viongozi hao wajue kuwa wanaweza kupoteza nafasi na vyeo vyao na kufanyiwa yale wanayoyafanyia wenzao. "Aliye juu mgonje chini".



"Watapanda na kushuka  
Na wataanguka kweli  
Wakisukumwa na upepo wa wakati"(uk.4).

Ingawa hawataki kushuka na wanapigania madaraja kila mara, siku itafika ambapo watafahamu ukweli, kuhukumiwa na kuona ubovu wa yale waliyoyarithi toka ukoloni. Mwandishi anaamini kuwa hali hiyo itashindwa na nguvu za haki na usawa. Tunasoma katika "Mto wa haki".

"Halafu alisikia kitu kama radi kutoka mbinguni  
Na umeme ulipiga moyo wake  
Alisikia sauti ya haki na usawa wa binadamu  
Kwa mda wa dakika moja alielewa ukweli"(uk.17).

Wanakandamiza wenzao hawakubaliki katika jamii kwani usawa ni jambo muhimu katika jamii. Tena viongozi wanalaumiwa kuwa wenyewe wanapingana. Na katika "Wanadamu tunawajuani" mwandishi anaeleza kuwa wote hao ni sawa. Hakuna haja ya kuendelea kubaguanana kwa kutaka kuonyesha kuwa wana uwezo zaidi wa kuongoza kuliko wengine. Wote ni sawa. Wanachotaka ni kupanda madaraka ili wapate kuwanyonya waliobaki chini.

Kezilahabi anaonyesha kuwa hali imechafuka na anawaita waafrika kujiepusha na hali hiyo kabla mambo hayajaharibika sana. Anawachochea waafrika kulikomboa bara lao, ku-liondoa katika hali ya ukoloni mamboleo, na unyonyaji wa viongozi na utawala mpya. Tena anawaalika waafrika wote kuungana kuwakomboa wenzao waafrika ambao bado wanakandamizwa na makaburu kama vile weusi wa Afrika kusini. Anasema katika "Kichwa na mwili"

"Bunduki! Harufu ya damu kutoka kusini!  
(...)

Uhusiano wa damu ndugu zangu mzito mno  
Na mapenzi ya Afrika nzima kama samaki na maji  
Bila kichwa ninasikia haki mwili mzima  
Na ninaona haja ya kushika bunduki"(uk.16).

Mwaliko huo ni wa kuwaita waafrika watumie silaha ili kuleta



ukombozi; kukubali kuwafia ndugu zao, kwani hata Mwanadamu aliokolewa utumwani mwa shetani kwa damu!

### 3.2.1.3. Ujamaa.

Hadi hapa, mshairi, ingawa alikuwa akiyagusa matokeo fulani ya nchi yake, alikuwa akizungumzia hasa juu ya Afrika kwa ujumla. Lakini kuhusu ujamaa na wazalendo wake ni swala la Tanzania peke yake. Kama ionekavyo katika mashairi kadhaa kitabuni, Afrika ina matatizo ya kutumia vilivyo uhuru uliopatikana kwa mapambano, na hata kwa kumwaga damu. Kizilahabi anaona kuwa matatizo hayo yanaweza kutatuliwa na siasa ya Ujamaa. Ujamaa ndio uwezao kuleta mazuri yaliyokuwepo kabla ya wakoloni kuichafua nchi. Lakini anajua kuwa ile hali ya zamani haiwezi kurudiwa, kinachofaa ni kuijenga jamii mpya kwa kutumia misingi ya jamii za asili. Anapolilia jamii ya zamani ambayo ilichafuliwa, anasisitiza katika "Namagondo".

"Yasikieni ya wataalam kwenu waliioletwa  
Sahauni ule wimbo wa zamani  
Zingatieni ya mbolea na ujamaa vijijini.

Ujamaa huo unaelezwa zaidi katika "Dakika 15 za Uzalendo". Baada ya kumsifu aliyeleta uhuru na kuuhifadhi uhuru huo ambaye ni Nyerere, anatumia madhumuni ya ujamaa :

"sasa sikia ya TANU, kazi na maendeleo :

- Azimio la Arusha
- Jeshi la kujenga Taifa
- Kuondolewa kodi ya kichwa
- Kisomo chenye manufaa
- Kutaifishwa kwa mabenki
- Kuchukuliwa kwa majumba
- Mwongozo wa TANU kutuongoza
- Ya anasa magari kukataliwa
- Na siasa ni kilimo"(uk.52).

Ingawa ujamaa unajaribu kutimiza lengo lake na baadhi ya viongozi kuonyesha uzalendo wao katika kuueneza, bado kuna



watu ambao hawana habari, labda kwa sababu ya uasi wao, au kwa kutojua jinsi ujamaa wenyewe unavyoendeshwa. Na mwandishi anawataka wale walio na wajibu wa kueneza siasa ya ujamaa kuiieleza kwa raia badala ya kuuwaangushia kama amri inayotoka juu. Na ndivyo yeye anavyofanya katika ngonjera hii ya "Daki-ka kumi na tano za uzalendo". Tunawaona wahusika fulani wakiuliza maana ya ujamaa, pengine kwa mwendo wa uasi. Hiyo ni njia ya kuwaamsha wale ambao mamlaka yao ni kueneza siasa ya ujamaa, ili wajishughulishie sana na kazi ya kuwaelezea wananchi siasa hiyo. Hivyo wananchi nao wanaweza kujishughulisha na siasa hiyo inayowahusu.

Kutowashughulisha wananchi wa chini, na kuufikiria ujamaa ofisini kunaweza kulifanya Azimio litoa maagizo yasiyo na mtazamo wowote juu ya mambo kama yalivyo, na kutoa maneno yasiyolandana na hali halisi ya nchi. Maswali wanayo-yaauliza wahusika kadhaa katika ngonjera iliyotajwa hapo juu, pamoja na malalamiko ya wengine ni namna ya kuonyesha haja na utaratibu unaohitajika katika kueneza ujamaa. Tunamwona kwa mfano mzee mmoja akiuliza

"Mwaka huu ni kilio, sisi hatuna mvua  
Tega vizuri sikio, huzuni itakuinua  
Nalo hilo Azimio, latuletea mvua ?  
Sisi twataka mvua, tupate piga horio.

Anaendelea "Niambie kwa mkato, kama laleta afua  
Je Azimio ni moto, hao tajiri kua  
Sisi tunao mafua, twataka dawa nzito".

Ni kweli kuwa ujamaa unahitaji maelezo zaidi hasa kwa watu wa kawaida. Ujamaa unazo nguvu na uwezo wa kuibadili jamii, lakini unatakiwa kuingizwa hatua kwa hatua badala ya kuyarukia na kuyabwambia mambo mengi ghafla. Lakini kama njia nyingine za kisiasa, ujamaa nao una makosa yake. Kila itikadi ina uzuri wake na ubaya wake. Katika "Kuchambua mchele" mshairi analalamika ya kwamba ingawa wanajaribu kujirekebisha na kujisahihisha katika maswala ya siasa, bado makosa yanajitokeza hapa na pale.



"Tukaanza kula  
Tukakuta bado mchnaga na chenga!  
Lini tutaula bila mchanga, bila chenga?"

Hata hivyo, kuna watu, kwa mfano baadhi ya viongozi ambao wanafanya mambo yasiyoambatana na maagizo ya ujamaa. Mshairi anawalaumu wale malenga wa ujamaa wa juzi ambao leo ndio wa kwanza kuupinga. Katika "Uliza wanaojua" Kezilahabi anasema :

"Wako wapi waliokuwa viongozi zamani  
Waliokitoa hotuba ujamaa kupigania  
Sasa wamestaafu ndio wafuga kuku  
Ndio wenye majumba ubepari kurithisha"(uk.60).

Kweli, kama wakoloni, nao ni wadanganyifu. Wanayoyasema hayaambatani na vitendo vyao ng'o!

"Ai! wako wapi wapenda ujamaa  
Waliopiga kelele juzi ?  
Kusema ukweli na kutenda  
Kumeambatana kama shoka mpini  
Usiku mchana, wema ubaya  
Wote tu wanafiki  
Ya wenzetu misiba kufurahia"(uk.24).

Ikiwa viongozi hawajiepushi na mabaya hayo ni wazi kwamba wananchi hawatapata mfano sahihi ya utekelezaji wa ujamaa. Kwa hiyo viongozi hawa hawana tofauti na wakoloni waliotunonyanya na kutugandamiza. Nchi za kiafrika zinayakabili matatizo mengi kama vile ukoloni mamboleo, unafiki na unyonyaji wa tabaka tawala. Na wito wa mwandishi ni kujiepusha na urithi huo wa unyonyaji tulioachiwa na mkoloni kwa kuimarisha siasa ya ujamaa tukishikilia kimsingi katika kanuni zinazoongoza siasa hiyo. Ingawa ujenzi wa ujamaa waonekana mgumu, itabidi kuukabili kwa kuteka katika mambo ya jadi, na bila kupoteza wakati kwa kuyafikiria hasa maovu ya wakoloni. Yaliyopita yalipita, tujenge wakati wa sasa kama asemavyo mwandishi :  
"Ya nyuma nisijali, ya mbele niyakabili".



### 3.2.2. Kuhusu jamii.

Kijamii, mshairi anayazungumzia mambo kadhaa ambayo kwa jumla yanatoa msimamo wa mwandishi juu ya upotofu wa jamii kutokana na mabadiliko ya wakati.

a) Kwanza tunaona mgongano kati ya wazee na vijana ama mgongano kati ya ukale na usasa. Mshairi anaona mzee kama mtu mwenye maarifa, mtu ambaye ameyazoea mambo ya ulimwengu, mtu ambaye vijana wanapaswa kuyaheshimu na kuyafuatilia maoni na maonyo yao juu ya mambo kadhaa yanayompata binadamu maishani. Anawalaumu vijana ambao wanakimbilia mambo bila kuyachunguza, na kuwafikiria wazee kuwa ni wajinga, na kuyaona mambo ya jadi hasa utamaduni wa kiafrika kwamba ni mabaya.

Inawapasa kuijenga jamii mpya wakipata misingi katika mambo ya asili, la sivyo "watasukumwa na mawimbi" na kutetemeshwa na kila kitu, kama aelezavyo mwandishi katika "Mwamba Ziwani"(uk.6). Ingawa wazee walipoteza nafasi yao katika ulimwengu wa kisasa, vijana wanapaswa kutojiepusha na busara yao katika maongozo ya leo. Kwani wazee hao, ambao ni wawakilishi wa wakati uliopita, waliona mengi - mabaya na mazuri - na kutokana na ujuzi wao huo, wanaweza kutoa mashauri yenye maana. Kwa hiyo wasitupiliwe mbali na kudharauliwa. Ndivyo tusomavyo katika "Mzee na Mzigo"(uk.38).

"Kula nimekula na sasa mwasema  
Niko nyuma ya wakati  
Lakini kama nungepita mbele  
(...)

Ningewambia siri ya miaka mingi".

Na anaendelea kuwambia katika "Ukucha wa mbwa" kuwa matatizo na misiba yote inayotokea, ni kwa sababu ya kuyakimbilia ya kigeni na kutoyafikiria ya kale. Hata hivyo, jamii imeshapoteza mfumo wake wa maisha na haiwezekani kurudi nyuma;



jambo la maana ni kutoa misingi katika wakati uliopita ili kujenga vilivyo wakati wa sasa na ujao, kama mtunzi asemavyo "mbele chui mweusi, nyuma mwanga". Maana mwandishi anaona kuwa wakati ujao utaharibika zaidi ikiwa mambo ya jadi na yaliyopita hayasaidii kuijenga jamii mpya.

b) Upotofu huo wa jamii, mshairi anauzungunzia katika vipengele mbalimbali vya maisha. Mwandishi, katika mshairi kadhaa anatupa jicho juu ya ndoa kama jambo la muhimu sana katika jamii. Katika "Hadithi ya kitoto"(uk.42), tunaona kuwa ndoa ni jambo la lazima, ndilo liwezalo kuwaachanisha wazazi na watoto wao, kwani kama isemavyo Biblia "msichana atawaacha wazazi wake na kuenda kuishi na mumewe, na wote wawili watafanya mtu mmoja". Hata hivyo mwanamume na mwanamke wanatakiwa kuishi pamoja bila kudanganyana wala kunafikiana. Mshairi analalamika juu ya kudhooka kwa familia za leo ambazo hazizingatii maana ya ndoa. Katika "Hutanihadaa", anatu-leza kuwa anayemhadaa mume au mkewe, afadhali auawe.

Kudhalika, katika "Hadija" tunamwona akilaumu wanawake wanaofanya dhambi ya kuwaloga waume zao. Pengine wake wanaopenda kuolowa kufuatana na utajiri wa mume hawa wanaonywa kuwa ukimbiliaji huo wa mali waweza kuwapotosha. Mshairi anaonyesha kuwa pesa si kiini cha maisha ya familia; jambo la muhimu ni kuaminiana na kushirikiana.

c) Jambo lingine linalozungumziwa ni utoaji mimba. Kama tulivyoona katika kurasa zilizotangulia, wazo la kutoa mimba ni wazo la kisasa na linapingana na jadi na msimamo wa dini. Jambo hilo ambalo lilikuwa kama mwiko katika Afrika ya jadi, sasa linakuwa la kawaida kwa kina dada. Na Keszilahabi anawambia kuwa "ingawa waue, na wasichana mimba watoe, sauti ya haki ipo daima kuwafukuza"(uk.47-48). Mambo yanachafuka zaidi ikiwa yote hayo yanaendeshwa na pesa na



taasisi za kigeni ambazo ni vyombo vya upotofu, kama mshairi atuelezavyo katika "Hadithi ya kitoto".

### 3.2.3. Dhana ya maisha.

"Kama Mungu angewauliza wanadamu  
Wanataka kuwa nani kabla ya kuzaliwa  
Hilo ndilo lingekuwa swala gumu maishani  
(...)

Wote wangetamani kuwa kinyume cha walivyo" (uk.64).

Ni kusema kwamba hakuna anayefurahia hali yake, na hili ni tatizo la maisha duniani. Kezilahabi anayazungumzia baadhi ya matatizo yanayoweza kumkabili binadamu maishani. Akizungumzia kifo, mwandishi anasema kuwa kinamchukua yeyote na kuacha katika mateso ndugu za yule aliyefariki. Lakini kifo kinaweza kuwa na maana ikiwa kinatokea kwa kupigania haki za binadamu kama anavyotueleza mshairi katika "Kichwa na mwili".

Vile vile, mshairi anazungumzia uzee. Siyo kifo tu kimsumbuacho binadamu, uzee nao unamtia mashakani. Na hakuna awezaye kuupea kwani "Njia ya maisha ni moja". Hata hivyo, uzee ni ishara ya busara na maarifa.

Matatizo yako mengi maishani na ni ya kila mtu. Hayatatuliwi kwa kuepwa bali lazima binadamu ayakabili. Hayo anayasema katika "Kisu Mkononi".

"Sasa kama simba-Mtu shauri nimekata  
Ya nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili  
Kwaujasiri na uangalifu..." (uk.13).

### HATIMA.

Yanayozungumzwa katika Kichomi ni mambo ya kisasa, yanayoikabili jamii ya mwandishi ambayo ni Afrika kwa jumla



na Tanzania, pia matatizo yanayomkabili binadamu yeyote. Hata hivyo, inajulikana kuwa ushairi unatoa hisia za ndani za mshairi, hivi yaliyomo katika kitabu hiki ni kama wito. Ufungamano wajitokeza katika shairi lake "Fasihi". Anajua kuwa fasihi ya kweli ni ile inayowatetea wanyonge na kuwashambulia waonevu. Mshairi katika diwani hii, anatoa mawazo yake kwa wanaoweza kuyazingatia, ili wayafikirie, na labda washirikiane naye. Ikumbukwe kuwa ushairi tangu harakati za uhuru, ulikuwa chombo cha kupigania haki za waafrika. Kama vile CESAIRE, DAMAS, Kezilahabi anafungamana kwa kutumia ushairi. Kisiasa anaweza kuainishwa katika waandishi wa kifungamano walioandika baada ya uhuru.

### 3.3. Dhamira katika "Gamba la nyoka."

Kama tulivyoona katika kurasa zilizotangulia, Gamba la nyoka, ni kitabu kinachohusu ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa nchini Tanzania, hasa katika kipengele cha ujenzi wa vijiji vya ujamaa. Mwandishi anaonyesha matatizo na makosa yaliyotokea katika kuanzisha vijiji vya ujamaa. Lakini chini ya kisa hicho, dhamira mbalimbali zinajitokeza, nazo zinahutanzia Tanzania, Afrika na hata binadamu kwa jumla. Baadhi ya dhamira zilizomo katika kitabu hiki zimezungumziwa katika vitabu vilivyotangulia hasa katika Kichomi. Ushairi huu umeonyesha hisi na manung'uniko ya mshairi juu ya hali fulani ya maisha. Kezilahabi amejaribu kutimiza na kuonyesha hali ya kufungamana zaidi kwa kuyaweka mawazo yake - kama yajitokezavyo katika Kichomi - hasa katika migogoro na migongano ya kitabaka. Chini ya mada ihusianayo na kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa, mambo yanayozungumziwa ni ya kisiasa katika vipengele mbalimbali.



### 3.3.1. Kuanzisha vijiji vya ujamaa.

Mojawapo ya kanuni za kueneza siasa ya ujamaa nchini Tanzania ni kuvijenga vijiji vya ujamaa ambavyo nia yake ni kuwakusanya watu katika kijiji ili washughulike na uzalishaji mali kiuajamaa na maendeleo yapate kuwafikia bila tatizo. Na katika kitabu hiki, mwandishi anaonyesha makosa yaliyofanywa katika kuanzisha vijiji hivyo na matatizo yaliyovizua kuenea kwa urahisi.

#### 3.3.1.1. Makosa ya kuanzisha vijiji.

##### a) Kuhusu utumiaji wa nguvu.

Dhana ya vijiji vya ujamaa, ingawa ni nzuri na ni ya kimaendeleo, jambo hili linatekelezwa kwa njia ambazo hazifai. Watu wanahamishwa kwa wingi kuenda kuishi katika vijiji hivyo bila mpango maalum, na mbinu zinazotumika katika uanzishaji wa vijiji hivyo sio sahihi. Hakuna maandalizi maalum kuhusu jinsi mashamba mapya yatakayoanzishwa na njia maalum za mgawanyo wa mapato. Badala yake, jambo hilo linafanywa kwa nguvu na bila maandalizi maalum. Nguvu hizo zinawafanya wananchi walaumu viongozi wa kisasa kiasi ambacho wanaona afadhali enzi zilizopita kuliko kuishi katika utawala huu wa vuguvugu ambao hautimizi matakwa yao. Tunamsikia mnyonge mmoja akinungunika "Tulipata uhuru kutoka kwa mwingereza bila kumwaga damu. Kwa nini tumwage sasa?" Utawala huu unakuwa mkali kuzidi kipimo, ndiyo sababu anapoulizwa kusimulia hadithi ya ukoloni, mzee mmoja, baada ya kueleza mateso waliopewa na wokoloni, anapaza sauti "Hao walikuwa wanaume!" Kama vile ange-sema afadhali wao, afadhali ukoloni kuliko hali hii mbaya isiyo na kifani.



Kezilahabi anaonyesha kuwa wananchi hawakatai ujamaa, bali hawanogewi na jinsi viongozi wanavyojaribu kuwaswagia, kuwasukumia na kuwaburuzia katika vijiji ambavyo walikuwa hawaandaliwa kuvifahamu lengo lake. Na ni kosa kubwa kuanzisha wazo hili jipya bila kuwaandaa kisiasa wanaohusika. Kwani "wazo hili la ujamaa limetoka juu na kuwaangukia wao kama jiwe zito walibebe"(uk.51). Wazo hili tunaona kwamba halipokelewi na wananchi, na baadaye linazuka tabaka lenye kulipinga eti kwa sababu hawaelewi umuhimu wake.

Tabaka hilo mwandishi analionyesha kitabuni hasa kwa kutumia wanakijiji wa Kisole. Watu hao, zaidi ya kupambana kisilaha na serikali, wanapambana kimawazo. Kwa mfano, walipokalishwa vijijini kwa nguvu, tunawaona wanakijiji hao wakikataa kujifunza mambo ya kisiasa na kuchanachana madaftari. Ina maana kuwa, kwa kushambulia vyombo vya kufundishia, wana-shambulia mwalimu na serikali yake. Mwalimu amekuwa kama mtu-nga sheria yaani hakimu ambaye anatoa adhabu kwa watu wake. Ebu tumsikie Mwalimu MAGAFU akitoa maonyo kwa wanakisomo : "Atakayemkataza mke wake kusoma atachukuliwa hali kisheria. Chezeeni mambo mengine lakini msicheze na sheria"(uk.95). Basi mwalimu anakuwa mtesaji. Anakusanya nguvu na uwezo wote kisiasa. Hivi kunatokea mgongano wa kiitikadi na uhusiano wa mwalimu na wanafunzi wake unakuwa wa kisiasa.

Hata hivyo, kuhamishwa kwa nguvu na bila mpango sahihi kunaharibu mambo kiasi ambacho mwishowe kunatokea maagizo ya kuwahamisha tena eti kwa sababu vijiji havikupangwa sawasawa, watu hubanana na hali Tanzania kuna bado ardhi ya kutosha. Pia nyumba zimejengwa haraka haraka na mahali pabaya. Wanakijiji wanalalamika na kusema : "Tumehama na kujenga nyumba kwenye rutuba. Sasa tutalima wapi ? Kule mchangani". Na hii ni dosari moja iliyofanywa na serikali katika kutimiza lengo lake la kujenga ujamaa.



b) Kuhusu demokrasia.

Demokrasia inafafanuliwa kama "utawala wa jamii kutoka kwa jamii na kwa makusudi ya jamii". Ni mfumo muhimu katika nchi ambayo inatarajia kuongozwa na siasa ya ujamaa. Kitabu chatuonyesha serikali yenye kutumia nguvu katika kutimiza malengo yake. Uhusiano wa wananchi na viongozi ni wa woga. Pia hakuna majadiliano. Wananchi hawapati nafasi ya kujadili mambo yanayowahusu. Mwandishi anatumia kuwa wananchi

"wakawa wananyamaza lakini moyoni mwao wazito; wakitaka kusema lakini wakashindwa kusema, wakitaka kuuliza lakini wakashindwa kuuliza, wakitaka kukataa lakini wakashindwa kukataa"(uk.30).

Mambo mengi yanawachukiza lakini wanaogopa kusema kwani serikali ina nguvu sana. Wananchi wenyewe wanakiri kwamba hawana uhuru wa kutoa maoni wala uhuru wa kusema : "Siwezi kuitaja kwa usalama wangu, maana siku hizi hata kuta na miti ina masikio"(uk.55) anasema Mamboleo akiogopa kuilaumu serikali. Watu wanavumilia na mwishowe wanafikia hatua ya kutenda maovu. Tunawaona wanakijiji cha Bucho wakilazimishwa kuwapiga vita wenzao na kuwahamishia katika vijiji vya ujamaa. Wenalishughulikia jambo hilo lakini "kwa kutazama sura zao, ilikuwa vigumu kutambua kama walikuwa wakifurahia jambo waliotumwa kutekeleza au la!"(uk.21). Yaonekana wazi kuwa misingi ya siasa ya ujamaa haifuatiwi, hivi mwandishi analaumu baadhi ya njia zilizotumiwa na serikali katika kutimiza lengo la siasa ya ujamaa.

c) Dhuluma.

Mojawapo ya nia kuu za siasa ya ujamaa ni kutetea haki na usawa kati ya binadamu. Lakini kufuatana na manung'u niko ya baadhi ya wahusika kitabuni, yaonekana wazi kuwa nia hiyo haikutimizwa katika uanzishaji wa vijiji vya ujamaa. Kama tulivyoona dhana ya vijiji vya ujamaa si mbaya, lakini



inatekelezwa kwa njia zisizofaa. Wahamishaji hawazingatii maswala ya usawa hasa wakati wa kuhamisha watu. Watekelezaji wenyewe ndio waharibuo matakwa ya ujamaa. Tunawaona wapimaji wakiepa majumba ya makabaila na kuyaangusha yale ya watu wa kawaida. Wapimaji ambao wanapenda "kula milungura" wanachukua pesa za matajiri ili wasiwabomolee majumba. Pia watu wanahamishwa kutoka sehemu moja kuenda nyingine ili kusalimisha nyumba nzuri za makabaila.

Hata hivyo, kuna ubaguzi katika kujenga vijiji na vijiji vya ujamaa. Kuna mikoa ambayo imeachwa "katika hali ya ukabaila kwa kisingizio ya kuwa imeendelea"(uk.55). Hata baada ya kuishi vijiji, usawa hauwezi kupatikana. Mashamba hayagawanywi kwa usawa. Mashamba ya watu binafsi yanapitana. Wakubwa wanachukua mashamba makubwa na yenye rutuba. Muundo wa vijiji bado unawaruhusu makabaila kuwafanya ndugu zao watumwa. Wakubwa na wafanyakazi wa serikali wanagandamiza wanakijiji. Pia wenye mali ndio washikao madaraka, na madaraka hayo wanayashika ili "kulinda mali yao isiingiliwe na kimbunga cha ujamaa"(uk.101). Hivi tunaona wafanyakazi wakiliumba tabaka la wanyonyaji.

Udhalimu huo wa kijamii wapatikana pia katika ubaguzi wa mke na mume. Unyonge wa kina mama nao unazungumzwa. Swali la ukombozi wa kina mama ni la msingi katika ujenzi wa jamii yoyote inayoheshimu na kupigania haki za binadamu. Lakini tunamwona mwanamke akigandamizwa na kunyang'anywa vyeo eti kwa sababu ni mwanamke. Kwenye ukurasa wa 131 tunasoma kuwa :

"Katika uchaguzi wa Wabunge Mama MZURI angeweza kushinda, lakini kwa kuwa katika historia ya kisiwa palikuwa hapajatokea wakati ambao kisiwa hicho kilitawaliwa na mwanamke, alishindwa".

Kuhusu dhamira hii ya usawa, ni kama mwandishi angetoa maswali mengi juu ya siasa ya ujamaa : Je, ujamaa



utajengwa kwa hiari ? Ujamaa una maana gani katika jamii ambayo bado inaishi katika ubaguzi wa kitabaka na kimaumbile ? Ili pawe na ujamaa halisi, ingefaa wadhalimu wapinduliwe, kama vile alivyofanywa Mambosasa; pasiwe na wanyonge na wanyonyaji, tabaka la wanyonge lishike hatamu, likiongozwa na nadharia sahihi ya ujamaa. Hata hivyo ujamaa hauwezi kujengwa. Ni muhimu kuishirikisha jamii yote, na kujenga jamii ambayo makabaila wanasalimu amri na kulazimishwa kufuata kanuni za ujamaa bila ubaguzi wa kitabaka wala kimaumbile.

d) Udhaifu wa viongozi.

Viongozi, katika kitabu hiki, wanaliyenga tabaka ambalo lengo lake, badala ya kueneza siasa ya ujamaa, ni kujitajirisha kwa haraka haraka kwa kuwanyonya ndugu zao kama alivyokuwa akifanya mkoloni. Ndiyo sababu kila mtu anafanya jinsi awezavyo ili ashike cheo cha juu apate kutajirika badala ya kujitahidi kulitimiza lengo la ujamaa.

Jambo hilo la kutaka kulundika pesa haraka haraka linawafanya wale "milungura" yaani rushwa katika kazi zao. Tuliishaona jinsi, katika kuwahamisha watu vijijini, jinsi watu walivyotoa pesa ili nyumba zao zisibomolewe, na hivyo kuufanya mpango wa serikali uharibike. Hata mkuu wa wilaya amekula pesa nyingi wakati wa kuhamishwa. Tunaambiwa kitabuni kuwa hongo zilizidi kipimo. Tunamwona Mambosasa akipokea "bahasha" ili aje kumruhusu mzee MASHARUBU kujenga duka mahali palipotarajiwa kujengwa duka la ujamaa. Sio kula hongo tu, hata mali ya jamii wanameza bila kusita. Alipopata cheo Mambosasa, alimaliza pesa za kijiji eti kwa sababu hata wale waliomtangulia nao walikula. Mwandishi anaonyesha kuwa jambo hilo limeisha enea nchini kwote kiasi ambacho tunamsikia mhusika mmoja akilalamika "Wanaoaminika kazini wachache sana Tanzania ya leo". Kwani kazi inakuwa chombo cha kufanya kila



kiwezekanacho ili kujifanyia maisha bora zaidi kuliko yale ya watu wa kawaida. Na uaminifu wa watu wa chini unakuwa faida kwa viongozi wa juu.

Pia tunawaona viongozi wakitumia vibaya vyeo vyao. Tunamwona mkuu wa wilaya akishtakiwa kwa kutembea ovyo na watoto wa shule. Tunamsikia mkewe Mambosasa akiwaonya mumewe na Mamboleo "Malaya wakubwa nyie. Mlipokuwa na vyeo pesa mlimaliza kwa kuwahonga wanawake vijijini"(uk.112). Mambo hayo ni ya kukatisha tamaa na kuwaambukiza uvu huo wale wawaangaliao, hivi kuipotosha jamii zaidi. Hayo yanaelezwa na Mambosasa ambaye anasema :

"Nilikuwa na moyo wa uanamapinduzi, na Tanzania nilipe-nda sana. Lakini matendo ya viongozi wetu yamenikatisha tamaa. Imenibidi nami nianze kuwa kama wao"(uk.102).

Je, ukorofi huo unaweza kuijenga jamii yenye ustawi, ikiwa viongozi wote wanakuwa kina "Malyangu"?(11)

Tena viongozi wanalaumiwa kutoishi vijijini ili waweze kuelewa mambo kama yalivyo huko vijijini, wapate ku-yashughulikia kwa maarifa maendeleo halisi ya taifa. Ndivyo mwandishi atuelezavyo :

"Wanamapinduzi halisi ni wale waishio vijijini, wanao-athiriwa na upepo wa wakati unaowasukuma mbele kutoka walipokuwa. Wanatazama kwa uangalifu kila badiliko linalohusu maisha yao"(uk.150).

Viongozi wanatakiwa kuenda vijijini ambako huduma yao inahitajika. Lasivyo :

"uzuri wa kulala katika nyumba za ghorofa na "flats" zenye vyoo ndani, maji na umeme, hauwezi kuwazuia wananchi kufikiria... kama wanaona mazao yao yana-haribika na hawapati utaalamu kutoka kwa wataalamu, wala hawaoni viongozi wao wakienda vijijini kwao, kuonyesha ubingwa wao wa kuongoza kwa kuelimisha, kufundisha, kuhimiza, kuelekeza na kuonyesha kwa njia ya vitendo"(12).



Kwa kifupi, mwandishi anaonyesha udhaifu wa viongozi katika fani mbalimbali za maisha. Viongozi hao ambao nia yao ni kulundika mali na kufanya maovu ya kila aina si wao watakaoneza ujamaa. Viongozi wa kina Mambosasa ambao wanapiga domo tu mambo wasiyoyaelewa. Ujamaa unahitaji watu wanaoufahamu kimsingi, wanaouendesha kwa busara na maarifa aghalabu waadilifu.

e) Unafiki.

Ni kawaida kuwa itikadi yoyote, ili ifanikiwe haina budi kutoa ahadi itakazotimiza. Kitabuni tunaona kuwa kabla ya kuwahamishia vijijini wanakijiji waliahidiwa mambo mengi kama vile mabomba ya maji, hospitali, mpango maalum wa kuzalisha mali kwa ushirika na mengineyo. Lakini kama ijitokezavyo katika malalamiko ya wahusika kitabuni - mojawapo akiwa TINDA (uk.108-109) - ahadi hizo hazikutimizwa. Na mhusika fulani anasema kuwa "wakati mwingine siasa inakuwa kama bangi. Huwa inalevya na kusema maneno mengi"(uk.22), maneno ambayo hayakufikiwa kwa undani, na kuwadanganya raia.

Unafiki huo unapogunduliwa mambo yanakuwa magumu zaidi. Tunawaona wakazi wa kijiji cha ujamaa wakilalamika juu ya unafiki huo wa serikali, kwani miaka mingi imepita na ahadi walizopewa kabla ya kuhamia vijijini bado hazijatimizwa. Mwandishi anatueleza kuwa :

"mioyo yao ilikuwa ikihesabu kila pigo kwa tumaini la kuona maajabu yaliyoahidiwa na serikali, ilikuwa imeanza kuchoka...mioyo yao ilikuwa ikisema kimya kimya "Nyerere ametudanganya""(uk.66).

Si ahadi tu za kutia moyo, lakini hata nia za siasa ya ujamaa hazitimizwi. Mengi yaliyoahidiwa kuwa mali ya wananchi wote yanawaendea wale wenye vyeo tu. Kwa mfano "bomba la maji lilifika tu karibu na nyumba ya mkuu wa shule za msingi"(uk.108).



Hata hivyo, mambo yameharibika zaidi. Badala ya kuwa na mapato ya kuridhiisha, "umaskini ndio sasa unazidi". Na mnyonge anashangaa, "ujamaa maana yake ni kushuka chini!" (uk.101). Wananchi wamegundua uongo wa viongozi na hapa wanaling' unika kuwa wamedanganywa. Wamegundua kuwa ujamaa unajimbwa kwa ulimi tu, kimatendo hauko; bali ubeberu ndio unaendelea. Na Mambosasa akitazama jinsi mabwana wenye vyeo wanavyo karibishwa kiasi ambacho wanamwaga chakula na hali pengine wananchi wanakufa kwa njaa, anauhakiki ujamaa na kutoa maoni yake kwa kusema "unafiki mtupu!" (uk.125).

Pia anaendelea kusema "nimechoka kudanganywa na wanasiasa Wanajitahidi kumeza chochote kabla ya ujamaa kuingia" (uk.139). Ni kweli kuwa siasa ni nzuri kwa wale wanaopata faida yake. Basi viongozi na serikali kwa jumla ni wanafiki. Nia yao ni kudanganya watu ili wapate kuwanyonya bila shida kama walivyofanya wakoloni na wanavyoendelea kufanya katika ukoloni mamboleo wakati sisi tunajidai kuwa na uhuru. Mwandishi anatufundisha hivi kuhusu ujenzi wa jamii mpya : juhudi ndizo huimarisha ujamaa, siyo kupiga domo tu. Ni kweli kuwa ujenzi wa ujamaa unahitaji ujasiri, tahadhari na mbinu sahihi za utekelezaji.

### 3.3.1.2. Matatizo.

#### a) Ukoloni mamboleo.

Ukoloni mamboleo ni tatizo gumu ambalo nchi zinazoendelea zinapambana nalo. Ni kweli kuwa baada ya "uhuru" kupatikana, Afrika kulitokea njia na miongozo mbalimbali ya kisiasa kufuatana na uchaguzi wa nchi zilizopata uhuru. Nchi kubwa zenye siasa zao zilitarajia kueneza siasa hizo barani Afrika. Ndivyo Nixon asemavyo, anapofasili Afrika ya siku chache baada ya uhuru kama uwanja thabiti wa mighalaba kati



ya nchi za kibepari na kisoshalisti.

Katika kitabu hiki, ugomvi huo wa kiitikadi unaonyeshwa wazi wazi. Mahubiri yote anayoyatoa Padri Madevu ni ku-laumu na kuonyesha uovu wa siasa ya kisoshalisti, na kusifu siasa ya kibepari ambayo anaonyesha ubora na umuhimu wake. Tunamsikia akiwahubiria Watanzania.

"Mmekubali kudanganywa na wanasisia wenye njaa ya kushiba kama mbwamwitu. Mnakubali ukoministi, hamjui shida ya ukoministi? Leo nchi yetu ya Marikani inawalisha Warusi [...]. Nanyi mtakapoona nchi nzima ina njaa jueni mashetani ya kikoministi yamewaandama" (uk.5).

Nia yake na kazi yake, chini ya udhuru wa upadri, ni kupinga ukoministi ili siasa yao idumishwe nchini Tanzania, wapate kuinyonya bila shida. Ndiyo sababu anajitahidi kuonyesha umuhimu wa ubepari, na uwezo wake.

"Tazameni, Padri Madevu anasisitiza, miaka mingapi imepita tangu Marx aseme kwamba jamii za kibepari zitaanguka? Karne zimepita na nchi kama Marikani ndipo inazidi kuchanuka na kuneemeka kiasi cha kuweza kuwalisha wakoministi ulimwenguni" (uk.65).

Sio kueneza siasa tu, bali ni kutafuta njia ya kuwanyonya Waafrika ambao wanajidai kuwa na uhuru. Ukweli ni kwamba hakuna uhuru wa kisiasa bila uhuru wa kiuchumi. Na nchi za kiafrika ni fukara na zinahitaji misaada kutoka nje. Ndivyo mwandishi atuelezavyo ya kuwa "baada ya uhuru Tanzania haikujitegemea na bado haijajitegemea [...]. imekuwa ikitegemea misaada ya nje kwa maendeleo yake" (uk.66). Lakini ikumbukwe kuwa hakuna nchi inayotoa misaada bila kutegemea kupata faida. Bila faida, hakuna kitendo! Hivi kweli unyonyaji bado unaendelea. Na mwandishi anaeleza kuwa ni vigumu kujiepusha na hali hiyo ikiwa nchi za kiafrika zingali maskini. Mzungu bado anatutawala; ameshaendelea, nasi kazi yetu ni kumfuata kama vifaranga vilivyoanguliwa katika mayai ya kuku mwingine. Hilo ni tatizo gumu kwa maendeleo ya Afrika.



Tena mataifa makubwa huyatumia mashirika ya upelelezi ili kuhujumu serikali na kuangusha uchumi wa nchi zingine kwa manufaa yao. Serikali ambayo haifuatii matakwa yao huanushwa. Hawa ndio waongozao nchi za kiafrika. Ndio wanawakubali au kuwapandisha madaraka viongozi wa Afrika. Ndivyo mwandishi atuelezavyo akimtumia Padri Madevu : "Tazama serikali yenu ilitaka kupinduliwa nani alimsadia Nyerere ? Mwingereza. Yule yule ambaye sasa mmamwita beberu"(uk.64). Ni kusema kwamba fujo zote zinazotokea katika Afrika zinaletwa na nchi kubwa duniani. Hivi uhuru hauwezi kupatikana kikamilifu kwani bado tunanyonywa na kutawaliwa na nchi za kigeni. Kwa hiyo ni vigumu kwa nchi za kiafrika kujichagulia mwelekeo maalum wa kisiasa, kwani zinaongozwa na zile zilizoendelea.

b) Mgongano wa wakati.

Maendeleo ya nchi zetu yanapambana na ukuta wa wakati. Taasisi mpya ambazo hasa ni mali ya mkoloni, zinatumiwa katika mazingira ambayo hayawezi kulandana nazo; au pengine hazikubaliki kwa urahisi hata zikiwa za kimaendeleo. Kwa mfano kitabuni, walipopewa bomba la maji wanakijiji, "kulikuwa na wazee ambao hawakufurahia jambo hilo [..] wali-ona kuwa bomba hilo lingewaharibia utamaduni"(uk.149).

Mgongano huo unawatenganisha wazee na vijana. Wazee wanaulilia wakati uliopita ambapo walikuwa mashujaa waheshimiwa. Wazee hao wanawalaumu vijana wa leo ambao hawawezi kuwaongoza vilivyo. Vijana hawa badala ya kuongozana yao ni kuwachanganya mawazo watu, kutokana na vuguvugu la taasisi za kigeni ambazo wanazikubali bila kuzichunguza. Wazee wanasikitishwa sana na mwenendo wa vijana ambao wanataka kujiepusha na mambo ya jadi kama vile utamaduni.

Msimamo wa mwandishi juu ya swala hilo unajitokeza katika tungo hizi mbili : "Mwewe hushinda angani lakini jioni



ikifika hulazimika kutua porini" na "ukale una wakati wake, ukale unastahili kuchunguzwa". Ni kusema kwamba watoto hawa-wezi kujiepusha na mambo ya jadi ikiwa wanataka kujenga usasa. Utamaduni ndio uongozao jamii; kuutupilia mbali ni kuizima jamii hiyo. Mwandishi anaona kuwa utamaduni unaweza kuvunja utengano huo na kuwaunganisha vijana na wazee. Tunaelezwa kikatuni kuwa "kulikuwa na jambo moja ambalo liliwafanya wana-Bucho waseme na vijana hawa yaani Mambosasa na Mamboleo bila woga wa elimu yao, walikuwa wakishiriki katika ngoma zao". Ngoma hizo zinawakilisha utamaduni mzima. Kadhalika mwandishi anawafundisha vijana kuchuma katika mambo ya kale ili kujenga kimsingi wakati wa sasa, sio kurukiarukia tu mambo ya kisasa. Ndivyo Mzee Farjalla asemavyo akiwaonya Mambosasa na Mamboleo : "Mkiwa viongozi, heshimuni wazee. Msifikiri kuwa kila wasemacho ni upuuzi"(uk.74).

Onyo hili linatuonyesha pia kuwa kila wasemacho wazee si chenze maana na kinahitaji udadisi. Ndivyo tusomavyo kwenye ukurasa wa 150 : "Ukale una wakati wake, ukale unastahili kuchunguzwa lakini haudumu milele". Pengine angesema kama BADIAN "Ulimwengu unabadilika, na yatupasa kuishi wakati tulio nao"(13). Ni kusema kwamba hatuezi kujifungia katika mambo ya jadi. Inatubidi kuchukua mema katika mambo ya jadi na kutupa mambo mabaya, kwa mfano, ugandamizaji wa mwanamke. Mema hayo yataunganishwa na mema yatakayochaguliwa katika mambo ya kisasa, hivi jamii itapata kuendelea vizuri zaidi.

### 3.3.2. Maana ya uhuru na uhafifu wa taasisi za kigeni.

Jambo halisi linalowasumbua baadhi ya waandishi wa riwaya za kiafrika tangu mwaka 1960 ni lile la kihistoria : uhuru au ukombozi wa mwafrika. "Na ninasema kuwa kazi ya mtu mweusi ni kuandaa vilivyo ukombozi wake, tena siyo ukombozi wa hivi hivi tu". Anasema CESAIRE (14). Onyo hilo lilikusu-



diwa wale ambao wajibu wao ulikuwa kuikomboa Afrika. Swali ni kama hao viongozi wa Afrika walitambua mitego aliyowatega mkoloni ambaye hataki kutengana na makoloni yake barani Afrika. Bila shaka riwaya nyingi zilitungwa zikizingatia hali ya kisiasa baada ya uhuru na matukio ya uhuru huo. Maoni wanayoyatoa juu ya swala hilo ni mengi lakini yana mtazamo mmoja kimsingi : uhuru huo hauna maana dhahiri. Na mwandishi E. DONGALA (15) anaona kuwa kutokuwa na maana dhahiri kwa uhuru huo kunajitokeza katika umbo la Afrika lenyewe ambalo linafanana na kofi. Hivi likiweza kuwa na maana mbili : maana ya "moyo" yaani upendo au ushirikiano; na maana ya "ngumi" yaani ujeuri. Maana ya uhuru inakuwa hivyo yenye kutatanisha kufuatana na msimamo wa nchi zenyewe.

Mwandishi KEZILAHABI naye **analizungumzia** kwa kiasi fulani swala hilo. Kwake uhuru unazusha maswali, mashaka na tahadhari. Miaka imepita tangu nchi ipate uhuru, lakini bado hatuamini. Uhuru hauko kwa sababu umetangazwa tu, bali unahitaji mabadiliko mengi kimsingi. Lakini kama ijitokezavyo katika kitabu, ingawa uhuru umetangazwa bado kuna giza lile lile la nyakati za ukoloni. Ndiyo sababu tunawaona wahusika wengi wakilaumu vikali sana uhuru huo kwani wamegundua unafiki wake. Wanasikitishwa na kuchukizwa na matukio mabaya ya nyakati za uhuru kiasi cha kusema : afadhali ukoloni!

Swala hilo la uhuru linazungukwa na matatizo mengi ambayo mara kwa mara hayapati suluhisho. Uhuru ambao ulipokelewa kwa vigelegele na shangwe, sasa unazusha manung'uniko. Uhuru haukuleta mabadiliko wala mapinduzi ya kisiasa na kijamaa, ambayo yalikuwa yakitegemewa katika nchi za Afrika. Dalili mbalimbali zinaonyesha kuwa mambo yalibaki yale yale tangu "uhuru" upatikane. Mabadiliko ni ya juu juu kiasi ambacho mtu anaweza kusema labda, afadhali waafrika wasi-ngeomba uhuru huo kwa nguvu na kwa pupa. Kwani badala ya neema umeleta machafuko zaidi, upotofu wa jamii, udhalimu



wa kila aina, mambo ambayo hasa ni urithi kutoka kwa mkoloni.

Mwandishi anapotupa jicho nyuma na kutukumbusha makossa, udhalimu, na maovu ya mkoloni, anataka kutuonyesha kuwa hakuna mabadiliko ya kimsingi yaliyoletwa na uhuru. Masikitiko na manung'uniko waliyo nayo wahusika wa kitabu hiki ni kama yale yale ya nyakati za ukoloni. Ijapo nyakati za ukoloni ziliacha kumbukumbu mbaya, hakuna fungu la maneno wala mhusika anayesifu nyakati za uhuru katika kitabu hiki. Bali wanasikitishwa na kuwa hali itachafuka na jamii kuzama jalalani ikiwa hali inaendelea kama ilivyo sasa. Ukweli ni kwamba baada ya kutoa jasho lao la kupigania uhuru, mavuno wanayoyapata ni uonevu, udhia, fedheha, ufukara n.k. Mwandishi anaona kwamba utawala wa leo, kwa kisingizio cha kulitumikia taifa, unalitumikia tabaka la watu wachache.

Sio wazee tu wanaoshindwa kufaidi uhuru, hata na vijana waliopata kisomo cha juu wanalalamika kwani hawapewi vyeo au kazi inayolingana na kisomo chao. Mambosasa na Mamboleo, baada ya kufukuzwa kazini, tunawaona wakingoja kupewa kazi bila mafanikio. Wanapofanikiwa wanafanya kazi za chini, na mkuu wa Wilaya ambaye hakusoma anawachukia kiasi cha kuwafichia barua zinazowaita kazini.

Katika kitabu, Kezilahabi analaumu utawala wa nguvu, hasa nguvu za kipolisi. Ni kweli kuwa uhuru hauwezi kuzungumziwa katika nchi ambayo inatumia ukali na nguvu ili kuwafanya wananchi wafuate maazimio ya serikali. Kuwakusanya wananchi katika chama kimoja na kuwaadhibu wapinzani sio dalili ya uhuru.

Hata hivyo, mwandishi anaonyesha jinsi utawala mpya unavyozusha tabaka lenye nafuu, tabaka la makabaila wapya, tabaka ambalo kiini cha maisha yake ni pesa. Pesa zinakuwa na uwezo kwa kiasi fulani na watawala wanatumia vyeo vyao



kwa faida yao. Tabaka tawala linakusanya mali nyingi kwa pupa, hivi likiharibu uchumi wa Taifa na kuwafukarisha watu wa chini. Ingawa ndio vyombo vya uzalishaji mali. Na si jambo la ajabu kuwaona watu wanaokabiliwa na hali hiyo wakishutumiwa kwa sababu ya unafiki wao.

Mashtaka anayoyatoa mzee Chilongo juu ya wakati wa sasa, yaani wa uhuru, pamoja na lawama za kisiasa anazotoa Mambosasa, yote hayo yanapata misingi katika mvurugiko wa akili ambao ni matokeo ya ukosefu wa mazao yaliyokuwa yaki-tegemewa. Wanasumbuliwa na hawana usalama uliotegemewa. Malalamiko yao ni kama haya ya Ocot p'BITEK :

"Vyama vilipasua miji kama shoka lipasuavyo vichwa vitani. Huo ni umoja ulioahidiwa na uhuru ? Hiyo ni amani tuliyoletewa na uhuru ?"(16)

Swala la uhuru linaelezwa pengine katika muundo wa riwaya yenyewe ambao ni duara ama rudiorudio. Muundo huo unaonyesha hasara, ukosefu wa mabadiliko na maendeleo. Muundo huo wa mzunguko unamfungia mhusika na mawazo yake katika ulimwengu usio na mlango. Tunavyomwona mzee Chilongo mwanzoni mwa kitabu, ndivyo tumwonavyo mwishoni mwa kitabu; daima anapinga mambo mapya. Anabaki mkaidi. Tumwonavyo huko porini akiwatia moyo wenzake kupiga vita serikali, ndivyo tumwonavyo hospitalini akiwapiga wauguzi, ndivyo tumwonavyo mwishoni mwa hadithi akikataa kulitumia bomba la maji na kuendelea kuogea kisimani. Ni kweli kuwa mzee huyu anawakilisha kundi la watu ambao wanakataa maendeleo kwa ukaidi wao, watu ambao hawataki kuingiliwa na mambo mapya. Lakini anaweza tena kuwakilisha unyonge wa uwezo wa jamii katika kumbadili kifikra. Mwendo wake usiobadilika tangu mwanzo hadi mwisho unaweza kumaanisha hali ambayo haipigi hatua mbele. Ulimwengu wa mhusika unakuwa kama kizimba chenye minyororo ambamo kazi yake ni kurudiarudia mambo yale yale. Ni kusema kuwa hali ile ya nyakati za ukoloni ndiyo inaendelea kimsingi wakati wa uhuru.



Hivyo mwandishi anaonyesha kuwa uhuru hautapatikana kikamilifu ikiwa hakuna mapinduzi ya kimsingi. Barua wanazoandikiana Mambosasa ambaye hajapata kazi na Mamboleo ambaye ameshapata kazi zinaonyesha mahung'uniko yao wote wawili. Lakini hasa zinaonyesha ufumbuzi wa Mambosasa ambaye anaanza kuona mambo kama yalivyo, ilihali Mamboleo, mwangalifu na mwenye maarifa, tangu zamani alitambua hasara ya uhuru ijapo kelele na risala zenye upuuzi zilipigwa kuwa uhuru umepatikana. Ni kweli kuwa mapinduzi halisi yanahitaji busara na maarifa, sio kelele na ushupavu usiona akili.

Zaidi ya muundo duara wa riwaya, wingi wa mahali duni kitabuni unazidi kuonyesha ukosefu wa uhuru. Mkutano porini kwenye baridi, huko kwenye mkuu wa Wilaya chini ya jua kali, kule vijijini kwenye fitina na upotovu na penginepo, hakuna uhuru. Humo humo wanamofinywa watu, ndimo hata wakaidi wakali wanaposhindwa na nguvu za serikali. Tunaona, kwa mfano, jinsi Wana-Kisole, ambao wamejenga "chama" cha upinzani, wavyolipa ujasiri wao wa kutaka kushambulia utaratibu ulioamuriwa kufuatiliwa. Wanaadhibiwa kiasi ambacho "hawatagamea" tena serikali. Watavumilia tu hali ilivyo kuliko kwenda na kurushwa kichura huko bomani, kwani serikali si ya kuchezea. Kwao, ulimwengu unakuwa kama chombo cha kukaba kinachokatisha tamaa, kinachowatia watu katika uchungu mkubwa.

Hivi kitabu cha Gamba la nyoka kinaweza kuwa na mtazamo wenye kutoa uchungu unaowasilishwa na matokeo ya uhuru. Tunaona kuwa dhana mpya ya uhuru inawafarakisha binadamu. Ufafakisho huo kiakili na kijamii unawafikisha kwenye mvurugiko wa akili. Mikinzano, mashaka ya kiitikadi, uchungu wa kimaisha, yote hayo yanamkabili mwafrika na kumvunja moyo. Mfano maarufu wa vurugiko la akili ni kina Mambosasa. Alipopoteza cheo chake, Mambosasa anakuwa kama mwendawazimu. Anakataa kushiriki na nduguze. Tunamfuata akijiingiza katika makaribisho ya mabwana wa serikali na kurudi nyumbani akibeba masalia yao.



Kadhalika anawaza kumloga rafikiye Mamboleo. Mwendo huo unaonyesha kwa kiasi fulani ufumbuzi wa mhusika. Ni matokeo ya kuwa Mambosasa haambatani na ukweli wa mambo, wala nafasi yake - kama mtu aliyesoma. Kwani kila mwendo wa binadamu una maana yake, na ni lazima kuutafutia sababu na misingi katika matukio ya jamii.

Mvurugiko huo undtekea katika kudanganywa, uongo, unafiki. Kutokana na hasara ya uhuru, kutatokea miendo mbalimbali. Kuna wale ambao wanavumilia hali kwa woga, kuna wengine wanaolalamika na kunung'unika kwa hasira, halafu kuna wahalifu na waasi. Makundi hayo matatu tunayaona kitabuni. Lakini wawe wavumilivu, wahalifu au wakaidi, miendo yao haitafaidika katika ulimwengu huu wa kukabana. Wanakuwa kama vikaragosi ambavyo hufuatia njia vinayoamuriwa kufuata. Vikaragosi hivyo, baada ya kupinduliwa katika pande kadhaa, vitaona kuwa wimefanya kazi bure. Wanakuwa kama "Sisyphe"(17) wa uhuru. Kama vile Sisyphe hatafaulu kulisukuma jiwe mpaka juu ya mlima, vile vile wahusika wetu hawafaulu kuyapindua matukio ya uhuru ambao haukumilikiwa vilivyo. "Tulishindwa kufaidi matunda ya uhuru!" analalamika mnyonge mmoja.

Kwa kifupi, swala la uhuru katika riwaya hii, linaweza kukabiliwa kwa njia mbili : kwanza tunaweza kukabili njia ya asili yenyewe ya uhuru ambayo ni ya ajabu kutokana na matarajio yake ghoshi. Uhuru haukutimiza lengo lake la kumkomboa mtu mweusi. Pili, ulimwengu wa riwaya unaonyesha wahusika wa ajabu, wahusika wanaokata tamaa, wanaoshindwa na shughuli zao katika dunia inayowapinga : Mama Tinda anakufa, Chilongo hawezi kurudisha na kudumisha mambo ya jadi, Mambosasa anakuwa kama mtu ajishughulishaye na kuimarisha hali bora ya kijamii na kisiasa katika ulimwengu ambao haujui kanuni zake. Hakuna shaka kuwa nia yao ya kudumisha usawa na mapinduzi haiambatani na uwezo wao. Wanataka kuwa wakombozi katika dunia isiyowakubali na isiyowahitaji.



Pengine, taasisi zenyewe, hasa zile za kisiasa zinazotumiwa hazifai kwani zinatoka katika ulimwengu ambao mazingira yake yanatofautiana na yale ya kiafrika. Zaidi ya taasisi hizo kutolingana na mazingira, hatuna wataalam wazaliwa wa nchi za kiafrika ambao wangejaribu kuzinyoosha na kuziambatani nisha na mazingira. Baada ya mkoloni kufukuzwa vyeo vinagawanywa ghafla kwa watu ambao mara kwa mara hawana maarifa na uwezo wa kufanya kazi wanazopewa. Wanasisia nao wanachaguliwa na mkusanyiko wa watu ambao kwa jumla hawajui maana ya kura zao, kwani jambo hilo ni jipya kwao. Haraka tabaka la wenye vyeo linaundwa na unyonyaji unaendelea. Ugombeaji wa makazi unaanza kutokana na heshima na fahari ya kazi za serikali, ambayo ni urithi wa mkoloni.

Viongozi pia wanaongezeka : kwa mfano kuna mkuu wa kijiji, mkuu wa wilaya, mkuu wa mkoa n.k. Jambo hilo ambalo ni jipya barani Afrika linawavuruga mawazo wananchi. Wanyonyaji wanaongezeka na kuwafilisi wananchi. Swali ni la kujua kama jamii inayojengwa ni ya ujamaa au la. Ukweli ni kwamba jamii inayohusika kitabuni, ni jamii ya majaribio ya kuijenga nchi ya ujamaa, lakini inakutana na matatizo ya kawaida ya nchi zinazoendelea. Jambo la muhimu sio kutimiza kwa pupa ndoto ya ujamaa, bali ni kuwasaidia wananchi kujiepusha na hali ya umaskini na kuwapatia uwezo wa kuupiga vita utawala msonge ambao unawanyonya kwa kutumia kisingizio cha ujamaa na chama. Tena katika jamii za kiafrika, mambo mapya ambayo ni mazuri kwa kiasi fulani kama vile vijiji vya ujamaa yanahitaji kutolewa ufafanuzi na maelezo zaidi badala ya kuyaingiza kwa nguvu na fujo.

Riwaya hii inatuonyesha jinsi viongozi wabichi wanavyoweza kushindwa kutekeleza kisiasa maagizo yenye basara na kutumia mabavu. Kama asemavyo A.G. GIBBE



"Kezilahabi anaonyesha bayana kuwa viongozi wa ngazi za chini waliposhindwa kutekeleza kisiasa mwito wa kuwashauri na kuwahimiza wananchi kuanzisha vijiji vya ujamaa, walitumia vitisho, marungu na bunduki" (18).

Labada mtazamo wa Kezilahabi unaangalia misiba na majonzi tu na kuweka kando mazuri waliyoyafikia viongozi wa Afrika tangu uhuru upatikane, lakini anawaonya kuongeza **bidii na jitihada** katika kuimarisha uhuru kisiasa, kiuchumi, na kupigania haki za binadamu. Na mwandishi anaonyesha kuwa yote hayo yatafikiriwa kwa kutumia siasa ya ujamaa ambayo itarekebishwa kufuatana na mazingira ya wakati na mahali, ili kuleta mafanikio makubwa zaidi. Mwandishi anasisitiza kuwa ujamaa utashinda ikiwa unatumia kwa maarifa na busara. Imani yake ya ushindi wa ujamaa inaonekana katika kichwa chenyewe cha kitabu "Gamba la nyoka". Taswira hii ina maana kwamba matatizo ya kiutekelezaji na ya kiitikadi yanayojichipuza hapa na pale ni kama gamba la nyoka ambalo likiondolewa jamii ya kijamaa inayojengwa itakuwa imara.



TANBIHI

- (1) KIANGO, S.D., na SENGO, T.S.Y., Ndini zetu 2, I.T.L., Dar-es-Salaam katika Utangulizi
- (2) Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, O.U.P., Dar-es-Salaam, 1981, uk.151.
- (3) "Méthode particulière employée pour former et instruire les jeunes." Le Grand Larousse Encyclopédique Vol.4, Larousse, Paris, 1981.
- (4) "L'ensemble des actions et des influences exercées volontairement par un être humain sur un autre être humain, en principe par un adulte sur un jeune, et orientées vers un but qui consiste en la formation dans l'être jeune, des dispositions de toute espèce correspondant aux fins auxquelles, parvenu en maturité, il est destiné."  
HUBERT akikiriwa na ERNY, P., L'enfant et son milieu en Afrique Noire, Payot, Paris, 1972, uk. 15.
- (5) "En principe(...) la mère est la seule initiatrice dont l'intervention s'impose avec la force d'une loi naturelle. Elle seule, en effet, peut connaître assez intimement l'état physique et mental de sa fille pour savoir exactement le langage qu'il faut bien tenir et le moment où il est nécessaire de le tenir."  
LENDOUSSE, P., L'âme de l'adolescente, P.U.F., 1963, uk.56.
- (6) Waefeso 6:4.
- (7) Wakolosai 3:21.
- (8) TOPAN, F., Uchambuzi wa maandishi ya kiswahili 2, O.U.P., E.A. 1977, uk. 72.
- (9) KANE, G.H., L'aventure ambiguë, 10/18, Paris, 1972. ...  
ACHEBÉ, C., Things fall apart, Heinemann, London, 1958.  
BETTI, M., Ville cruelle, P.A., Paris, 1971.
- (10) MAO TSE TUNG akikiriwa na SENKORO katika makala yake "Mwamko wa kisiasa katika mashairi ya Shaban Robert" Mulika na.8, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Septemba 1976.
- (11) MALYANGU (au Mali-yangu) ni mhusika mkuu katika hadithi iliyotungwa na E. Kezilahabi katika gazeti la MZALENDO na.717, Jumapili, Aprili 7, 1985. Bwana huyo ambaye ni katibu mkuu anayakusanya maovu ya kila aina.
- (12) "KAKA MIYE" katika MZALENDO, Jumapili, Feb.17, 1985, uk.7.



- (13) "Tout change et nous devons vivre avec notre temps"  
RADIAN, S., Sous l'orage, P.A., Paris, 1963.
- (14) "Et je dis aussi que c'est la mission de l'homme de culture noire de préparer la bonne décolonisation et ce n'est pas n'importe quelle décolonisation."  
CESAIRE, A., "L'homme de culture et ses responsabilités" in Premiers jalons pour une politique de la culture, P.A., Paris, 1968; uk.38.
- (15) DONGALA, E., Un fusil dans la main un poème dans la poche, Albin MICHEL, Paris, 1973.
- (16) Ocot p'BITEK, Song of Lowino
- (17) Sisyphe ni mtu, katika ngano za kigriki, aliyelaaniwa kufikisha jiwe kubwa juu ya mlima kwa kulisukuma; lakini kamwe hakufanikiwa.
- (18) GIBBE, A.G., "Baadhi ya taswira katika Gamba la nyoka" Kiswahili, td 49/1, Machi, 1982.



HITIMISHO

Mwishoni mwa kazi hii, inafaa kuyazingatia kwa jumla yote tuliyayazungumzia na kutoa maoni juu ya swala lililokuwa liki-sudiwa kujibiwa. Kusudi la kazi hii lilikuwa la kuchambua nadharia ya kifungamano katika maandishi ya Kezilahabi kwa kutumia vitabu vyake vya Rosa Mistika, Kichomi na Gamba la nyoka. Kuchambua nadharia ya kifungamano, kama ituelezavyo fasili yenye-we ya ufungamano, hi kuchunguza kama mwandishi ametimiza lengo la fasihi ambayo inatakiwa kuwa kioo cha jamii. Ni kudadisi jinsi mwandishi alivyochunguza jamii yake, mazingira na hali ya jamii yake, jinsi anavyouchambua mwenendo fulani wa jamii na jinsi anavyotoa njia na suluhisho la matatizo yanayoikabili jamii yake.

Hitimisho hili litatokana na yanayozungumzwa katika maandishi ambayo hatuna budi kuambata, isha na mfumo wa jamii ambayo mwandishi anaongelea ili kuweza kutoa kauli juu ya ufungamano wake; kwani fasihi yenye kufungamana haina budi kuambatana na mkondo pamoja na misingi ya jamii ambayo fasihi hiyo inatumikia. Na hayo yanalandana na mbinu ya uhakiki iliyochaguliwa kutumiwa katika kazi hii yaani uhakiki wa kisosholo-jia ambao unakusudia kuonyesha jinsi maudhu ya fasihi yaonyeshavyo wazi aina ya jamii na mfumo wa jamii inayohusika kwa wakati maalum, uhusiano wa kitabaka katika jamii hiyo, na mambo kama vile uchumi, utamaduni na imani za watu.

Kama tulivyoona, mwandishi Kezilahabi ni mtungaji wa riwaya na mshairi, katika maandishi yake, anashughulikia kuumba jamii mpya kufuatana na matatizo yanayoikabili jamii yake. Mchoro ufuatao unajumlisha kwa kifupi mambo au dhamira kuu zinazojitokeza katika maandishi yake.



!	!	! Rosa Mistika!	! Kichomi!	! Gamba!	!
!	!	!	!	! la nyoka!	!
! Kupinga taasisi za kigeni	!	+	!	+	!
! Swala la ukale na usasa	!	+	!	+	!
! Mgongano wa utamaduni	!	+	!	+	!
! Kulilia mambo ya jadi	!	+	!	+	!
! Swala la kukosoa mifumo	!		!		!
! mbalimbali	!	+	!	+	!
! Kupinga ukoloni na ukoloni!	!		!		!
! mamboleo	!	-	!	+	!
! Kalaumu viongozi walioongo	!		!		!
! za baada ya uhuru	!	-	!	+	!
! Kupinga uhuru wa bendera	!	-	!	+	!
! Kupigania uhuru kusini mwa!	!		!		!
Afrika	!	-	!	+	!
! Ujamaa kama suluhisho la	!		!		!
! ujenzi wa jamii mpya	!	-	!	+	!
! Wazo la ujamaa kutoka juu	!	-	!	+	!

Mchoro huu unaonyesha kwa kiasi fulani tofauti iliyoko baina ya Rosa Mistika\* ni riwaya inayohusu upotofu wa jamii za kiafrika dhidi ya taasisi za kigeni; wakati Kichomi na Gamba la nyoka vinahusu hasa mambo ya kisiasa.

Katika Rosa Mistika, ambayo inahusu mgongano wa tamaduni, mwandishi anaonyesha jinsi mazingira (na siyo roho, fikra au wadilifu wake) yanavyoyenga mtu. Na anaonyesha jinsi taasisi za kigeni zilizokuja kutegua mfumo wa jamii ya kiafrika na watu wake. Swala linalojitokeza ni la kujua kama inafaa kutupilia mbali mambo ya jadi na kuyakimbilia ya kigeni? Swali Kilo ambalo linazungunzwa tena katika vitabu vyake

\* na vitabu vingine viwili. Tunaona kuwa Rosa Mistika



vingine kama utuonyeshavyo mchoro, mwandishi analitatusa kwa kushauri kuunganisha mambo ya jadi na mambo ya sasa kwa kuchunguza mazuri na kutupa mabaya, kwani kwa pande zote mbili kuna mabaya na mazuri. Ni kweli kuwa ulimwengu unaendelea na anafaa kuishi wakati tulio nao, lakini tena inatupasa kutojivunja misingi yetu ya asili, na tunatakiwa kujenga wakati wa sasa kwa kutumia baadhi ya vipengele vya jadi yetu na vile vya kigeni tukivambatanisha na mazingira na wakati.

Vitabu vya Kichomi na Gamba la nyoka kama uonyeshavyo mchoro, vinazungumzia matatizo ya kisiasa yenye uhusiano na ujenzi wa jamii mpya. Matatizo hayo ambayo hasa ni udhaifu wa viongozi, ukoloni mambao, ngongano wa wakati n.k., mwandishi anayakabili kwa kutumia kisa cha uanzishaji wa ujamaa nchini Tanzania. Mambo mengi yanayozungunziwa katika Kichomi, tunayakuta pia katika Gamba la nyoka.

Tatizo linalojitokeza katika Gamba la nyoka ni la kuanzisha vijiji vya ujamaa bila mpango na kutumia nguvu ambazo haziambatani na nia ya siasa ya ujamaa. Mwandishi anonyesha uovu wa tabaka tawala ambalo halielewi siasa litakayo kuimarisha, pamoja na unyonge wa watu wa kawaida ambao wanakwaji anywa uhuru wao. Kezilahabi anawahurumia na kuwatetea wanyonge na huku akiwahakiki na kuwakosoa waanzilishi wa siasa ya Ujamaa na kujitegemea.

Mambo anayozungunzia katika kitabu hicho hakuna shaka kuwa yanambatanana na yake tuliyoyaona katika kurasa zilizotagulia kuhusu historia na hali ya kisiasa ya Tanzania, tunaona kwamba mwandishi amechukua mengi kutokana na mazingira yake. Khusu ujenzi wa vijiji vya ujamaa, URFER anatueleza baadhi ya matatizo yaliyotokea kama ifuatavyo:

"Toka mwezi Agosti mpaka mwezi Novemba mwaka wa 1974, kimbunga kiliangukia nchi na maelfu ya watu walihamishwa kwa nguvu siku hadi siku, kupelekwa mashambani ambapo palikusudiwa kujengwa vijiji vya ujamaa. Mahali pengi, jeshi lilishirikishwa katika kuwashika watu na kuwahamisha kwa silaha. Mwezi Oktoba, nchi



ilionekana kama kwamba imo katika mapinduzi makubwa : kando ya barabara vilikuwa vimejengwa vijumba vibovu vya nyasi."(1)

Pia tunasoma katika Daily News ya tarehe ya 4 Octoba 1974, kuwa

"Watu waliamishwa kwa wingi, bila ya mpango wowote wa jinsi watavyoishi mahali papya (...) Watu wali-chukuliwa kwa nguvu kutoka vijiji vyao na kutupiliwa porini, pale ambapo palitegemewa kujengwa vijiji vyenye mpango maalum; viongozi walizidi kipimo katika ushupavu wao na hawakujihadhari vilivyo." (2)

René DUMONT mwandishi wa Afrika inakwenda kombo, anatupa maelezo zaidi katika maneno yafuatayo aliyemtotea mwanasiasa fulani wa Tanzania katika mahojiano:

"Mkulima hana neno, kwani anagandamizwa na serikali, na hatufanyi lolote la kumhimiza. Tungaliwashiriki-sha kwa uaminifu, watu wanalitueleza matatizo yao. Lakini njia tulizotumia ni kama zile za ukoloni; hali ya kuwapeleka watu vijijini ni ile ya mkoloni; na wananchi hawatwambii lolote kwani wanatulinganisha na nguvu za serikali. Tunawalazimisha mambo mengi kiasi ambacho wanastahabu kutojali kitu. Hiyo ndiyo labda njia yao ya kuishi. Mwendo huo unapaswa kure-kebishwa kwa pande zote mbili."(3)

Yote hayo yanatueleza kuwa mambo aliyoyazungumzia Kezilahabi ni ya kweli. Hivi analitimiza lengo la fasihi la kuambatanisha maandishi na matukio ya jamii inayohusika. Ni kusema kwamba mwandishi aliandika akisumbuliwa na hali hiyo ambayo anaitaka ibadilike. Na anapinga hali hiyo kwa ujasiri. Si kama waandishi "wengine ambao wakiandika utadhani kuwa Tanzania ya leo ni pepo ya ujamaa ambamo hama matabaka, hama unyonyaji na unyonywaji."(4) Kezilahabi anajua kuwa kuficha ubaya wa mambo ni kuzuri kwa wakati wake, mazingira yake na jamii yake, lakini kufichua ukweli wa jambo ni kuzuri zaidi, kwani mtu, ingawa anaumia, ataelewa kwa nini anaumia. Na hapa tunagundua upande mwingine wa ufungamano wake. Inapasa sasa kujua ni nani anayeandikiwa, na athari ya kazi zake juu ya jamii, ili kupata ufungamano wake kamili.



Katika mahojiano yake na BERNANDER(5) Kezilahabi anaeleza kuwa anawaandikia wakulima. Ni kweli kuwa anatumia lugha ya Kiswahili katika maandishi yake; na tunajua kuwa lugha inaweza kuwa kielelezo cha ufungamano kwani lugha ni chombo cha mawasiliano, misingi ya utamaduni na hisi za bi-nadamu, hivi ikirahisisha kumfikishia mtu ujumbe kwa kutumia lugha yake. Lakini jambo hili linahitaji uchunguzi ili kujua ni wakulima wangapi wanaojua kusoma na wanaoweza katika jiografia andishi ya Kezilahabi. Kama tulivyoelezwa katika majadiliano ya Tanzania, wataanzania wanaojua kusoma bado ni wachache sana nchini. Tena wengi hawafahamu Kiswahili.

Ukweli ni kwamba anaandika juu ya wakulima. Na anapozungumzia maovu yanayoikabili jamii yake, hasa akihaki-ki mwenendo wa viongozi, si kusema kwamba anapinga nchi yake wala kuiona nchi yake katika njia mbaya, bali ana-waita watu kufikiria suluhisho fulani la mambo, na anataka kuwa wale waliomsoma wajiepushe na ule mwenendo wa wale wali-owatangulia. Mwandishi anawaandikia wanyonge na wanyonyaji, na anawaonyesha kuwa ushirikiano wa matabaka hayo ndio utaka-enga jamii mpya. Hapo tunapata msimamo wake timamu juu ya wa jamii mpya nchini Tanzania na hata Afrika nzima; di ya kuwa mtanzania, Kezilahabi ni mwafrika anaye- tapo la waandishi wa baada ya uhuru. Na tunajua wa tapo hilo wanazungumzia utawala uliotokea da ya uhu ujenzi wa jamii mpya.

Basi itikadi ya Kezilahabi ni ya kikulima yenye ani ubepari. Anaona kuwa mfumo wa kibepari si pepo du- , bali umejaa vurugu na maovu mengi. Hivi anaamua ekeza siasa ya ujamaa ambayo inatakiwa kutumiwa kwa

kuwa mwanachama na wakati na mahali yaani na

liiza  
lahabi unatufanyakadi kama



itikadi katika ujenzi wa jamii mpya barani Afrika. Raia wanatakiwa kushirikishwa katika mambo yanayowahusu. Wanatakiwa kuandaliwa kisiasa. Kwa kufanya hivyo wataweza kushughulikia maendeleo yao bila tatizo. Viongozi nao wanatakiwa kuwa wenye maarifa na mabingwa wa siasa wanayoiendesha. Inawapasa mambo yote kwa itikadi kwa utaratibu na busara, na kutobwambia mambo yote kwa pamoja. Wajue kuwa "Haba na haba hujaza kibaba" kama wasemavyo wawahili, "mwendapole huvuka maji ya nguvu; kwani kama asemavyo Kezilahabi, "masikio, pembe huota baadaye." ( 7 )  
Ni kweli kuwa mbinu zinazotumiwa ni mpya kwa kiasi fulani na zaziambatani na mazingira. Kwa hiyo zinahitaji maelezo zaidi.

Ni vigumu kuamua mfumo unaofaa kwa nchi za kiafrika kutokana na matatizo mbalimbali. Tatizo muhimu ni umaskini wa kiafrika. Umaskini huo, nchi za kiafrika za mifumo ya kisiasa ya kutunyonya tu. Pengine ni kutusaidia hali nia yao ni kutunyonya tu. Pengine ni umaskini huo, hata wale viongozi wanaoamua kuisiasa ya ujamaa wanashindwa; kwani wanashughulikia mdeleza uchumi ambao bado uko nyuma.

Hata hivyo, Kezilahabi amefaulu kujishughulisha na kuwa akiandikia kufuatana na mambo mbalimbali amaduni, utetezi wa haki za binadamu, athari ya jamii na hata rama ya kujenga jamii mpya. Amesha vile ambavyo aliweza kuitumia chombo cha jamii jamii na dira ya kukiielekeza kutoa makosa kwa jamii. Kwani mwamko wa mwandishi si kutoa makosa kama penye uovu tu, bali kusaidia umma katika goro na mtatizo yake.

amekuwa na shida ya kupata vitabu vya maendeleo wa mada iliyokuwa ikihusika, hata hivyo hizi makusudi yangu ambayo yalikuwa ni



kuchambua nadharia ya kifungamano katika maandishi ya kezilahabi kwa kutumia mbinu ya kisosholojia. Ni kweli kuwa kazi ya sanaa inaweza kuwa na mitazamo mbalimbali; ni kusema kwamba hakuna mhakiki awezaye kujidai kuzingatia kwa utimilifu ujumbe wote uliomo katika kazi fulani.

Nona kwamba uko uwezekano mkubwa sana kwa upande wa wahakiki watakaofuata kuendeleza uhakiki wa kazi za Kezilahabi kwa kutumia mitazamo mingine ya nadharia za uchambuzi kama zinavyopendekezwa na wataalamu mbalimbali. Namalizia kwa kusema kuwa "Kuzima koleo sio mwisho wa uhunzi."



TANBIHI

(1) "Entre Août et Novembre, un véritable raz de marée défer-  
la sur le pays, et des millions de personnes se virent  
autoritairement transférées, parfois du jour au lendemain,  
sur des espaces en friche dont ils devaient faire leurs  
villages et leurs champs. En maints endroits, l'armée  
fut mise à contribution pour mettre Courant Octobre, le  
pas et les démenager manu d'un militaire. les récalcitrants au  
pays et semblait sortir bien que mal alignés, se succédaient  
des routes tant que mal alignés, se succédaient  
de misérables huttes de branchage."

URFER, S, Une Afrique socialiste, la Tanzanie, Ed. Sociales,  
Paris 1976

"Le Daily News (...) parle de populations déplacées, sans  
qu'ait été étudiée la manière dont elles pourraient  
organiser leurs nouvelles terres (...) des arrachés  
leurs villages pour être installés des villages pleine brousse,  
où devaient être enthousiastes ont dépassé la mesure, n'ont  
dirigeants pris les précautions suffisantes."

News du 4 oct. 1974 ikikiriwa na  
René, L'Afrique étranglée, Seuil, Coll. Histoire  
Immédiate, Paris 1980 uk 131

op.cit, uk. 144.  
M.M. "Ushairi na Kiswahili Sept. 1977

"Ezekiel (1) Kazilahabi, Narrator of Modern  
Tanzania" katika jarida la LUGHA, Vol I  
(University of Uppsala, Sweden 1977. UK.49  
M.M. "Dunia  
kikiriwa na fujo" Kiswahili tol. 50/1 TUKI  
Dar es Salaam 1983

mba la nyoka, E.A.P., Arusha 1979, UK 147



MAREJEO

- ANOZIE, S.O.,  
Sociologie du roman africain, Aubier, Paris, 1970.
- BADIAN, S.,  
Sous l'orage, Présence Africaine, Paris, 1963.
- BARTHES, R.,  
Le degré zéro de l'écriture, Coll. Points,  
Ed. Seuil, Paris, 1975.
- ..., Y.,  
Indépendances africaines, idéologies et réalités I,  
Maspero, Paris, 1975.
- ..., A.,  
Discours sur le colonialisme, Présence Africaine,  
Paris, 1970.
- J.,  
Littérature nègre, Armand Colin, Paris, 1974.
- ...,  
Littérature et son peuple comme producteur de civilisation,  
Actes du Colloque de Yaoundé du 16-20 Avril,  
Présence Africaine, Paris, 1977.
- ...,  
Reception des littératures négro-africaines, Colloque  
tenu à l'Université de la Sorbonne Nouvelle  
les 10 et 11 mars 1978, in Afrique Littéraire  
et Artistique n°50.
- ...,  
La composition et les genres littéraires,  
Wesmael-Charlier, Namur, 1965.
- ...,  
L'Afrique noire est mal partie, Seuil,  
Paris, 1962.
- ...,  
L'Afrique étranglée, Coll. Histoire  
d'Afrique, Seuil, Paris, 1980.
- ...,  
L'Afrique et son milieu en Afrique noire,  
P.U.F., Paris, 1971.
- ...,  
Masques blancs, Seuil, Paris, 1965.
- ...,  
Littérature, Armand Colin, Paris,  
Paris, 1972.
- ...,  
"Maswira katika Gamba la nyoka"  
49/1, TUKI, Machi 1982.
- ...,  
L'humanité, Coll. Idées,  
Paris, 1970.



Katika mahojiano yake na BERNANDER(5) Kezilahabi anaeleza kuwa anawaandikia wakulima. Ni kweli kuwa anatumia lugha ya Kiswahili katika maandishi yake; na tunajua kuwa lugha inaweza kuwa kielelezo cha ufungamano kwani lugha ni chombo cha mawasiliano, misingi ya utamaduni na hisi za binadamu, hivi ikirahisisha kumfikishia mtu ujumbe kwa kutumia lugha yake. Lakini jambo hili linahitaji uchunguzi ili kujua ni wakulima wangapi wanaojua kusoma na wanaoweza kusoma maandishi ya Kezilahabi. Kama tulivyoielezwa katika jiografia ya Tanzania, wataanzania wanaojua kusoma bado ni wachache sana nchini. Tena wengi hawafahamu Kiswahili.

Ukweli ni kwamba anaandika juu ya wakulima. Na anapozungumzia maovu yanayoikabili jamii yake, hasa akihaki-ki mwenendo potovu wa viongozi, si kusema kwamba anapinga nchi yake wala kuiona nchi yake katika njia mbaya, bali anawaita watu kufikiria suluhisho fulani la mambo, na anataka kuwa wale waliomsoma wajiepushe na ule mwenendo wa wale waliowatangulia. Mwandishi anawaandikia wanyonge na wanyonyaji, na anawaonyesha kuwa ushirikiano wa matabaka hayo ndio utaka- ojenga jamii mpya. Hapo tunapata msimamo wake timamu juu ya ujenzi wa jamii mpya nchini Tanzania na hata Afrika nzima; kwani zaidi ya kuwa mtanzania, Kezilahabi ni mwafrika anayewekwa katika tapo la waandishi wa baada ya uhuru. Na tunajua kuwa waandishi wa tapo hilo wanazungumzia utawala uliotokea baada ya uhuru na ujenzi wa jamii mpya.

Basi itikadi ya Kezilahabi ni ya kikulima yenye kulaani ubepari. Anaona kuwa mfumo wa kibepari si pepo duniani, bali umejaa vurugu na maovu mengi. Hivi anaamua kupendekeza siasa ya ujamaa ambayo inatakiwa kutumiwa kwa busara na maarifa kufuatana na wakati na mahali yaani na mazingira.

Msimamo huo wa Kezilahabi unatufanya kujiuliza juu ya kazi ya raia, kazi ya viongozi na ya itikadi kama



kuchambua nadharia ya kifungamano katika maandishi ya kezilahabi kwa kutumia mbinu ya kisosholojia. Ni kweli kuwa kazi ya sanaa inaweza kuwa na mitazamo mbalimbali; ni kusema kwamba hakuna mhakiki awezaye kujidai kuzingatia kwa utimili-fu ujumbe wote uliomo katika kazi fulani.

Naona kwamba uko uwezekano mkubwa sana kwa upande wa wahakiki watakaofuata kuendeleza uhakiki wa kazi za Kezilahabi kwa kutumia mitazamo mingine ya nadharia za uchambuzi kama zinavyopendekezwa na wataalamu mbalimbali. Namalizia kwa kusema kuwa "Kuzima koleo sio mwisho wa uhunzi."



MAREJEO

- ANOZIE, S.O., Sociologie du roman africain, Aubier, Paris, 1970.
- BADIAN, S., Sous l'orage, Présence Africaine, Paris, 1963.
- BARTHES, R., Le degré zéro de l'écriture, Coll. Points, Ed. Seuil, Paris, 1975.
- BENOT, Y., Indépendances africaines, idéologies et réalités I, Maspero, Paris, 1975.
- CESAIRE, A., Discours sur le colonialisme, Présence Africaine, Paris, 1970.
- CHEVRIER, J., Littérature nègre, Armand Colin, Paris, 1974.
- Critique africain et son peuple comme producteur de civilisation, Actes du Colloque de Yaoundé du 16-20 Avril, Présence Africaine, Paris, 1977.
- Critique et réception des littératures négro-africaines, Colloque tenu à l'Université de la Sorbonne Nouvelle les 10 et 11 mars 1978, in Afrique Littéraire et Artistique n°50.
- DOUTREPONT, C., La composition et les genres littéraires, Wesmael-Charlier, Namur, 1965.
- R., L'Afrique noire est mal partie, Seuil, Paris, 1962.
- et MOTTIN, M.F., L'Afrique étranglée, Coll. Histoire Immédiate, Seuil, Paris, 1980.
- LELIEU, Le socialisme, P.U.F., Paris, 1971.
- ERNY, P., L'enfant et son milieu en Afrique noire, Payot, Paris, 1972.
- FANON, F., Peaux noires, masques blancs, Seuil, Paris, 1965.
- FAYOLLE, R., La critique littéraire, Armand Colin, Paris, 1964.
- GIBBE, G.A., "Baadhi ya : Haswira katika Gamba la nyoka" Kiswahili, vol. 49/1, TUKI, Machi 1982.
- GOLDMANN, L., Marxisme et sciences humaines, Coll. Idées, Ed. Gallimard, Paris, 1970.



TANBIHI

- (1) "Entre Août et Novembre, un véritable raz de marée déferla sur le pays, et des millions de personnes se virent autoritairement transférées, parfois du jour au lendemain, sur des espaces en friche dont ils devaient faire leurs villages et leurs champs. En maints endroits, l'armée fut mise à contribution pour mettre les récalcitrants au pas et les démenager manu militari. Courant Octobre, le pays semblait sortir d'un cataclysme national: le long des routes tant bien que mal alignées, se succédaient de misérables huttes de branchage."

URFER, S, Une Afrique socialiste, La Tanzanie, Ed. Sociales, Paris 1976

- (2) "Le Daily News (...) parle de populations déplacées, sans qu'ait été étudiée la manière dont elles pourraient s'organiser sur leurs nouvelles terres (...) des arrachés à leurs villages pour être abandonnés en pleine brousse, là où devaient être installés des villages planifiés (...) des dirigeants enthousiastes ont dépassé la mesure, n'ont pas pris les précautions suffisantes."

Daily News du 4 oct. 1974 ikikiriwa na

DUMONT, René, L'Afrique étranglée, Seuil, Coll. Histoire Immédiate, Paris 1980 uk 131

- (3) DUMONT, R, op.cit, uk. 144.

- (4) MULOKOZI, M.M. "Ushairi na *Ukashuku*" Kiswahili tol/47/2  
TUKI Dar-es-salaam Sept. 1977

- (5) BERNANDER, L, "Ezekiel (!) Kezilahabi, Narrator of Modern Tanzania" katika jarida la LUGHA, Vol I (University of Uppsala, Sweden 1977. UK.49  
akikiriwa na Mulokozi M.M. "Dunia uwanja wa fujo" Kiswahili tol. 50/1 TUKI Dar es Salaam 1983

- (7) KEZILAHABI, E, Gamba la nyoka, E.A.P., Arusha 1979, UK 147



- Pour une sociologie du roman, Coll. Idées, Gallimard, Paris, 1964.
- HARELIMANA, P.C., La politique et les politiciens dans "Violent était le vent" et "Les malheurs de Tchakô" de Charles NOKAN, mémoire de fin de 1er cycle, Ruhengeri, mai 1983 (inédit).
- HUSSEIN, E., -Mashetani, O.U.P., Nairobi, 1976.  
-Wakati ukuta, E.A.P.H., Dar-es-Salaam, 1971.
- KANDORO, S.A., Mashairi ya Sadaan, Mwananchi Publishing, Da-es-Salaam, 1972.
- KANE, C.H., L'aventure ambiguë, 10/18, Paris, 1972.
- KEMP, P., Théorie de l'engagement I: pathétique de l'engagement, Seuil, Paris, 1973.
- KESTELOOT, L., Anthologie négro-africaine, Marabout Université, Paris, 1967.
- KIANGO, S. na SENGO, T.S.Y., "Fasihi" Mulika, na<sup>2</sup> Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam.  
-Hisi zetu 1, Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam, 1973.  
-Ndimi zetu 2, L.T.L., Dar-es-Salaam, 1975.
- KI-ZERBO, J., Histoire de l'Afrique d'hier à demain, Hatier, Paris, 1972.
- KOUROUMA, A., Les soleils des indépendances, Seuil, Paris, 1970.
- LANDSBERG, P.L., Problèmes de personnalisme, Seuil, Paris, 1952.  
Mashairi ya "Mambo leo", kitabu cha kwanza na cha pili, The Sheldon, Press, London, 1975.
- MAKWARD, E., Is there an African approach to African literature? A.S.A., New York, 1968.
- MARCEL, G., Le journal métaphysique, 1928.
- MENDOUSSE, P., L'âme de l'adolescente, P.U.F., Paris, 1963.
- MHINA, G.A., Mtu ni utu, T.P.H., Dar-es-Salaam, 1977.
- MINYONO M'KODO, M., Comprendre "Le vieux nègre et la médaille" de F. OYONO, Ed. Saint-Sy les-Moulineaux, Paris, 1978.



- MNYAMPALA, M.E., Ngonjera za ukuta, O.U.P., Dar-es-Salaam, 1974.
- MOUNIER, E., Le manifeste, 1938.
- MOURALIS, B., Individu et collectivité dans le roman negro-africain d'expression française, Fayard, Paris 1972.
- MULOKOZI, M.M., -"Ushairi na Ukasuku", Kiswahili, tol.47/2, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam, Septemba 1977.
- "Dunia uwanja wa fujo", Kiswahili, tol.50/1 Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam, Machi 1983.
- NDUNGURU, Kanuni na Mbinu za kufundishia, E.A.P.L., Arusha, 1979.
- NEMEYABAHIZI, D., Pour une approche sociologique du roman: Un fusil dans la main un poème dans la poche, mémoire de licence, U.N.R., Ruhengeri, 1982.
- NKASHAMA, N.P., Comprendre la littérature africaine écrite en langue française, Ed. Saint-Paul, Issy les-Moulineaux, 1979.
- N'KRUMAH, Y., Le consciencisme, Présence Africaine, 1976.
- NYERERE, J.K., Socialisme, démocratie et unité africaine, Présence Africaine, Paris, 1970.
- OHLY, R., Agressive prose, a case study in Kiswahili prose of the Seventies, Institute of Kiswahili Research, Dar-es-Salaam, 1981.
- PALMER, C., An introduction to the African Novel, C.K. Heinmann, London, 1972.
- PAOLI, P., L'Afrique des Grands lacs, Seghers, Paris, 1978.
- RAMADHAN, J.A., "Fasili ya Kiswahili" Mulika, na.2, Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam.
- RUMBU-a-KAYIMBU, "Problématique de la critique littéraire contemporaine" in La Sémiologie et la littérature africaine, Actes du Colloque tenu à Lubumbashi, Mars 1977, Edité par le Centre d'Etudes des Littératures Africaines (C.E.L.A.)



- SARTRE, J.P., Qu'est-ce que la littérature? Coll. Idées, Ed. Gallimard, Paris, 1948.
- SENGHOR, L.S., Anthologie de la nouvelle poésie africaine et malgache, P.U.F., Paris, 1948.
- Liberté I, Négritude et Humanisme, Seuil, Paris, 1964.
- SENKORO, F.E.M.K., "Mwanko wa kisiasa katika mashairi ya Shabaan Robert" Mulika, na.8, Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam, 1976.
- THOMAS, L.V., Le socialisme et l'Afrique, Coll. Le Livre Africain, Paris, 1966.
- TOPAN, F., Uchambuzi wa maandishi ya Kiswahili 2, O.U.P., E.A., 1977.
- TOURE, A.S., L'Afrique et la révolution, Présence Africaine, Paris, s.d.
- YAHYA, Masaibu ya ndugu Jero, (Mchezo wa Wole SOYINKA) O.U.P., Dar-es-Salaam, 1976.
- ZERAPPA, M., Roman et société, Coll. Sup. P.U.F., Paris 1976.



YALIYOMO

0. UTANGULIZI .....	1
0.1. Madhumuni ya kazi .....	1
0.2. Umuhimu wa kazi .....	2
0.3. Mbinu za uhakiki .....	2
0.3.1. Bourgeois Criticism .....	6
0.3.2. Marxist Criticism .....	7
0.3.3. Socio-criticism .....	8
TANBIHI .....	10
1. NADHARA YA KIFUNGAMANO NA FASIHI YA KIAFRIKA .....	12
1.1 Nadharia ya kifungamano .....	12
1.1.1. Ufungamano kama mwenendo .....	13
1.1.2. Ufungamano kama kitendo .....	14
1.2. Ufungamano katika fasihi .....	15
1.3. Ufungamano katika fasihi ya kiafrika .....	20
1.3.1. Ufungamano katika fasihi ya Afrika ya Mashariki .....	26
TANBIHI .....	31
2. JAMII NA MAANDISHI YA KEZILAHABI .....	34
2.1. Nchi ya Tanzania .....	35
2.1.1. Jiografia .....	35
2.1.2. Historia .....	36
2.1.3. Hali ya kisiasa tangu 1964 .....	40
2.1.4. Hali ya kiuchumi .....	41
2.2. Muhtasari wa kazi zinazohusika .....	41
2.2.1. "Rosa Mistika" .....	41
2.2.2. "Kichomi" .....	42
2.2.3. "Gamba la nyoka" .....	43
1.3. Ufungamano katika fasihi ya Afrika ya Mashariki .....	26



TANBIHI .....	44
3. DHAMIRA .....	45
3.1. Mgongano wa utamaduni katika	
"Rosa Mistika".....	45
3.1.1. Tatizo la malezi .....	46
3.1.2. Dhamira zingine .....	54
3.2. Dhamira katika "Kichomi".....	58
3.2.1. Iwanko wa kisiasa .....	59
3.2.1.1. Ukoloni .....	59
3.2.1.2. Uhuru .....	61
3.2.1.3. Ujamaa .....	65
3.2.2. Khusu jamii .....	68
3.2.3. Ihana ya maisha .....	70
3.3. Dhamira katika Gamba la nyoka .....	71
3.3.1. Kuanzisha vijiji vya ujamaa .....	72
a) Kuhusu utumiaji wa nguvu .....	72
b) Kuhusu demokrasia .....	74
c) Dhuluma .....	74
d) Udhafu wa wiongozi .....	76
e) Unafiki .....	78
3.3.1.2. Matatizo .....	79
a) Ukoloni mamboleo .....	79
b) Mgongano wa wakati .....	81
3.3.2. Ihana ya uhuru na uhafifi wa	
taasisi ya kigeni .....	82
TANBIHI .....	90
HITILISHO .....	92
TANBIHI .....	99
MAREJEO .....	100
YALIYOMO .....	104